# *Kufunuliwa Kwa Mungu*

Na tubaki tumesimama kwa dakika moja wakati tukiinamisha vichwa vyetu kwa maombi.

2 Bwana wetu mwenye Neema, kwa kweli leo tunashukuru kwa ajili ya majaliwa haya tuliyo nayo ya kukusanyika pamoja juu ya nchi kabla ya kule Kuja kwa Bwana. Jalia tuichunguze mioyo yetu leo, kwa Neno Lako, na tuone kama tuko katika Imani, tupate kuwa tayari, ili, ile saa ya Kuonekana Kwake. Tupate kuwa kama vile Maandiko yamesema ingekuwa, "Kutwaliwa pamoja, pamoja na wale waliolala, na kumlaki Bwana hewani, na milele tuwe pamoja Naye."

3 Tunakushukuru kwa ajili ya Roho ya kweli ya Ukristo ambayo ingali ulimwenguni, miongoni mwa watu, kwamba wangali wanakuamini Wewe na Neno Lako. Kwa hiyo tunaomba baraka Zako juu yetu leo, kwamba utatumiminia kila mmoja wetu kile tunachohitaji, tupate kumwagiliwa maji kwa Neno, kusudi tuweze kukua tuwe vyombo vya kutumiwa mikononi Mwako, kwa ajili ya siku hii ya mwisho. Kwa kuwa tunaomba haya katika Jina la Bwana Yesu Kristo, Mchungaji wetu mkuu, ambaye tunamtarajia kutokea. Amina.

Mwaweza kuketi.

4 Nami ninataka kusema ya kwamba ninaihesabu hii kuwa ni upendeleo mkubwa asubuhi hii wa kuwa hapa tena. Na samahani ya kwamba hatuna nafasi ya kutosha kuketi. Nasi tutajaribu, usiku wa leo, sasa kufanya maombi kwa ajili ya wagonjwa; leo, asubuhi hii, ingekuwa ni vigumu kidogo.

5 Na—na nilikuwa ninaenda kuurekodi Ujumbe huu kwenye kanda leo. Mimi . . .Bwana alionekana kuniongoza juu ya jambo hilo, loo, mwezi mmoja ama miwili iliyopita, na ni muda mrefu. Na sina wakati huko nje mikutanoni, kwa sababu tunaipa hiyo dakika thelathini, arobaini za ibada. Na halafu tunaninii . . . Kwa sababu ya watu kulazimika kwenda kazini na kadhalika, niliona kwamba ni bora zaidi kama nikifupisha Jumbe zangu. Nao hawakuwa na wakati huko kuurekodi, kwa hiyo nilifikiria nitangojea tu mpaka nitakapokuja hapa maskanini halafu nirekodi kutoka hapa. Nao ni mrefu kidogo, na ninajua mnasimama, na ni—nitaharakisha upesi tu niwezavyo. Na, sasa, hamtanisumbua kama mnabadilishana viti, ama chochote kile, hilo litakuwa—hilo litakuwa ni sawa kabisa kwangu kwa maana hii ni siku maalum ambapo tunafanya tu huku kurekodi.

6 Na kwa hiyo tuna taarifa kuu za yale Bwana amefanya huko nje hudumani, ila labda tutatoa hayo zaidi sana usiku wa leo wakati tunapoweza kutoa wakati mwingi kwa ajili yake, kuwa na wakati mwingi wa kutoa.

7 Na sasa tunatumaini ya kwamba Bwana atambariki kila mmoja wenu. Ninajua mioyo yenu imejaa shangwe, mkikutazamia kule Kuja kwa Bwana. Na wangu pia, unabubujika zaidi, kuona mambo yakitukia jinsi yanavyotukia. Na—na mizozo ya kitaifa, na kanisa katika hali lililomo, na kuona ishara za Kuja Kwake, kimwili na kiroho pia, na kujua ya kwamba wakati huu wa Kuonekana Kwake uko karibu sana, kunaijaza tu mioyo yetu kwa furaha kujua ya kwamba tutabadilishwa moja ya siku hizi. Tutabadilishwa kutokana na viumbe hivi tulivyo.

8 Sasa, ninaamini, kama nikielewa, wana mawasiliano ya simu mahali fulani, kwamba Ujumbe huu unaenda huko Phoenix na—na mahali mbali mbali, kwa simu. Na kwa hiyo sasa tunatumaini ya kwamba kama ndivyo ilivyo . . . sijui; niliambiwa tu hilo kabla sijaingia. Na—na watu wote huko nje wanafurahia afya nzuri na—na Utukufu wa Bwana juu yao.

9 Na sasa—sasa tutalifungua Neno la Bwana. Na kile kilichotuleta hapa sisi sote ni kujifurahisha na kujua sisi ni nani . . . Ha—hatuji hapa na tunaninii . . . Hakuna mtu aliyepo anayejua ya kwamba mtu yeyote angeketi kwenye joto hili namna hii, na kwa wazo tu la kuwa hapa. Tupo hapa kwa kusudi moja, na hilo ni, "kutembea karibu zaidi na Mungu." Hilo tu ndilo tuwezalo kufanya, ni kuamini Bwana Yesu yu pamoja nasi. Nasi tupo hapa ku—kutembea karibu zaidi na Yeye.

10 Sasa joto hili ni kali kidogo kwangu. Kwa namna fulani nilizoea lile joto kavu huko Tucson, ambalo ni . . . Unyevu hapa sasa; joto letu kule ni kali zaidi kuliko hili, bali ni kavu. Unyevu wetu wakati mwingine ni sehemu moja ya ishirini ya asilimia moja, labda, kitu kama hicho, ni kama tu kuishi chini ya hema la oksijeni. Lakini hapa ina u—u—unyevu ndani yake, na inakufanya kwa namna fulani kujisikia tu "umekamuliwa kabisa," kama tulivyozoea kuliita. Kwa hiyo inakuchosha, kwa hiyo ninajua jambo hilo, na ninyi akina mama mlio na watoto wachanga na ninyi watu mnaosimama, wazee kwa vijana, na kuwekwa pamoja kama mlivyo. Na sasa tuna—tunatumaini ya kwamba Mungu atawatunukia sana kwa kujitolea kwenu.

11 Ninasikia ya kwamba Ndugu Roy Borders yuko hapa mahali fulani. Nilisikia akitangazwa, lakini nadhani labda asingeweza kuingia. Vema. Huyo ndiye meneja wa mikutano.

12 Kwa hiyo sasa sisi pia tunataka kutangaza ya kwamba mmoja aliyekuwa miongoni mwetu alienda kuwa pamoja na Bwana asubuhi hii, mwanamume, Ndugu Jackson kutoka Sturgis, Michigan. Hakuna mtu anayejua jinsi alivyoenda ama chochote kile kuhusu jambo hilo. Alikuwa mzima tu, naye alininii tu . . . Nafikiri walimkuta amekufa, ama kitu fulani. Si—sikupata utondoti wake wote. Nasi tunamshukuru Mungu sana ya kwamba Ndugu Jackson alikuwa ni Mkristo. Sijamwona kwa

miaka kadhaa, bali aliketi miongoni mwetu naye ni mmoja wetu. Mungu na aipe raha nafsi yake shujaa! Kuondoka namna hiyo, tunaamini ya kwamba labda ilikuwa ni jambo fulani, ya kwamba wakati wake wa kuondoka ulikuwa umewadia. Bwana kamwe hakutuonya juu ya jambo hilo, ama kumwonya juu yake, aliondoka tu. Hivyo ndivyo ilivyokuwa. Nami ninataka kumpigia simu mkewe mara niwezapo, na kumpa rambirambi zetu. Nasi sote tunataka kumshukuru Mungu kwa ajili ya maisha yake ya kishujaa ya Kikristo, na yale aliyomaanisha hapa duniani, na hasa sana kwetu hapa katika kusanyiko hili la mahali hapa.

13 Sasa usiku wa leo, nimetangaza kutakuwako na maombi kwa ajili ya wagonjwa usiku wa leo, nami nitazungumza zaidi juu ya wagonjwa usiku wa leo.

14 Lakini kwa wakati huu, hebu na tuingie moja kwa moja kwenye Neno sasa, kwa sababu kuna kusongamana na ni joto. Tutaenda moja kwa moja kwenye Neno. Ninataka kusoma kutoka katika sehemu mbili za Maandiko asubuhi ya leo, ndefu, kusudi zipate kunipa msingi kidogo juu ya yale ninayotaka kusema.

15 Na, sasa, natamani kama wangeliishikilia kanda hiyo, Ndugu Sothmann na hao wengine, kabla ya kuiuza, ikiwezekana, nami ni—ningetaka kuisikiliza kabla hatujaninii . . . kabla haijaenda kwa umma.

16 Sasa katika . . . Ninataka kusoma kutoka Wafilipi, mlango wa 2, 1 hadi 8, na Wakorintho wa Pili 3, kuanzia 6, na kusoma mpaka kwenye mlango wa 4 wa Wakoritho wa Pili, kwa msingi tu. Sasa katika Wafilipi, mlango wa 2, nitasoma kwanza.

Kabla ya kusoma, na tuombe.

17 Bwana Yesu, Neno Lako ni Kweli. Na katika saa hii ya dhiki ambayo tunaishi, taifa dhidi ya taifa, masumbufu, matetemeko ya ardhi mahali mahali, mioyo ya watu ikivunjika, hofu, tunaona maandiko ya mkono kwenye ukuta. Sasa, hiyo ni milki ya maumbile ya kawaida, kwamba ulimwengu wote unapaswa kuona jambo hili. Lakini sasa kuna milki ya kiroho, pia, nasi tunaona hayo matukio makuu, nasi tunataka kuzungumza juu ya hayo leo hii.

18 Bariki Neno Lako kwenye moyo wetu. Tunajua ya kwamba hakuna mtu Mbinguni wala duniani anayestahili kukichukua Kitabu hiki, kuifungua ile Mihuri, au, hata kuiangalia. Lakini kuna Mmoja aliyejitokeza, Mwana-kondoo aliyechinjwa, akiwa ameloa damu, ambaye alikuja akakitwaa Kitabu, na alistahili na aliweza kukifungua. Ee Mwana-Kondoo wa Mungu, fungua Neno Lako kwenye mioyo yetu leo, kwa faraja. Sisi ni watumishi Wako. Samehe dhambi zetu, Bwana. Na chochote ambacho kingelizuia Neno kuendelea kwa nguvu kuu na ushawishi leo juu ya maisha yetu, kiondoe, Bwana, kizuizi chochote, tupate

kiingilio kamili kwa baraka zote zilizoahidiwa kwetu kupitia Neno Lako. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

19 Wafilipi 2.

*Basi ikiwako faraja yo yote katika Kristo, yakiwako matulizo yo yote ya mapenzi, ukiwako ushirika wo wote wa Roho, ikiwako huruma yoyote na* rehema,

*Ijalizeni furaha yangu, ili mwe na nia moja, wenye mapenzi mamoja, wenye roho moja, m—mkinia mamoja.*

*Msitende neno lo lote kwa kushindana wala kwa majivuno; bali kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake.*

*Kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe, bali kila mtu aangalie mambo ya wengine.*

*Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo* pia ilikuwamo *ndani ya Kristo Yesu;*

*Ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho,*

*Bali alijifanya kuwa hana utukufu, akitwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu;*

*Tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba.*

20 Sasa kama tutafungua sasa kwenye Wakorintho wa Pili, mlango wa 3, tutaanza na kifungu cha 6, na kusoma hiki hadi cha 18, na kuendelea hadi kwenye sehemu ya mlango wa 4.

*Naye ndiye aliyetutosheleza kuwa wahudumu wa Agano Jipya, si wa andiko bali wa roho, kwa maana andiko huua bali roho huhuisha.*

*Basi, ikiwa huduma ya mauti, iliyoandikwa na kuchorwa katika mawe, ilikuja katika utukufu, hata Waisraeli hawakuweza kuukazia macho uso wa Musa, kwa sababu ya utukufu wa uso wake; nao ni utukufu uliokuwa ukibatilika;*

*Je! huduma ya roho haitazidi kuwa katika utukufu?*

*Kwa maana ikiwa huduma ya adhabu ina utukufu, siuze huduma ya haki ina utukufu unaozidi.*

*Maana hata ile iliyotukuzwa haikuwa na utukufu hivi, kwa sababu ya utukufu uzidio sana.*

*Kwa maana, ikiwa ile inayobatilika ilikuwa na utukufu, zaidi sana ile* ina. . .*ikaayo ina utukufu.*

*Basi, kwa kuwa mna taraja la namna hii, sisi* hatuna budi. . .*twatumia ujasiri mwingi;*

*Nasi si kama Musa, alivyotia utaji juu ya uso wake, ili kwamba Waisraeli wasiutazame sana mwisho wa ile iliyokuwa ikibatilika;*

*Ila fikira zao zilitiwa uzito. Kwa maana hata leo hivi, wakati lisomwapo Agano la Kale, utaji uo huo wakaa; yaani, haikufunuliwa kwamba huondolewa katika Kristo.*

*Ila hata leo, torati ya Musa isomwapo, utaji huikalia mioyo yao.*

*Lakini wakati wo wote watakapomgeukia Bwana, ule utaji huondolewa.*

*Basi 'Bwana' ndiye Roho; walakini alipo Roho wa Bwana, hapo ndipo penye uhuru.*

*Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho.*

*Kwa sababu hiyo, kwa kuwa tuna huduma hii, kwa jinsi tulivyopata rehema, hatulegei;*

*Lakini tumekataa mambo ya aibu yaliyositirika, wala hatuenendi kwa hila, wala kulichanganya neno la Mungu na uongo; bali kwa kuidhihirisha iliyo kweli twajionyesha kuwa na haki, dhamiri za watu zikitushuhudia mbele za Mungu.*

*Lakini ikiwa injili yetu imesitirika, imesitirika kwa hao wanaopotea.*

21 Bwana na aongeze baraka Zake kwa kusomwa kwa Neno Lake!

22 Sasa, somo langu asubuhi ya leo, ninatumaini ya kwamba Mungu atafunua jambo hili. Na kila wakati, kama ninyi mnaozichukua kanda na kusikiliza, nami ninatumaini na kuamini ya kwamba—ya kwamba mmekuwa na ufahamu wa kiroho juu ya yale Mungu amekuwa akijaribu kuliambia Kanisa bila ya kulisema moja kwa moja. Unaona? Ni jambo, wakati mwingine, inatubidi kusema mambo kwa njia fulani kwamba iweze kupunguza, iweze kuwafanya wengine kutoka nje, wengine kuondoka, na wengine ku—ku—kutafakari. Lakini hilo linafanywa makusudi. Lazima lifanywe hivyo.

23 Ndipo huenda ikawa kwamba wengine wangesema, "Unamaanisha Mungu angefanya jambo kama hilo makusudi?" Hakika alifanya. Angali anafanya.

24 Yeye alisema siku moja, wakati alipokuwa na maelfu wamemzunguka, Yeye alisema, "Msipoula Mwili wa Mwana wa

Mungu, ama Mwana wa Adamu, na kuinywa Damu Yake, hamna Uzima ndani yenu."

25 Unafikiri ni tamshi la namna gani daktari wa tiba ama nesi, ama mtu yeyote msomi angewazia juu ya tamshi kama hilo, kwa Mtu aliyekuwa na huduma kama ile Yeye aliyokuwa nayo? Mbona, angesema, "Ati kula mwili? Huyo ni mtu mla watu! Ati kunywa damu ya mwanadamu? Ni kizuu kifyonza damu! Kwa maneno mengine, Yeye anataka sisi tuwe wala watu na vizuu vifyonza damu." Na umati wote ukaondoka ukamwacha.

26 Na kulikuwako na shirika la wahudumu pamoja Naye, wa sabini, ambao walikuwa wamechaguliwa. Ndipo akawageukia, na akasema, "Mtawazia nini mtakapomwona Mwana wa Adamu akipaa juu kwenda mahali alipotoka?" Sasa, Yeye hakueleza hayo. Kamwe hakuelezea *vipi*; Paulo alifanya hivyo baadaye. Yeye alilisema tu. Unaona? Na ndipo wakati hili, Yeye alisema, "Mtasemaje," kwa hawa wahudumu, "mtakapomwona Mwana wa Adamu akipaa kwenda mahali alipotoka?"

27 Hapana shaka hao watu walisema, "Sasa, hebu tu kidogo. Loo, tunakula pamoja na Yeye. Tunavua samaki pamoja naye. Tunalala pamoja Naye. Tu—tunajua mahali alipozaliwa. Tuliona kitanda kidogo ali—alichopembezewa. Basi Mtu huyu . . . Hili ni neno gumu."

28 Na Biblia ilisema, "Hawakutembea pamoja Naye tena." Walimwacha.

29 Ndipo akabakia na kumi na wawili. Alikuwa amewachagua kumi na wawili, na mmoja wao alikuwa ni shetani, Yeye akasema. Kwa hiyo akawageukia.

Na hakuna mtu angaliweza kuelezea yale aliyokuwa ndiyo kwanza aseme. "Wataulaje Mwili Wake na Kuinywa Damu Yake? Na Yeye alishukaje, wakati alizaliwa papa hapa duniani?" Mnaona? Wasingeweza kuelewa jambo Hilo.

Na kisha akawageukia mitume, na akasema, "Ninyi pia mnataka kwenda?"

30 Na hapo ndipo mtume Petro alipotoa lile tamshi kuu, "Bwana, twende kwa nani?" Unaona? "Kwa kuwa tumeridhika. Tunajua hakika ya kwamba Wewe, na Wewe pekee, una Neno la Uzima la wakati huu." Unaona? "Na tumeridhika na hilo." Unaona, wasingeweza kuelezea jambo Hilo. Wao . . .

Huwezi kuelezea imani. Ni jambo fulani unaloamini, nalo ni imara sana hata hakuna kitu kingine kingalipachukua mahali pake.

Kwa hiyo, walijua ya kwamba Neno lililokuwa limeandikwa kwa ajili ya wakati ule waliokuwa wakiishi, ule wakati wa Masihi, ya kwamba aliafiki mahali hapo kikamilifu. Nao wangefanya nini kurudi katika hayo makanisa baridi, ya kawaida waliyokuwa wametoka kwake? Kasema, "Tungeenda

wapi?" Unaona? "Tumeshawishika kabisa ya kwamba Wewe una Neno la Uzima." Unaona? Na wao—wao wasingeweza kuelezea jambo Hilo, bali waliliamini. Mnaona?

31 Na Yesu alisema jambo hilo apate kupunguza kundi Lake, mnaona, mpaka alipoweza kukusanya kundi hilo pamoja. Na kutoka katika watu hao wote, wao, ni kumi na mmoja tu wa hao waliofahamu kikamilifu kwamba Yeye alikuwa ni Nani. Walijua ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu, na Mungu peke yake. Sasa, ninii . . .

32 Somo langu asubuhi ya leo ni kufunua, ama, kumfunua Mungu huyo.

33 Mungu daima ameninii, katika kila kizazi, amejificha nyuma ya pazia, nyakati zote, bali Yeye amekuwa ni Mungu wakati wote. Unaona? Lakini Yeye amejificha Mwenyewe kutoka kwa ulimwengu, na hujifunua Mwenyewe kwa Wateule Wake, kama wale mitume kwenye siku hiyo. Sasa, huyo alikuwa ni Mungu akinena ndani ya Kristo.

34 Sasa, mwanadamu daima, imekuwa ni tabia ya mwanadamu, yeye alitafuta kumwona (kimwili) huyo Mungu. Daima amekuwa anataka kumwona. Mwanadamu ametengeneza viumbe ambavyo vinafanana na Yeye. Wao wanawazia juu ya . . . Wahindi waliabudu jua. Na—na tunaona, katika Afrika, aina mbalimbali za wanyama, na kadhalika. Na huko juu . . . zile nguzo za mizimu huko Alaska, na—na maumbo mbalimbali ambayo wanawazia Mungu huyu yuko ndani yake. Kama vile Paulo alivyosema kule Athene wakati ule, kwenye mlima wa Areopago, na kuwaambia ya kwamba walikuwa washirikina kuhusu Mungu huyu asiyejulikana, ya kwamba, walijua alikuwako bali hata hivyo hawakumjua Yeye.

35 Na kwa hiyo tunaona hata huko nyuma zama za Ayubu. Ayubu alijua ya kwamba kulikuwako na Mungu. Alijua jambo hilo. Wala hakuna mwa—mwa—mwanadamu, wenye akili timamu, ila wale wanaojua hapana budi kuwako na Kitu fulani mahali fulani. Na, sasa, Ayubu alitaka kuzungumza naye.

Nami nawatakeni mwone umbo ambalo Mungu alichagua kumzungumzia Ayubu kwalo. Mungu alikuwa ana utaji wakati alipoongea na Ayubu. Alikuwa amefunikwa utaji katika upepo wa kisulisuli, alishuka katika upepo wa kisulisuli. Mnaamini ya kwamba Mungu ambaye bado huja katika upepo wa kisulisuli anaweza kuja mahali ambapo mnaona? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

36 Kuna baadhi ya wanaoketi hapa, watu kadhaa, waliokuwa pamoja nasi hivi majuzi wakati Yeye alipokuja katika upepo wa kisulisuli. Alitwambia siku moja kabla, Ndugu Banks Wood na hao wengine, wakati Yeye aliposema, "Litwae jiwe hili, litupe hewani, na useme, 'BWANA ASEMA HIVI! Mtaliona mara moja.'" Ndipo nikaokota jiwe hilo, huko juu ya kilele

cha mlima, nikalitupa hewani, na ninii . . . hapana shaka, lilipokuwa likishuka, lilisababisha upepo wa kisulisuli, unaona, mfyonzo wake.

37 Huna budi kufanya jambo fulani kusababisha jambo fulani kulifuata. Yesu alichukua kipande cha mkate na kukimega, kisha akaizidisha kutokana na kipande hicho cha mkate. Alichukua maji, akayamwaga kwenye balasi. Eliya alichukua chumvi, akaitia kwenye chupa; akakata kijiti, akakitupa majini. Ni kitu fulani cha kuonyesha mfano.

Basi nililiokota jiwe hili na kulitupa hewani, na lilipokuwa linashuka likaanzisha upepo wa kisulisuli.

38 Kesho yake, mbona, kulikuwako na mhudumu mmoja pamoja nasi kwenye safari ya kuwinda. Alikuwa amesimama karibu, na akaniambia, "Je! Bwana huonyesha maono huku nje namna hii, Ndugu Branham?"

39 Nikasema, "Naam, bali kwa kawaida mimi huja huku nipate kupumzika." Na papo hapo hilo ono likatokea.

40 Na Ndugu Borders, nafikiri yeye yuko nje sasa, alikuwa hapo. Ndugu Banks Wood, nafikiri, na, loo, watu kadhaa walikuwa kule juu, wanane ama kumi. Na Ndugu Banks Wood akiangalia jambo hili. Moja kwa moja huko mlimani, moja kwa moja kutoka, hasa, karibu nusu maili mahali wale Malaika saba walipotokea, ambapo niliondoka hapa kwenda kule kwa ajili yao, ambao walirudi na kusema . . . kuhusu ile Mihuri Saba. Yapata tu nusu maili kutoka pale.

41 Na ndipo kesho yake, wakati jambo hili lilipokuwa likiendelea, mbona, ninii . . . nilimwambia ndugu, huyu ndugu, nikasema, "Shida yako ni kwamba, una mzio jichoni mwako. Madaktari wamejaribu kwa miaka kadhaa kuukomesha nao hawawezi kufanya hivyo. Wanasema utaninii . . . utakula jicho lako lote." Nami nikasema, "Bali usifadhaike, Bwana Yesu ameiheshimu imani yako." Na ndipo akaiangusha tu bunduki yake. Kisha nikasema, "mama yako," vile hasa alivyokuwa na shida aliyokuwa nayo.

Naye akasema, "Hiyo ni kweli."

42 Ndugu Roy Roberson kutoka hapa kanisani, anayesimama hapa sasa, nadhani ninyi nyote mnamfahamu. Nikijua alikuwa shujaa wa vita, na nikijua kilichokuwa kinaenda kutukia, niliweka mkono wangu juu ya bega lake; nikasema, "Ndugu Roberson, kuwa mwangalifu, angalia, jambo fulani liko karibu kutukia."

43 Nilirudi mahali nilipokusudiwa kusimama, na kutoka hewani ukaja upepo wa kisulisuli, ukashuka kupita kwenye magenge, kutoka juu, ambao ulikuwa mkali sana hata ukaipasua miamba, inchi nane ama kumi kupenyeza ndani, kutoka kwenye kilele cha mlima huo, na kuyatupa umbali wa yadi mia mbili.

Na kukanguruma mara tatu namna hiyo, ndipo Sauti ikatoka kwake. Unaona?

44 Na hao wote wakisimama pale. Ndugu Banks, aliyepo sasa, alikuja na kusema, "Hayo ndiyo uliyoniambia jana?"

Nikasema, "Naam, bwana, ndiyo hayo."

Akasema, "Sasa, ilisema nini?"

45 Nikasema, "Sasa, hayo ni kwa ajili yangu mimi tu kujua, Ndugu Banks, unaona, kwa sababu ilikuwa. . .Ingewashtua watu sana."

46 Lakini iliendelea, ilitendeka tu kidogo. . .ikielekea kaskazini. Kidogo, siku chache baadaye iliipiga bahari, na mliona lililotukia kuzunguka Fairbanks. Ilikuwa ni ishara ya hukumu. Sasa tunaona ya kwamba—ya kwamba Mungu angali. . .Mnaona, lingewapa watu hofu kuu. Na kwa hiyo basi walikuwa. . .Hilo ilibidi litukie, mnaona. Halina budi kutukia. Mambo ambayo hayana budi kutukia hayana budi kutukia, kwa vyovyote vile. Unaona, litatukia, kwa vyovyote.

47 Musa wakati mmoja alitamani kumwona Mungu, ndipo Mungu akamwambia asimame juu ya mwamba. Na, juu ya mwamba, Musa alisimama na akamwona Mungu akipita, na mgongo wake ulionekana kama mgongo wa mwanadamu. Mungu alikuwa katika upepo wa kisulisuli, na Mungu. . . wakati Musa akisimama juu ya mwamba.

48 Nadhani nyote mliona hiyo picha huko nje hivi majuzi, tulisimama kwenye mwamba uo huo. Na hii hapa Nuru hiyo, Malaika wa Bwana, mahali pale pale ilipongurumia. Tukisimama. . .Iko pale pale kwenye ubao wa matangazo sasa, tena.

49 Angalia, Yehova wa Agano la Kale Ndiye Yesu wa Agano Jipya. Mnaona? Yeye ni Mungu yeye yule, akibadilisha tu umbo Lake.

50 Sasa, mtu fulani alisema hivi majuzi, m—m—mhudumu wa Kibaptisti huko Tucson, "Unawezaje kusema ya kwamba—ya kwamba Yesu na Mungu wangekuwa Mtu yule yule?"

51 Nikasema, "Vema, ni rahisi sana kama ukiacha mawazo yako mwenyewe yapite, na uwazie katika kanuni za Biblia za jambo hilo. Wao ni Mwenye Uhai yule yule. Mungu ni Roho; Yesu ni Mwili ambao Yeye alifunikwa ndani yake. Unaona?" Nikasema, "Ni kama vile nyumbani kwangu. Kwa mke wangu, mimi ni mume wake. Pia nina binti mdogo, Rebekah, mimi ni baba yake. Kisha nina mjukuu, na jina lake ni Paul, mimi ni babu yake. Mimi ni mume, baba, na babu. Na mke wangu hana madai kwangu kama baba wala babu; ana madai juu yangu tu kama mume. Naye binti yangu hana madai juu yangu kama mume wala babu; yeye ni mtoto wangu. Mnaona? Lakini hata hivyo watu hawa wote watatu ni mtu yule yule. Mnaona? Huyo ni Mungu;

Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, ni madai tu ya kipindi cha wakati." Mungu ni yeye yule, Mungu yeye yule.

52 Mungu alijibadilisha Mwenyewe, hubadilisha umbo Lake. Kama ukiangalia hapa katika Wafilipi, Yeye alisema, "Hakuona kuwa ni kitu cha kushikamana nacho, bali alichukua *mfano* wa mwanadamu."

53 Sasa, neno la Kiyunani hapo la hilo *umbo*, nimekuwa nikilitafuta siku nzima jana, nikijaribu kuwazia kwamba lilikuwa ni nini, ninapata, linaambatana na neno hili la "en morphe." Linaendelezwa e-n m-o-r-p-h-e. Nikiangalia katika Kiyunani, kutaka kujua en morphe ilikuwa ni nini . . . Huenda nikatamka hilo visivyo, bali sababu ya mimi kuliendeleza, wakati kama kanda ikitolewa, watu wataninii, wasomi wataninii, watajua kile ni—ninachomaanisha kwalo. Yeye, wakati ile en morphe, hilo linamaanisha kwamba Yeye alijibadilisha. Yeye, alishuka chini. Sasa, neno la Kiyunani pale linamaanisha, ya kwamba, "Kitu fulani ambacho kisingeweza kuonekana, hata hivyo kipo, kisha kinabadilishwa na jicho linaweza kukiona." Unaona?

54 Kama vile Eliya alivyokuwa, huko Dothani. Mnaona, yule—yule mtumishi asingeweza kuwaona Malaika hao wote waliopazunguka mahali pale, ndipo Mungu akabadilisha tu; si kwamba aliwashusha hao Malaika, bali alibadilisha kuona kwa yule mtumishi. Na hapo ilikuwapo milima imejaa Malaika, na moto, na farasi wa moto, na magari ya moto, kote kumzunguka nabii Wake. Mnaona, wao, Yeye alibadilisha kule kuona. Ki—kitu hicho tayari kipo pale.

55 Kwa hiyo, lile ninalojaribu kusema, ni ya kwamba Mungu ambaye amekuwapo daima yupo hapa. Jambo pekee alilofanya hapo alipofanyika mwanadamu, alibadilisha kinyago Chake. Unaona? Yeye—Yeye, hii en morphe, Yeye—Yeye alijibadilisha kutoka kile alichokuwa akawa kile alicho, ama kinyago Chake, onyesho lingine.

56 Kama vile katika mchezo mkuu wa kuigiza. Kama nilivyokuwa nikizungumza asubuhi ya leo, kwa namna fulani nikifuatilia kwenye huu wa Shakespeare. Imekuwa ni muda mrefu. Lakini wakati Shakespeare alipoandika huo—huo—mchezo wa kuigiza, nanii . . . kwa ajili ya Mfalme James wa Uingereza, wakati yeye . . . sifa bainifu ya Macbeth. Unaona, Shakespeare hakuamini katika wachawi; bali katika tamthilia hiyo, kwa kuwa Mfalme kweli aliamini katika wachawi, kwa hiyo ilibidi awajumuishe wachawi. Unaona? Na sasa, ili aweze kufanya hivyo, walibadilisha wachezaji.

57 Becky hapa, katika *Carmen*, waliigiza huo katika—katika shule ambako ndio kwanza ahitimu majuma machache yaliyopita. Sasa, labda mtu mmoja aliigiza sehemu tatu ama nne. Kusudi afanye hivyo, ali—alibadilisha kinyago chake.

Wakati mwingine anatokea, yeye ni mwigizaji *huyu*; na wakati mwingine anapotokea, yeye ni mwigizaji mwingine. Lakini ni mtu yule yule wakati wote.

58 Na ndivyo ilivyo na Mungu. Yeye alijibadilisha kutoka—kutoka kwenye Nguzo ya Moto, akawa Mwanadamu. Kisha akajibadilisha kutoka kwenye huyo, akarejea kwenye Roho tena, apate kuishi ndani ya mwanadamu. Mungu akitenda katika mwanadamu kile alichokuwa hasa. Yesu Kristo, alikuwa ni Mungu akitenda kazi katika Mwanadamu, katika Mwanadamu *mmoja*. Katika Mwanadamu mmoja, hivyo ndivyo Yeye alivyokuwa. Alikuwa amejibadilisha kutoka Nguzo ya Moto, na halafu alikuwa ameingia; ambayo ilikuwa ni pazia huko jangwani, ambalo lilimficha Mungu kutoka kwa Israeli. Musa aliona umbo la mwili Wake, bali kweli Yeye sikuzote alikuwa amefichika nyuma ya Nguzo hii ya Moto, ambayo ilikuwa ni Logos ambayo ilitoka kwa Mungu.

59 Sasa tunaona hapa, sasa tangu Pentekoste, Mungu hatendi kazi akiwa *ndani ya* mwanadamu, ama kutenda…sasa anatenda *kupitia* mwanadamu. Mnaona? Yeye alikuwa akitenda kazi akiwa *ndani ya* Mwanadamu wakati huo, Yesu. Sasa Yeye anatenda kazi *kupitia* mwanadamu ambaye Yeye amemchagua kwa kusudi hili. Mungu, katika umbo la mwanadamu, Yeye alijibadilisha kutoka umbo la—la…la Mungu, akawa katika umbo la mwanadamu.

60 Yeye alikuja katika majina matatu, majina matatu ya wana. Alikuwa katika Mwana…jina la Mwana wa—wa Adamu, Mwana wa Daudi, na Mwana wa Mungu; majina matatu ya wana.

61 Sasa, Yeye alikuja kwanza katika Mwana wa Da-…Mwana wa Adamu, kwa sababu Yeye alikuwa ni Nabii. Sasa, Yehova Mwenyewe alimwita Ezekieli na manabii, "mwana wa Adamu, unaona nini?" Yesu kamwe hakujiita Mwana wa Mungu; Yeye alijiita Mwana wa Adamu, kwa sababu Ma—Maandiko hayawezi kuvunjwa.

Hakuna kitu kinachoweza kuvunjwa katika Maandiko. Kila Neno halina budi kuwa hivyo. Hivyo ndivyo ninavyoamini jambo hilo. Hivyo ndivyo linavyopaswa kuwa, si kwa sababu ninaliamini, ni kwa sababu ni Neno la Mungu.

62 Sasa kama utaona hapo mwanzo, Neno moja, ukurasa wa kwanza katika Biblia, katika Mwanzo 1, tunaona kwamba ninii yote…Magonjwa yote, huzuni yote, taabu zote, na kila kitu kilichowahi kuwapata wanadamu, kilikuja kwa sababu mtu *mmoja* alishuku Neno *moja*, ikasababisha haya yote. Hapo ni mwanzoni mwa Biblia. Mwishoni mwa Biblia, Ufunuo 22, Mungu yeye yule alisema, "Mtu atakayeondoa Neno moja kutoka katika Hiki, au kuongeza neno moja Kwake." Mnaona, haina budi kuwa ni Neno kwa Neno, jinsi tu lilivyo.

63 Kwa hiyo, basi, na kuondoa tu kitu kidogo kama ninachoenda...mtu fulani daima akinifuatilia kuhusu wanawake kukata nywele zao. Sasa, kwangu mimi, mradi tu anafanya jambo hilo, sijali anafanya kitakatifu jinsi gani na anajua kiasi gani, angali yuko makosani. Anavaa kaptura na nguo hizi namna hiyo; sijali anafanya nini, jinsi anavyoweza kuimba, jinsi anavyoweza kuhubiri vizuri, chochote angaliweza kufanya, anaishi maisha ya namna gani, bado ni hilo Neno moja limevunjwa. Unaona? Unaona, haina budi kuwa ni kila Neno. Sio sentensi; Neno, Neno moja! Kwa hiyo, Biblia si ya kufasiriwa apendavyo mtu yeyote. Halina budi kuwa ni Neno kwa Neno, jinsi ilivyoandikwa. Hatuna budi kuamini jambo Hilo.

64 Na si kuliamini tu, bali kuliishi. Tusipoliishi, basi hatuliamini; tunasema tu tunaliamini. Kama vile mimi... Kulingana na vile nilivyosema, hao wanafunzi wasingeweza kulielezea, bali waliliamini, hata hivyo, nao wakafanya maungamo yao na kuliishi. Wakati hao wengine wote walipoliacha, wao walidumu Nalo! Waliliamini! Hivyo ndivyo tunavyofanya. Hivyo ndivyo inavyokubidi kufanya jambo hilo. Haidhuru mtu mwingine yeyote anafanya nini, tunaliamini na halafu tunalitekeleza. Usipofanya hivyo, basi huliamini.

65 Sasa angalia sasa wakati Yeye alipokuja, ilimbidi kuja kama Mwana wa Adamu, kwa sababu Maandiko Matakatifu yalisema ya kwamba angefanya hivyo, "Mungu angewaondokeshea Nabii." Kwa hiyo Yeye asingekuja akijiita Mwana wa Mungu, kwa sababu haikuwa ni kipindi hicho cha wakati. Yeye alikuwa ni Mwana wa Adamu akitabiri, kutimiza, na kuwafunulia mambo yote yaliyokuwa yamefanywa, na kufananisha kile alichokuwa. Wakati huo Yeye alikuwa duniani kama Mwana wa Adamu.

66 Mwangalie yule mwanamke Msirofoinike aliyemkimbilia, na kusema, "Ewe Mwana wa Daudi, nirehemu!" Kamwe hata hakuinua kichwa Chake. Yeye hakuwa na madai juu Yake kama Mwana wa Daudi. Yeye alikuwa ni Mmataifa.

Si zaidi sana ambavyo binti yangu awe na madai juu yangu kama mume; ama, mke wangu, kama binti. Hata hivyo, yeye ni binti yangu na mke wangu, yeye ni binti yangu katika Injili. Lakini, duniani, hana haki ya kuniita ba—baba. Unaona?

Sasa angalia, mwanamke huyu Mmataifa hakuwa na madai Kwake kama Mwana wa Daudi. Lakini kipofu Bartimayo alikuwa nayo, unaona, yeye alikuwa ni Myahudi. Sasa, Yeye alikuja kama Mwana wa Adamu.

67 Hamna budi kuyajua maneno haya na mambo haya. Mwangalieni Hattie Wright wakati ule, wakati ule Mvuto wa Tatu. Mnakumbuka jambo hilo. Zaidi ya mambo yote, mwanamke huyo alisema jambo lililo sahihi. Huna budi kusema neno hilo lililo sahihi, jambo lililo sahihi kwa Mungu.

68 Angalieni sasa, Yeye alikuja kwanza kama Nabii, nao wakamsulibisha. Walio Wake walimsulibisha. Yeye alikuja kama Mwana wa Adamu.

69 Ndipo baada ya Roho Mtakatifu kuja, Yeye basi alikuwa ni Mwana wa Mungu. Mungu ni Roho. Yeye alikuwa ndiye Roho Mtakatifu, Mwana wa Mungu. Aliishi katika nyakati za kanisa kama Mwana wa Mungu.

70 Sasa, katika ule Utawala wa Miaka Elfu, Yeye atakuwa ni Mwana wa Daudi, akiketi juu ya Kiti cha Enzi cha baba Yake, Daudi. Yeye ni Mwana wa Daudi, basi.

71 Pia, kumbukeni, kati ya Mwana wa Mungu. . . Katika wakati wa kanisa la Laodikia, walimtoa nje. Na katika Luka, Yeye alisema angefunuliwa tena kama Mwana wa Adamu, yule Nabii, akitimiza yaliyosalia. Unaona? Maandiko yanafungana pamoja kikamilifu. Mwana wa Adamu, Mwana wa Mungu, Mwana wa Daudi. Ilikuwa ni kitu gani? Ni Mungu yeye yule wakati wote, akibadilisha tu umbo Lake, en morphe. Yeye alilibadilisha tu. Ni mchezo mkubwa wa kuigiza Kwake. Yeye anaucheza.

72 Yeye alikuja kama Mwana wa Adamu, yule Nabii. Akafanya vivyo hivyo hasa. Hata maskini yule mwanamke katika dhambi zake zote, pale kisimani, alimtambua. Alisema, "Tunajua yuaja Masihi, ambaye anaitwa Kristo, hivyo ndivyo atakavyofanya." Unaona, alitambua kwa sababu yeye alikuwa Mbegu iliyokusudiwa tangu zamani. Ndipo yeye . . .

Ambapo, hao wengine hawakutambua jambo Hilo. Hawakuwa na kitu cha kutambulia. Walikuwa katika dhambi, kwanza kabisa.

73 Kwa kuwa, kwa kuigiza Kwake, Yeye hubadilisha umbo Lake. Ndipo Yeye akaja katika namna ya Mwana wa Adamu.

Kwa wakati wa wale watengenezaji, Wesley, Luther, na hao wote kotekote, ndipo tunakuta kwamba waliyarundika sana, kama tu Israeli walivyofanya, mpaka anapotokea katika siku za mwisho, katika wakati wa kipentekoste, kama Roho Mtakatifu, walimkataa. Walifanya jambo lile lile Israeli ililofanya.

Na Yeye anafanya nini sasa? Anarudi kama Mwana wa Adamu. Na kisha, kutoka huyo, Mwana wa Daudi. Mnaona jinsi tulivyo karibu? Mwana wa Adamu, Mwana wa Daudi, Mwana wa Mungu. Yeye anafunuliwa katika siku za mwisho kama Mwana wa Adamu, kulingana na Malaki 4, unabii mwingine wote unaohusu wakati huu. Hajishughulishi na kanisa tena baada ya Yeye. . . Walimtoa nje; yuko nje, akibisha mlangoni. Mbegu fulani iliyokusudiwa mle ndani, bado. Hana budi kuzifikia.

74 Na Mungu, katika mwanadamu, alikuwa amejimimina mzima. Yoeli 2:28, tunaona, Yeye alisema, "Nitammwaga, katika siku za mwisho, Roho Wangu." Sasa, kama ukiangalia hilo neno

hapo, neno la Kiyunani. Huenda nikakosea kwa hili, bali lile ningeweza kupata . . .

75 Inawabidi kuyaangalia maneno. Kiingereza wakati mwingine huwa na maana maradufu. Kama tu neno tunalosema, "mungu." Mungu aliumba mbingu na nchi, Mwanzo 1. Lakini sasa, katika Biblia, Ilisema, "Hapo mwanzo Elohimu." Sasa, Elohimu, Kiingereza kinaliita "mungu," lakini kwa kweli haikuwa ni *Elohimu*. Chochote kinaweza kuwa mungu, kwa neno *mungu*; unaweza kufanya sanamu mungu; unaweza kuifanya piano hiyo mungu; unaweza kufanya chochote mungu.

76 Lakini sivyo ilivyo kwa neno *Elohimu*; linamaanisha, "Yeye aishiye peke Yake." Mnaona? Ile piano haiwezi kuishi peke yake yenyewe, hakuna kitu kingine kinachoweza kuishi peke yake. Kwa hiyo, neno *Elohimu*, linamaanisha, "Yeye aliyekuwapo daima." *Mungu* linaweza kumaanisha chochote. Mnaona tofauti katika neno hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

77 Sasa, wakati liliposema hapa ya kwamba yeye *alijimimina* mzima, ama *alijimwaga*, sasa, tungewazia hivi, ya kwamba Yeye "alitapika," neno la Kiingereza la *kufanya tupu*, ama *kumwaga* kutoka Kwake, unaona, kitu fulani kilitoka Kwake kilichokuwa ni tofauti na Yeye. Lakini neno *kenos*, katika Kiyunani, halimaanishi ya kwamba Yeye "alitapika," ama ninii . . . Mkono Wake ulikatika, ama jicho Lake lilitoka, mtu mwingine.

78 Hiyo ni kusema, Yeye alijibadilisha, Yeye "alijimwaga katika," (Amina), katika kinyago kingine, katika umbo lingine. Si kwamba mtu mwingine alitoka Kwake, anayeitwa Roho Mtakatifu, bali ilikuwa ni Yeye Mwenyewe. Mnalipata? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Yeye Mwenyewe alijimwaga ndani ya watu. "Kristo ndani yenu!" Ni zuri jinsi gani, ni ajabu jinsi gani, kuwazia, Mungu akijimwaga ndani ya mwanadamu, ndani ya mwaminio. "Kumwaga!" Ilikuwa ni sehemu ya mchezo wake wa kuigiza, kufanya hivyo.

Mungu, utimilifu wote, Uungu wote kwa jinsi ya mwili ulikuwa ndani ya Mtu huyu, Yesu Kristo. Yeye alikuwa Mungu, na Mungu peke Yake. Sio nafsi ya tatu ama nafsi ya pili, ama nafsi ya kwanza; bali ni *ile* Nafsi, Mungu akijificha katika mwili wa mwanadamu.

79 Timotheo wa Kwanza 3:16, "Na bila shaka siri ya utauwa ni kuu; kwa kuwa M-u-n-g-u, Elohimu," herufi kubwa M-u-n-g-u, katika Biblia. Lirejeshe nyuma, mtu yeyote yule. Linahusu, katika ile ya asili, ilisema, "Elohimu." "Hapo mwanzo, Elohimu." Mnaona? "Na, Elohimu, bila shaka siri ya Elohimu ni kuu; kwa maana Elohimu alifanyika mwili, nasi tukamgusa kwa mikono." Elohimu, alijificha katika mwili wa kibinadamu! Yule Yehova mkuu aliyefunika anga lote, wakati, na kila mahali, alifanyika mtu. Tulimgusa kwa mikono,

Elohimu. "Hapo mwanzo, Elohimu. Naye Elohimu alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu."

80 Ni kitu gani? Hii ndiyo njia Yake, sehemu za mchezo wa kuigiza. Hivyo ndivyo atakavyoucheza, njia Yake ya kujifunua Mwenyewe kwetu kama mtu mwingine. Sisi ni wanadamu, Naye anajua jambo hilo. Nasi tunafahamu tu kama wanadamu. Sisi tunajua tu kama wanadamu. Tunajua tu kama vile hisi zetu zitakavyoturuhusu kujua, na hayo yaliyosalia hatuna budi kuamini kwa imani. Hatuna budi kusema kuna Mungu; kama tunamwona, ama hatumwoni, tunaamini, kwa vyovyote. Mnaona? Kama yupo ama hayupo, tungali tunaamini kwa sababu Mungu alisema hivyo.

81 Kama vile Ibrahimu, asingeweza kumwona yule mwana, hakuna dalili, hakuna mimba kwa—kwa Sara, hata hakuna vipindi vya hedhi wala chochote kile, bali hata hivyo Mungu alisema hivyo. Matumaini yote, hata tumbo la—lake la uzazi lilikuwa limekufa, na uhai wa mumewe ndani yake ulikuwa umekwisha, na—na mtiririko wa uhai wake ulikuwa umekauka, na uhai wa—wake ulikuwa umekauka ndani yake. "Na hata hivyo hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini, bali alipata nguvu, akitukuza, akijua ya kwamba Mungu alikuwa anaweza kufanya lolote alilosema angefanya."

Hivyo ndivyo inavyotupasa kuliamini hilo Neno siku hizi. Itakuwaje? Sijui. Mungu alisema itakuwa hivyo, na hilo latosha.

82 Mtu huyu mkuu asiyeonekana ni nani? Ni nani Huyu ambaye Ibrahimu alimwona katika maono? Mwishoni kabisa, hata hivyo, Yeye alidhihirishwa katika mwili, kabla yule mwana hajaja. Mungu Mwenyewe alimjia Ibrahimu katika umbo la mwanadamu, katika wakati wa mwisho. Akadhihirishwa! Yeye alimwona katika Nuru ndogo wakati mmoja; alimwona katika maono; aliisikia Sauti Yake; mafunuo mengi. Lakini kabla tu ya mwana aliyeahidiwa, yeye alimwona katika umbo la mwanadamu, na akazungumza Naye, na akampa nyama na kinywaji. Unaona? Angalia, Mungu Mwenyewe akiwa amefunikwa katika mwili wa mwanadamu.

83 Hii ni sehemu ya njia Yake. Hivi ndivyo ambavyo Yeye hujidhihirisha kwetu, hulidhihirisha Neno la Milele, Mungu, Yehova aliyefanyika mwili. Kama vile katika Yohana Mtakatifu 1, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, na ninii. . . Hapo mwanzo kulikuwako Elohimu, naye Elohimu alikuwa . . . akafanyika Neno, na huyo Neno alikuwa ni Elohimu. Naye Neno alifanyika Elohimu." Unaona? Ni jambo lile lile, likijifunua tu.

84 Kama vile sifa, unaona, imo ndani ya Mungu. Sifa ni wazo lako. Mungu hapo mwanzo, yule wa Milele, Yeye hata hakuwa Mungu. Yeye alikuwa ni wa Milele. Hata hakuwa ni Mungu; Mungu ni kitu cha kuabudiwa, ama kitu fulani. Unaona? Kwa

hiyo hata hakuwa hivyo. Yeye alikuwa ni Elohimu, yule wa Milele. Lakini ndani Yake mlikuwamo na mawazo kwamba alitaka kufanyika mwili. Naye alifanya nini? Basi alinena Neno, nalo Neno likafanyika mwili. Hiyo ndiyo picha nzima, kutoka Mwanzo hadi Ufunuo. Hakuna kosa. Ni Elohimu akifanyika mwili kusudi apate kuguswa, kuhisiwa. Na katika ule Utawala wa Miaka Elfu, huyo hapo Elohimu ameketi kwenye Kiti cha Enzi, mnaona, hiyo ni kweli, pamoja na raia Wake wote wamemzunguka, ambao aliwakusudia kabla ya kuwekwa msingi wa ulimwengu.

85 Ni kama mtu anayejenga sauti za kengele ama anayefanya sauti za kengele, mfinyanzi. Kila kengele haina budi kulia tofauti na nyingine. Nyenzo zile zile, bali kiasi fulani cha chuma, kiasi fulani cha feleji, kiasi fulani cha shaba, kuifanya itoe ule mlio wa "ngoo."

86 Hivyo ndivyo Mungu alivyofanya. Yeye alizalisha hiki kikawa kile, kwa kile kwa hiki, kwa hiki kwa kile, mpaka akapata kile hasa Yeye alichotaka. Hivyo ndivyo Yeye alivyoshuka. Mungu alijifunua Mwenyewe katika Nguzo ya Moto kote kupitia kwa manabii, kisha katika Mwana wa Mungu, ambaye, Yeye alikuwa ni Mungu. Mnaona, ni Mungu yeye yule akileta hasa, kutoka utimilifu hadi utimilifu, kutoka utukufu hadi utukufu. Hivyo ndivyo Kanisa linavyoenenda.

87 Angalia, kupitia katika nyakati, vivyo hivyo, kwa manabii Wake, Yeye amejifunua Mwenyewe. Hao hawakuwa ni manabii hasa, walikuwa ni miungu. Yeye alisema hivyo. Kwa kuwa, kile walichosema kilikuwa ni Neno la Mungu. Walikuwa ndio mwili ambamo Mungu alikuwa amejifunika. Walikuwa ni miungu. Yesu alisema, Mwenyewe, alisema, "Mnawezaje kunihukumu ninaposema Mimi ni Mwana wa Mungu, na torati yenu wenyewe inasema ya kwamba hao ambao walijiliwa na Neno la Mungu walikuwa ni miungu?" Unaona?

88 Kwa hiyo ilikuwa ni Mungu aliyejileta katika umbo la mtu aliyeitwa nabii. Unaona? Nalo Neno la Bwana lilimjia mtu huyu, kwa hiyo haikuwa ni nabii huyo; nabii alikuwa ni pazia, bali hilo Neno lilikuwa ni Mungu. Neno la mtu huyo lisingefanya hivyo. Mnaona ninalomaanisha? Haliwezi kutenda kazi jinsi hiyo. Lakini kwa uwezekano ilikuwa ni Mungu. Mnaona, Yeye alikuwa Neno la Mungu katika umbo la mwanadamu, aliyeitwa "mtu."

Angalia, Yeye kamwe hakubadilisha tabia Yake, ni umbo Lake tu. Waebrania 13:8, ilisema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Kwa hiyo Yeye hakubadilisha tabia Yake wakati alipokuja. Yeye daima ni yule Nabii, kote kote katika wakati, kitu kile kile: Neno, Neno, Neno, Neno. Unaona? Yeye hawezi kubadilisha tabia Yake, bali alibadilisha umbo Lake. Waebrania 13:8, ilisema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Yeye alibadilisha tu kinyago Chake.

89 Kama vile nilivyobadilika kutoka mume, wakati mtoto wangu amezaliwa, ndipo mimi ni baba. Wakati mjukuu wangu anapozaliwa, mimi ni babu. Mnaona? Lakini, sibadiliki; huyo angali—angali ni mimi. Mnaona? (Na huyo ni Mungu.) Ni kwamba tu nilibadilisha ninii yangu . . . Mnaona, ni kwamba tu ulibadilisha umbo lako. Unaona?

Angalia. Na maumbile yanalibadilisha kutoka kijana hadi mtu wa makamu, hadi mzee. Haya basi, unaona, unabadilisha tu umbo lako.

90 Sasa, usingeweza kusema maskini jamaa mdogo anayesimama hapa, mwenye umri wa miaka kumi na sita, useme alikuwa ni babu. Asingeweza kuwa. Umbo lake halina budi kubadilishwa. Miaka michache hulibadilisha, ndipo anakuwa babu. Unaona ninalomaanisha?

91 Lakini ni Mtu yule yule wakati wote, Mtu yule yule, Mungu wakati wote. Kwa njia hii Yeye hujifunua kwa watu Wake, katika kufanya jambo hili. Angalia, kupitia kwenye wakati wa ile Nguzo ya Moto, Yeye alijifunua Mwenyewe kwa watu Wake. Katika wakati wa—wa Yesu, Yeye alijifunua Mwenyewe kwa watu Wake. Katika wakati wa Roho Mtakatifu, kama Mwana wa Mungu. Mwana wa Daudi . . . Yeye daima hujifunua kwa njia hiyo kwa watu Wake, akiwafanya watu wamjue. Yeye amejifunika nyuma ya kitu fulani, angalia, kwa njia ile ile, ama tabia ile ile, kila wakati.

92 Mungu akijificha nyuma ya pazia katika Yesu, kufanya kazi ya ukombozi pale msalabani. Mungu asingeweza kufa, kama Roho. Yeye ni wa Milele. Bali ilimbidi kuvaa kinyago na kutekeleza sehemu ya kifo. Yeye alikufa, bali asingeweza kufanya hivyo katika umbo Lake la Mungu. Ilibidi afanye hivyo katika umbo la Mwana, kama Mwana wa Adamu, duniani. Unaona? Ilibidi awe katika umbo la Mwana. Ndipo wakati aliporudi kwenye Pentekoste, Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu tena. Mnaona kile ninachomaanisha? Mnalipata hilo wazo? Yeye alikuwa . . .

93 Ilibidi aje katika mwili wa binadamu, kuninii . . . na hakuna mtu, pasipo na tamaa ya kujuana kimwili. Kwa sababu hilo linathibitisha tena tamshi letu la uzao wa nyoka, unaona, "kujuana kimwili," ni kujuana kimwili hasa. Si matofaa; kujuana kimwili! Hiyo ni kweli. Hilo lilibidi liwe. Angalieni hapa, mnaona, kwa mtu yeyote mzuri . . . Waangalieni hao manabii huko nyuma, bali ilibidi Yeye awe zaidi ya nabii. Mnaona? Kusudi aweze kufanya jambo hilo, ilibidi apitie kwenye kuzaliwa na bikira, ikionyesha ya kwamba kuzaliwa na bikira kulithibitisha . . . Ilibidi azaliwe na bikira, apate kuondoa laana hiyo, kile kiuasumu. Mnaona kile ninachomaanisha? Kwa hiyo, ilibidi iwe ni kujuana kimwili. Yeye alithibitisha hilo kwa kule kuja Kwake Mwenyewe; Yeye alikuja si kwa tamaa ya kujuana

kimwili, bali kwa kuzaliwa na bikira. Naye akabadilisha kinyago Chake kutoka Yehova akawa Yesu, kusudi achukue kazi ya ukombozi katika ule mchezo wa kuigiza aliokuwa akiigiza, katika Mungu pale msalabani.

94 Wayunani walitaka kumwona. Katika Yohana Mtakatifu 12:20, wengi wenu mlinisikia nikihubiri juu ya jambo hilo nikisema, "Mabwana, tungetaka kumwona Yesu." Mliona jambo hilo?

95 Sasa, Wayunani walikuwa ni wasomi, walikuwa ni watu mashuhuri. Nao walikuwa na ninii—walikuwa na ninii—juhudi kali juu ya Mungu sana, kama vile Paulo alivyowahubiria kwenye mlima wa Areopago. Nao walikuwa, wao—waliongoza—waliuongoza ulimwengu katika sayansi na—na elimu, walikuwa ni watu mashuhuri. Lakini waliabudu na kuamini hekaya za kale na kwa hiyo, vitabu vya sanaa na udadisi wa sanaa, na kadhalika.

96 Lakini wao—wao—wao walipatwa na kiherehere kuhusu Mtu huyu ambaye angeweza kuwaponya wagonjwa na angeweza kutabiri mambo yaliyotukia, juu ya alama. Basi walishikwa na kiherehere, kwa hiyo wakaja kumwona. Sasa, angalia kwa makini sasa, usikose jambo hili. Unaona? Nao wakaja na wakamwambia Filipo, ambaye alikuwa wa Bethsaida, "Bwana, tungependa kumwona Yesu." Basi Filipo na mwanafunzi mwingine wakawaleta kwa Yesu, kumwona Yesu.

97 Sasa angalieni maneno yenyewe ambayo Yesu aliwaambia, kwa kuwa walikuja kuona Yeye alikuwa ni Nani, wala hawakuweza kumwona. Waliona lile umbo, bali Yeye alikuwa katika hekalu Lake. Mungu alikuwa katika hekalu Lake, amefunikwa pazia katika mwili wa binadamu. Angalieni maneno aliyosema, "Chembe ya ngano isipoanguka ardhini, unaona, na ikafa, inakaa peke yake." Unaona? "Saa imewadia, hivi karibuni Mwana wa Adamu atatukuzwa, unaona, Naye hana budi kutoka humu duniani. Na isipokuwa saa hii ije, kamwe hamtaweza kuliona Hilo." Unaona?

98 Hapa, kwa nini wasingeweza kumwona Yesu? Yeye alikuwa amevaa kinyago. Mungu alikuwa amevaa kinyago. Wayunani walimtaka Mungu, na alikuwa ndiye Huyu hapa, lakini hawakuweza kumwona kwa sababu ya ule utaji. Na ni jambo lile lile leo, wao hawawezi kumwona kwa sababu ya pazia. Limefunika uso wao. Hawa Wayunani walikuwa wamefunikwa kwa kinyago, ama Yesu alikuwa amefunikwa kwa kinyago kwa Wayunani.

99 Angalia, Yeye aliwaambia, "Chembe hii ya ngano isipoanguka ardhini, hukaa peke yake."

100 Wao, wasingeweza kufahamu ni jinsi gani, ni kwa nini wasingeweza kumwona. Hapo amesimama mtu. Walikuja kumwona Mungu, nao wakamwona mwanadamu. Mnaona?

Hawakuweza kumwona Mungu kwa sababu Mungu alikuwa amefichwa nyuma ya pazia kwao. Sasa wekeni hilo niani mwenu, Mungu alikuwa ametiwa utaji katika mwanadamu. Wao wangeweza kusema, "Hakuna mtu angeweza kufanya mambo haya isipokuwa iwe ni Mungu. Hakuna mtu anayeweza kuyafanya, na jinsi ambavyo huyu hapa mtu amesimama na hata hivyo kazi za Mungu zinadhihirishwa kupitia Yeye!" Mnaona! Hawakuweza kufahamu ya kwamba Mungu alikuwa amefichwa nyuma ya pazia.

101 Yeye amejificha ndani ya mwanadamu, kama vile alivyojificha nyuma ya pazia daima. Lakini, Yeye alikuwa amejificha nyuma ya pazia kwao, alikuwa katika hekalu Lake la kibinadamu. Mungu alikuwa katika hekalu la kibinadamu. Sasa, iweni waangalifu sana, sasa Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Unaona? Mungu nyuma ya pazia, akijificha Mwenyewe kwa ulimwengu, akiwa nyuma ya pazia la mwanadamu. Mnaona? Huyu hapa Mungu! Wale Wayunani wakisema, "Tunataka kumwona Yeye."

102 Ndipo Yesu akasema, "Chembe ya ngano haina budi kuanguka ardhini ikafa." Huna budi kufa kwa mawazo yako yote. Huna budi kuyaondokea mawazo yako mwenyewe.

Kama vile hao wanafunzi walivyokuwa, hawakuweza kueleza kuhusu kula mwili Wake na—na kuinywa Damu Yake, lakini, unaona, walikuwa tayari wamekufa kwa mambo hayo. Walikuwa wamekufa kwa Kanuni fulani, walikuwa wamekufa kwa Kristo. Haidhuru ni kitu gani, ama alionekana ameshindwa jinsi gani, hata hivyo wangali waliamini jambo hilo. Unaona? Wangeweza kuona katika Mtu huyo; Mtu aliyekula, aliyekunywa, aliyevua samaki, aliyelala, chochote kile, aliyekuwa amezaliwa hapa duniani, na akatembea pamoja nao, akazungumza nao, akavaa nguo kama hao wengine, bali huyo alikuwa ni Mungu.

103 Kwa hiyo Wayunani hawakuweza kumwona, kwa sababu Yeye alifichwa kwao, katika mwanadamu. Angalieni Neno Lake kwao, "Chembe hii ya ngano isipoanguka ardhini."

104 Mungu nyuma ya pazia katika umbo la mwanadamu, alijificha wasiweze kumwona. Waliweza tu kumwona mtu. Lakini wale Waliokusudiwa tangu zamani walimwona Mungu. Mmoja aliona mwanadamu, huyo mwingine alimwona Mungu. Unaona? Na ilikuwa ni Mungu nyuma ya pazia la mwanadamu, ikiwafanya wote wawili kuwa sahihi, lakini imani yako katika yale usiyoyaona. Unayaamini, hata hivyo. Mungu nyuma ya pazia la mwanadamu. Yeye alikuwa katika mwili huo, nao mwili huo ulikuwa ndio pazia Lake. Lile pazia lilipasuliwa, unaona, kusudi Mungu apate kudhihirishwa.

105 Katika Agano la Kale, Mungu alikuwa amefichika wakati alipokuwa kwenye kiti Chake cha rehema; kwenye kiti cha

rehema, kwa pazia. Katika Agano la Kale, Mungu alikuwa katika hekalu Lake. Lakini watu walikuja na kuabudu namna hii, lakini, kumbukeni, kulikuwako na pazia (amina) lililomficha Mungu. Walijua Mungu alikuwa yupo. Wasingeweza kumwona. Ile Nguzo ya Moto haikuonekana tena kule. Je! mlifahamu? Hakuna wakati mmoja katika Maandiko, tangu wakati ile Nguzo ya Moto iliporudi nyuma ya lile pazia, ilipopata kujionyesha tena, mpaka ilipokuja kutoka kwa Yesu Kristo. Mungu alikuwa nyuma ya pazia!

106 Wakati aliposimama duniani, Yeye alisema, "Nimetoka kwa Mungu tena ninarudi kwa Mungu."

107 Ndipo Paulo, (baada ya kufa Kwake, kuzikwa, na kufufuka), akienda zake Dameski, hii hapa ile Nguzo ya Moto tena. Ilikuwa ni kitu gani? Imetoka nyuma ya pazia! Utukufu kwa Mungu!

108 Yeye alikuwa ndani nyuma ya pazia. Sasa Yeye alikuwa nyuma ya nini? Pazia la ngozi. Mnaona, "ngozi za pomboo," nyuma ya pazia. Ndipo wakati hilo pazia lilipopasuliwa siku aliyosulubiwa, pazia alilokuwa amefungwa kwalo lilipasuka kwenye ile siku ya kusulubiwa, kiti chote cha rehema kilionekana wazi.

109 Sasa, Wayahudi hawakuweza kufahamu jinsi ambavyo Mungu angeweza kuwarehemu watu wenye dhambi, wachafu kama tulivyo sisi. Bali hawakuweza kumwona Huyu aliyekuwa akitoa rehema, kwa kuwa alikuwa amefichwa. Alikuwa nyuma ya kiti cha rehema, upande wa ndani, huku ngozi za pomboo zikining'inia chini, zikimfunika. Kabla . . .

110 Hapo nyuma, kama mtu yeyote aliingia nyuma ya lile pazia, ilikuwa ni kifo cha ghafla. Amina. Loo, tutapata somo hapa katika dakika moja, unaona, kama mnaweza—mnaweza kulipokea. Kutembea nyuma ya hizo ngozi . . . Hata mmoja wa wana wa kuhani alijaribu kufanya hivyo wakati mmoja, na akafa. "Usiende nyuma ya pazia hilo." Yule mtu aliyeingia nyuma . . . Kwa nini? Hakukuwako na ukombozi bado, katika hilo. Ilikuwa ni kwa uwezekano. Ilikuwa tu ni kwa uwezekano. Na chochote cha *uwezekano* si kitu halisi bado, mnaona, ni kwa uwezekano tu. Ilikuwa ni ukombozi . . . Dhambi ilifunikwa, sio kuachwa . . . kuondolewa, hasa, sio kuondolewa. *Kuondolewa* ni "kutalikiwa na kutengwa." Na kwa hiyo damu ya kondoo na ya mbuzi isingeweza kufanya hivyo, kwa hiyo Yehova alikuwa amefichwa nyuma ya pazia. Sasa, huko nyuma ya pazia hili ambako Yeye alikuwa amefichwa, kuingia mle, mtu alianguka akafa, kujaribu kuingia ndani Yake.

111 Lakini tangu Pentekoste, tangu kule Kusulubiwa, wakati hilo pazia lilipopasuliwa toka juu hata chini, kwa ajili ya kizazi hicho . . . Yesu alikuwa ndiye huyo Mungu, aliyefunikwa pazia. Na wakati alipokufa pale Kalvari, Mungu alituma moto na radi, na kulipua pazia hilo toka juu hata chini, hivi kwamba

kiti chote cha rehema kilionekana wazi. Bali wao walikuwa ni vipofu sana kuweza kuona jambo hilo. Kama Musa alivyosema hapa, ijapokuwa, ama . . . Paulo alivyosema, kusomwa kwa Musa, "Musa anaposomwa, bado, lile pazia lingali moyoni mwao." Loo, ndugu, dada, hilo ndilo Wayahudi walilofanya wakati pazia lilipopasuliwa na kumweka Mungu dhahiri kabisa, akining'inia msalabani. Yeye alikuwa anaonekana dhahiri kabisa, bali hawakuweza kuona jambo hilo.

112 Je! ingewezekana ya kwamba Mataifa wamefanya jambo lile lile? Ee Mungu! Wakati wamekuwa na nyakati za kanisa, za Mwana wa Mungu; bali wakati sasa pazia la madhehebu haya na kadhalika, pazia hili la mapokeo tulilo nalo tangu Pentekoste, wakati mapokeo ya kanisa yamepasuliwa, mambo ambayo watu walisema, "Siku za miujiza zimepita, na mambo haya," na Mungu ameondoa pazia Kwake, na kuliweka dhahiri kabisa, nao wako tayari kulisulibisha tena, vile vile hasa.

113 Mungu aliyefunuliwa, dhahiri, walipaswa kumwona amesimama pale. Hata hivyo alikuwa ni wa kawaida sana, Yeye alikuwa ni mtu wa kawaida. Hawakuweza kuona jambo Hilo. Mnaona, hapo alisimama mtu. "Vema," wao walisema, "jamaa huyu, yeye alitoka kwenye shule gani?" Lakini, kumbukeni, wakati mkuki huo ulipouchoma mwili Wake, huyo Roho alimwacha, hekalu . . . vibao vya dhabihu vikapinduliwa, na radi ikapiga kupitia hekaluni na kulipasua lile pazia. Ilikuwa ni kitu gani? Huyo hapo Mungu wao ameangikwa pale Kalvari, nao walikuwa vipofu sana kuona hilo.

114 Ikamweka dhahiri, na bado hawalioni! Wao ni vipofu. Mungu, aliyetiwa utaji katika mwanadamu!

115 Mnakumbuka, Yeye halafu alirudi kwa Paulo baada ya jambo hilo, na kwa Petro akiwa gerezani, kama Nguzo ya Moto. Mnakumbuka hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

116 Lakini katika siku za mwisho anapaswa kurudi tena, lakini Nguzo ya Moto inapaswa kurudi tena kumdhihirisha Mwana wa Adamu, mnaona, kuonyesha Neno, ile Nuru. Mapokeo, ambayo yamekuwako, yataondolewa. Hakuna kitu kitakacholisumbua; litatendeka, hata hivyo. Mungu anayararua tu hayo madhehebu na mapokeo.

Yeye atafanya hivyo na Roho wa aina gani? Kama alivyofanya mara ya kwanza. Angalia yale aliyofanya katika siku za Eliya, katika siku za Yohana. "Msianze kusema mioyoni mwenu mna 'baba Ibrahimu,' maana Mungu anaweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto." Mnaona? Msiwazie, "Maana, mimi ni mfuasi wa *hili* na ni mfuasi wa *lile*." Mnaona? Mungu akilirarua lile pazia, mnaona, kuonyesha Yeye ni nani. Unaona, angalieni pazia wakati linapopasuka hapa sasa, tunaona sasa.

117 Sasa, na wakati mmoja, kama mtu alipitia kwenye pazia hilo, ilikuwa ni kifo cha ghafla. Sasa, ni kifo kutolipenya! Amina. Kama huwezi kuvunja pazia hilo la mapokeo, uvunje ukuta huo wa dhehebu, kumwona Mungu katika nguvu Zake, ni kifo. Ambapo wakati mmoja ilikuwa ni kifo kuingia, sasa ni kifo kukaa nje. Kiti chote cha Rehema kimewekwa wazi, mtu yeyote anaweza kukiona, pazia limepasuliwa. Utukufu kwa Mungu! Kiti chote cha rehema kinaonekana wazi.

118 Jinsi ambavyo Mungu angewarehemu wenye dhambi wachafu sana kama sisi, wakati Yeye alipojificha, ilikuwa ni siri. Na sasa liko dhahiri, ama wazi kabisa, limefunuliwa na Neno Lake. Ni Neno daima, sikuzote, huyo ni Mungu. Neno ndilo linalolifungua. Kama watu hao wangalilijua Neno la Mungu siku hiyo wakati Yesu alipokufa, wangelikiona Kiti cha Rehema, wangeliona Yeye alikuwa ni Nani.

119 "Huyo alikuwa ni Nani basi? Kwa nini pazia likapasuka?" Kumbukeni, ilikuwa ni kifo kuingia Mle. Hakuna mtu angaliweza kumwona. Musa alimwona katika mfano, ilikuwa ni kisulisuli. . .ilikuwa ni m—mgongo wa Mwanadamu. Vema, Huyu hapa, mgongo unaotokwa damu, Mtu yuyo huyo! Ilikuwa ni kitu gani? Mungu alitaka kuwaonyesha kile Kiti cha Rehema. Mungu alitaka kuwaonyesha kwamba Yeye alikuwa ni Nani. Kwa hiyo lile pazia hekaluni, kutoka katika mkono wa Mungu, juu, lilipasuliwa toka juu mpaka chini, na likamwonyesha Mungu dhahiri. Ilikuwa ni Yesu Kristo ameangikwa msalabani, kile Kiti cha Rehema. Na ilikuwa ni kitu gani? Watu walikuwa vipofu sana kuliona.

120 Sasa limejirudia tena, mapokeo yao! Vipi, basi, kwenye ile Siku ya Pentekoste, Neno lilikuja na lilikuwa katika umbo la "Mwana wa Mungu." Nao wakaanza kuliundia madhehebu huko Nikea, Rumi. Na, jambo la kwanza, walishika njia wakaenda kwa Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Pentekoste, na kadhalika. Ni mapokeo yaliyoundwa mpaka mtu hajui mahali anaposimama.

Lakini, utukufu kwa Mungu, Yeye aliahidi katika siku za mwisho yale angefanya.Yeye angeonyesha Neno Lake dhahiri, limefunguliwa mbele zetu tena, mnaona, kulifungua.

121 Kama wangalilijua tu Neno, wangalijua Yesu alikuwa ni Nani. Kama mtu angalilijua tu Neno la Mungu, angejua saa tunayoishi na kile kinachoendelea. Wao wanakataa tu kulisikiliza hilo Neno. Mapokeo yao! Ni kitu gani kiliwafanya wale Wayahudi kuona hilo? Nini? Ilionekana kana kwamba kweli wangeliliona, kwa sababu kitu hicho kilipasuliwa kikafunguliwa. Kilipasuliwa kikafunguliwa kwa kusudi fulani.

122 Uamsho huu unaoendelea sasa ni kwa ajili ya nini? Ungefanikiwaje? Ungebarikiwaje? Sijali una maigizo mangapi, ama chochote kile, hilo halininii. . .Wakati Musa alipotoka,

kulikuwako na kundi mchanganyiko lililoandamana naye. Lakini hilo linafanywa hivyo kwa sababu gani? Ni Yehova Mwenyewe akiondoa utaji kwa Mungu, aonyeshe tofauti kati ya kweli na uongo. Ni lipi, Methodisti, Baptisti, ama Presbiteri, au ni nani aliye sahihi? Neno la Mungu ni kweli! "Neno la kila mtu na liwe uongo, na Langu Kweli." Mungu hahitaji mfasiri yeyote. Yeye hujifasiria Mwenyewe. Hulidhihirisha, na ku-. . . linatoa tafsiri yake. Mungu akijifunua Mwenyewe. Loo, jamani! Moja kwa moja miongoni mwetu, tunauona mkono Wake mkuu ukisema mambo haya, ukifanya mambo haya.

123 Nina jambo fulani juu ya hilo usiku wa leo, unaona, juu ya jinsi ya kuuangalia mkono wa Mungu, yale unayofanya, jinsi unavyojifunua. Unaona?

124 Nao watu wanasema, "Loo, huo ni upuuzi. Huo ni ulokole hapo. Hakuna kitu Hapo. Upuuzi huo. Huyo ni Beelzebuli. Huyo ni shetani. Huko ni kupiga ramli. Hilo ni *hili*." Unaona, jambo lile lile walilosema kumhusu.

125 Ee kanisa, na kama kanda hii ikitoka nje, hivi hamwezi kuona, enyi wahudumu wa Injili, mahali mnapoishi? Hivi hamwezi kuona saa tunayoishi? Mungu, akijionyesha Mwenyewe, akiweka kando. . .Angalieni, Yeye alichukua hilo pazia la hekalu na kulipasua vipandevipande, wapate kumwona Mungu dhahiri, nao walikuwa vipofu mno wasingeweza kumwona. Naye amefanya jambo lilo hilo leo, akiweka Neno Lake moja kwa moja mbele, yale Yeye aliyoahidi. Kila ahadi katika Neno, ikiwa moja kwa moja mbele zetu, dhahiri!

126 Mnajua kile kanisa la Kimataifa linachofanya? Jambo lile lile kanisa la Kiyahudi lililofanya, pofu mno kuliona. Hivyo tu. Litakuwa mioyoni mwao kama tu ilivyokuwa katika siku hiyo.

127 Angalia, kifo, kukaa mbali Nalo sasa. Huna budi kuingia ndani Yake kupitia kwenye pazia hili, la sivyo hutaingia. Jinsi ambavyo Mungu angeweza kuwarehemu, bali kumbukeni vile ilivyokuwa, ya kwamba Mungu anadhihirisha kile kilichokuwa nyuma ya lile pazia. Angalieni kile kilichokuwa nyuma ya pazia, hilo Neno! Lilifunika nini? Neno! Ilikuwa ni kitu gani? Liko kwenye sanduku. Lilikuwa ni lile Neno ambalo lile pazia lililificha. Mnaona? Naye Yesu alikuwa ndiye Neno hilo, Naye Ndiye hilo Neno, nalo pazia la mwili Wake lililificha.

128 Na siku hizi pazia la mapokeo linalificha Neno tena, likisema, "Si hivyo." Lakini ndivyo ilivyo! Mungu analishuhudia, akijitangaza Mwenyewe moja kwa moja mwenye kung'aa kama jua, mbele ya kila mtu, nao wanashindwa kuliona. Mungu, uturehemu.

129 Katika mfano, Musa akija kutoka katika Uwepo wa Mungu, akiwa na Neno la Mungu kwa wakati huo. Sasa angalia, tuko katika Kutoka 19 sasa. Msikose jambo hili sasa. Kutoka 19, Musa anatoka Katika Uwepo wa Mungu, ama 20 na 21, 19:20

na 21. Musa anatoka katika Uwepo wa Mungu. Amekuwa ndani ya Neno. Neno limeandikwa. Naye, akiwa Mbele za Mungu, na Neno, yeye alikuwa na Neno la wakati huo. Kuna Neno kwa kila wakati. Na Musa akitokea, uso wake uling'aa sana! Unaona? Neno lilikuwa ndani yake, tayari kudhihirishwa, litolewe kwa watu.

130 Neno la Kweli, Mungu alikuwa ameliandika, Nalo lilikuwa pamoja na Musa. Angalia, lilikuwa pamoja na Musa na lilikuwa tayari kudhihirishwa. Yeye alikuwa Neno kwao, alikuwa Neno lililo hai, lililofichwa. Alijitia utaji, ilibidi Musa kuweka utaji juu ya uso wake mwenyewe. Kwa nini? Yeye alikuwa ni hilo Neno. Amina. Mpaka Neno hilo lilipotambulishwa, ilimbidi Musa kujitia utaji. Amina!

Mnaona Hilo? Popote lilipo Neno, limetiwa utaji.

131 Musa alikuwa na Neno. Sasa kumbukeni, baada ya Neno kudhihirishwa, Musa alikuwa ni Musa tena. Mnaona? Lakini wakati Neno hilo lilipokuwa ndani Yake lipate kutolewa, yeye alikuwa ni Mungu; vema, yeye hakuwa ni Musa tena. Yeye alikuwa na Neno la Bwana kwa ajili ya wakati huo. Hakuna kitu kingaliweza kumgusa mpaka kipindi hicho kiishe; alikuwa na Neno hilo ndani yake. Kwa hiyo, basi, wakati alipokuja, watu waligeuza vichwa vyao; wasingeweza kufahamu. Walikuwa wamebadilishwa. Yeye alikuwa ni mtu wa tofauti. Alikuja na Neno hilo. "Naye aliweka utaji," Biblia ilisema, "juu ya uso wake," kwa kuwa yeye alikuwa na Neno. Naye alikuwa ni Neno kwao.

132 Sasa angalia, kama Musa...Ee ndugu, hapa patakuwa na tusi. Lakini kama Musa...Kama vile Paulo alivyosema hapa katika Wakorintho wa Pili, mlango wa 3. Kama ilimbidi Musa kufunika uso wake akiwa na Utukufu wa namna hiyo juu yake...unaona, kwa sababu huo ulikuwa ni utukufu wa kawaida, hiyo ilikuwa ni torati ya mambo ya kawaida. Na ikiwa Musa, akijua ya kwamba ilibidi torati hiyo iangamie, bali Utukufu huo ulikuwa ni mkuu sana hata uliwapofusha watu, hata ikabidi waweke utaji juu ya uso wake. Ni zaidi sana vipi itakavyokuwa? Watu waliopofushwa kiroho! A-ha. Huo Utukufu ulikuwa ubatilike, bali Utukufu Huu hautabatilika. Unaona? Musa alikuwa na sheria za kimwili, hukumu, hakuna neema, hakuna chochote; ilikuhukumu tu. Lakini Huu tunaonena kuhusu...Hiyo haikuwa na msamaha, hiyo ilikwambia tu kile ulichokuwa. Huu unakupa njia ya kuepukia.

133 Na wakati Neno hilo linapofunuliwa, loo, jamani, litakuwa na uso wa namna gani? Itabidi litiwe utaji. Halina budi kutiwa utaji. Sasa angalieni. Kwa hiyo Roho anatiwa utaji katika hekalu la kibinadamu, mnaona, Yeye anapaswa kuzungumza maneno ya kawaida akiwa na utaji wa kawaida.

134 Sasa, Paulo akizungumza hapa sasa, na katika mwe—mwelekeo huu, Roho-Neno. "Sisi ni wahudumu, si wa andiko, torati; bali ni wahudumu hodari wa Roho," kwamba Roho huchukua andiko na kulidhihirisha.

135 Hiyo ilikuwa ni torati tu, ilibidi uende ukaiangalie, useme, "Usizini. Usiibe. Usiseme uongo. Usifanye *hili*, *lile*, ama *linginelo*." Mnaona? Ilikubidi kuangalia hilo.

136 Lakini hii ni Roho inayokuja juu ya Neno lililoahidiwa kwa ajili ya wakati *huu*, na inaleta na kudhihirisha, sio vibao viwili vya mawe, bali Uwepo wa Mungu aliye hai. Si wazo fulani la kubuniwa alililobuni mtu fulani, ama Houdini fulani, njama; bali ahadi halisi ya Mungu iliyofunuliwa na kudhihirishwa moja kwa moja mbele zetu. Hilo litakuwa nyuma ya pazia la aina gani? Na ku—kupoteza hilo . . .

137 Mnaona, hilo lilikuwa ni kuu sana mpaka hata watu wakasema, walisema walipomwona Yehova akishuka katika hii Nguzo ya Moto, na kuanza kuitikisa nchi, na—na mambo aliyofanya, na mlima ukiwaka moto. Na hata kama mtu yeyote alijaribu kwenda karibu na mlima huo, aliangamia. Ulikuwa ni mkuu sana hata Musa aliogopa lile tetemeko. Basi, kama wakati huo Yeye aliutikisa mlima pekee, wakati huu atazitikisa mbingu na nchi.

138 Na utukufu Huu je? Kama huo ulifunikwa na utaji wa kawaida, huu ni ninii sana . . . umetiwa utaji wa kiroho. Kwa hiyo usijaribu kuangalia mambo ya kawaida; vunja uingie katika Roho uone mahali ulipo, uone ni wakati gani tunaoishi.

139 Je! lina maana yoyote kwenu? Unaona, ni utaji wa kiroho ulio juu ya watu, wakisema, "Mimi ni Mmethodisti. Mimi ni sawa na mtu mwingine yeyote. Mimi ni Mbaptisti. Na mimi ni Mpentekoste." Hivi hamtambui, kitu hicho ni utaji wa mapokeo? Kinaficha Mungu kutoka kwenu. Hicho ndicho kitu kinachowafanya msifurahie ninii yote . . .

Loo, unasema, "Mimi hupaza sauti na kuruka-ruka."

140 Yeye alisema, "Kila Neno!" Hawa aliamini kila Neno ila moja. Unaona? Ni Neno lote la Mungu, ahadi ya wakati huu ikidhihirishwa. Unaona?

141 Angalieni sasa tunapoendelea. Nina mengi hapa ya kuzungumzia, lakini nina karibu kurasa ishirini, lakini ni . . . za—za mihtasari, lakini si—sitazungumza juu yake yote. Unaona, nitaharakisha.

142 Yeye amefunikwa na utaji wa kawaida kabla hajawazungumzia watu Neno. Sasa, Mungu hana budi kujifunika, kama alivyoahidi, katika mwili wa kibinadamu. Mungu! Mnalipata? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mungu hana budi kujifunika katika mwili wa kibinadamu, na kuweka utaji wa kiroho juu yao, (kusema, "Vema, mimi ni

*hiki* na mimi ni *kile*”), kusudi aseme na watu. Wakati pazia hilo, ambalo ni pazia la mapokeo, linapopasuliwa vipande viwili, basi ninii. . .hivyo ndivyo wanavyosema, “Mbona, siku za miujiza zimepita.”

143 Jamaa fulani aliniambia hivi majuzi, maskini mhubiri wa Kibaptisti huko mahali fulani, alinijia, Ndugu Green, na akasema, “Ndugu Branham, hili hapa jambo moja nililo nalo dhidi yako.” Akasema, “Unajaribu kuwafanya watu. . . ” Ilikuwa ni huko chini kwenye Hoteli ya Ramada, wakati tulipokuwa na mkutano huko chini. Kasema, “Unajaribu kuwafanya watu waamini katika wakati wa kimitume, kuishi siku hizi kana kwamba walikuwa katika wakati wa mitume.” Kasema, “Wakati wa Kimitume uliisha pamoja na mitume.”

Nikasema, “Ati uliisha?”

“Naam.”

Nikasema, “Ni nani aliyekuwa msemaji kwenye wakati wa mitume?”

Akasema, “Wale mitume kumi na wawili kwenye chumba cha juu.”

144 Nikasema, “Basi Paulo hakuwa mmoja wao.” Nikasema, “Msemaji alikuwa ni Petro. Na Petro alisema, kwenye ile Siku ya Pentekoste, walipoona haya yote yakiendelea, na Roho Mtakatifu akitenda kazi, yeye alisema, ‘Ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa hao walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.’ Kama Yeye angali anaita, basi Jambo lile lile lipo hapa. Wakati wa mitume uliisha lini basi? Wakati wa mitume unaisha wakati Mungu anapoacha kuita.” Hakusema lolote ila aliichukua kofia yake akaondoka.

145 Inachukua Neno kufanya jambo hilo. Ni Neno. Yesu alimwambia Shetani, “Imeandikwa.” Mnaona? Jambo ndilo hilo, “Imeandikwa.”

146 Nikasema, “Petro alisema ya kwamba hautaisha kamwe. Wote watakaoitwa na Bwana wamjie, Baraka hii ilikuwa ni kwa ajili yao. Sasa mnasema, ‘Alikoma.’ Lini?”

“Hakuna madhara yaliyofanywa?”

Nikasema, “La, bwana, hata kidogo. Endelea.” A-ha. Papo hapo. Mnaona?

147 Petro alisema ilikuwa ni kwa kila Mtu atakayeitwa na Mungu amjie, angepokea Baraka ile ile ya kimitume. Hilo ni— hilo ni Neno la Bwana. Unaona?

148 Sasa utaji wa kawaida. Mungu, Neno, akiwa katika pazia la mwili wa kibinadamu. Ilikuwa ni kitu gani? Mungu alitiwa utaji katika Musa. Mungu alikuwa ndani ya Musa, ametiwa utaji, na Uwepo wa Mungu ulikuwa ndani yake. Yeye alikuwa mkamilifu sana akiwa na Neno ndani yake namna hiyo, hata ilimbidi kuutia

utaji uso wake. Na alikuwa ni nabii aliyethibitishwa aliyelifunua Neno na kuwaambia, “Msininii! Mtaninii! Na hamtaninii!” Unaona?

149 Kukipa kizazi hicho Neno Lake, Yeye alijifunika pazia katika Mwanadamu, la sivyo Neno lingaliwapofusha hata walioitwa watoke. Unaona? Hata watu waliokuwa huko nje, wasingeweza kuvumilia kuona jambo hilo. Katika—katika Kutoka tunaona ya kwamba, wao walisema, “Acha Musa aseme, sio Mungu.” Mnaona ni kwa nini Nguzo ya Moto haitokei mara nyingi mno? Mnaona?

150 Mungu alisema, “Mimi—mimi—mimi nitafanya hivyo. Nitawaondokeshea Nabii.” Amina! “Nitawaondokeshea mmoja.” Naye akaja vivyo hivyo hasa. “Nitawaondokeshea, Naye atakuwa, atakuwa ni Neno.”

151 Akasema, “Kama wanataka kuona kwamba Neno ni nini . . . ” Kasema, “Sasa, Musa, nilikutokea huko ng’ambo, kile kichaka kilichowaka moto.” Kasema, “Nitashuka na kuuwasha moto mlima huo.” Kasema, “Wataona ya kwamba umesema kweli. Nitaonekana hapa katika—katika njia iyo hiyo ya moto. Nitaonekana hapa na kuwathibitishia watu, nitaithibitisha huduma yako.” Hayo ndiyo Yeye aliyomwambia Musa hapa, kwa maneno mengi.

152 Angalieni, Yeye alisema, “Sasa nita—nitakutukuza wewe mbele za watu.” Kasema, “Sasa, wewe uliwaambia ya kwamba nilikutana nawe pale kwenye kichaka kilichowaka moto; sasa nitashuka, Moto ule ule, Nami nitawaacha watu waone ya kwamba hukusema uongo juu ya jambo hilo.” Hata unaweza kuthibitisha jambo hilo kisayansi, ukitaka. Unaona? “Nitashuka moja kwa moja na kuwafanya wajue.”

153 Ndipo wakati alipoanza kunguruma, wakati Yehova alipoanza kunguruma, hao watu walisema, “La! La! La! Usiache Yehova aseme; tuta—tutakufa.”

154 Mnaona, ilimbidi kutiwa utaji, kwa hiyo Mungu Mwenyewe alijitia utaji katika Musa na kumpa Musa Neno. Ndipo Musa akashuka na kunena Neno la Bwana, huku ametia utaji juu ya uso wake. Hiyo ni kweli? Yehova akiwa ametiwa utaji katika mfano wa nabii, kwa kuwa ingekuwa ninii kabisa . . . Na Mungu akasema asingenena nao tena namna hiyo. Yeye angesema nao kwa nabii pekee. Hivyo ndivyo tu angenena tangu wakati huo na kuendelea. Hivyo ndivyo tu alivyowahi kunena. Hiyo ni kweli. Si kwa njia nyingine yoyote. Yeye hasemi uongo.

155 Angalieni, Musa pekee ndiye aliyekuwa na Neno. Sasa, hapakuwapo na ku—kundi lililoshuka likaja, hakukuwako na Mafarisayo tu, ama Masadukayo, ama haikuwa ni dhehebu fu—fulani ama ukoo. Ilikuwa ni Musa! Yeye alimchukua mtu mmoja. Yeye hawezi kuwachukua watu wawili ama watatu tofauti. Yeye humchukua mtu mmoja. Musa alikuwa na Neno, na Musa

peke yake. Yoshua hata hakuwa nalo. Hakuna mtu mwingine aliyekuwa nalo. Amina! Yoshua alikuwa ni je—jemadari; Yoshua alikuwa ni amiri jeshi wa jeshi; Yoshua alikuwa ni mwaminio, Mkristo. Lakini Musa alikuwa ni nabii! Neno haliwezi kumjia Yoshua; halina budi kumjia Musa. Yeye alikuwa ndiye nabii mkuu wa wakati huo. Angalieni, Neno kamwe halikumjia Yoshua mpaka Musa alipokuwa ameondoka. La, bwana. Mungu hutenda kazi na mtu mmoja kwa wakati mmoja. Mungu ni mmoja. Mnaona? Sasa, Musa tu ndiye aliyekuwa na Neno, sio kundi.

156 Angalia, Mungu alimwonya mtu yeyote asijaribu kumfuata Musa kuingia kwenye pazia hilo; waigaji. Mnaona? Mwanamke, mwanamume, kuhani, yeyote yule, awe mcha Mungu jinsi gani, awe mwanamume jinsi gani, awe mheshimiwa jinsi gani, hata wawe jinsi gani; Yeye aliwaonya, "Acheni Musa aje peke yake! Na kama mtu yeyote, hata mnyama, akiugusa, hana budi kuuawa papo hapo." Msipenye mkaingie mbele ya pazia hilo. Pazia hilo ni la mtu mmoja. Ujumbe huo ni mmoja. Mnaona? Hekaluni, mtu mmoja aliingia mara moja kwa mwaka, ametiwa mafuta na kutayarishwa kuingia; sio kulileta Neno, bali kutoa dhabihu ya damu. Hata kwenda mle ndani mbele Yake, ni mmoja tu. Mtu mwingine yeyote alikufa. Mnaona?

157 Wanakufa kiroho sasa. Huu ni utaji wa kiroho. Unaona? Huo ulikuwa ni utaji wa kawaida. Huu ni utaji wa kiroho. Unaona? Wanaendelea kutembea moja kwa moja kuingia kule nyuma, unaweza kuwaambia. "Loo, najua! Ninajua hilo, bali mimi . . . "

Nilisema, "Endeleeni, ni sawa, linanena tu . . . " Mnakumbuka, pigo la mwisho kule Misri lilikuwa ni mauti, kabla ya kule kutoka. Pigo la mwisho duniani ni mauti ya kiroho, kabla ya kule kutoka. Ndipo maiti yao itachomwa moto na kurejeshwa mavumbini, nao wenye haki watatembea juu ya majivu yao. Lakini jambo la mwisho ni mauti ya kiroho, kulikataa Neno.

158 Sasa angalieni, Mungu aliwaonya watu wowote wasijaribu kumfuata Musa kuingia katika pazia la Moto. Musa alikuwa atiwe utaji, ilibidi atoke mle. Musa aliingia kama Musa, aliingia katika Nguzo hii ya Moto; na wakati alipotoka nje, alikuwa ametiwa utaji. Kwa kuwa, yeye aliingia Mle, kutoka katika mapokeo yake, mapokeo ya wazee. Alikuwa *ameiona* Nguzo ya Moto, bali sasa anaingia *ndani* ya Nguzo ya Moto. Mnaona? Amina! Ndipo akatoka, ametiwa utaji. Neno la Mungu katika mwanadamu, limetiwa utaji! Huyu hapa yuaja akitoka, loo, jamani, ninaweza kuona jambo hilo. Alimwonya mtu mwingine yeyote asijaribu hilo, hakuna mtu anayeweza kuiiga Hiyo. Afadhali usiige. Mnaona? Hata kuhani ama mtu mtakatifu, yeyote yule, kadinali, askofu, chochote kile, kilichojaribu kuingia kwenye pazia hilo, kilikufa. Mungu aliwaonya. Hatutakuwa na uigaji wowote.

159 Neno Lake linafunuliwa kwa mmoja. Daima imekuwa hivyo, nabii alikuja na Neno la Bwana, kila kipindi cha wakati, kila wakati, kote katika Maandiko. Neno humjia mmoja. Katika kila wakati, vivyo hivyo, hata katika nyakati za kanisa, tangu wa kwanza hadi wa mwisho. Wengine wana mahali pao, hiyo ni kweli, angalia, lakini kaeni mbali na hiyo Nguzo ya Moto. Unaona? Ni somo la jinsi gani tunalosoma hapa! Unaona, kila mtu akitaka kuwa Musa, na kila mtu . . .

160 Mnakumbuka yale Dathani na hao wengine waliyosema kule njiani? Walisema, "Sasa, Musa, hebu ngoja hapa kidogo tu! Unajitukuza sana, unaona. Sasa, wapo watu wengine hapa ambao Mungu amewaita."

161 Hiyo ni kweli. Wao, kila mmoja, walikuwa wakifuata vizuri mradi tu waliendelea mbele, lakini wakati mmoja alipojaribu kuinuka na kuchukua nafasi ya Mungu ambayo alikuwa amempa Musa, ambaye alikuwa amekusudiwa tangu zamani na kuchagulia kwa ajili ya kazi hiyo, alipojaribu kupachukua, moto ulishuka na ukaifunua nchi na kuwameza moja kwa moja ndani yake. Unaona? Unaona? Kuwa mwangalifu. Unaona? Kuwa mwema tu, Mkristo wa Mungu mcha Mungu, ukiliamini Neno. Unaona? Kaa mbali na hiyo Nguzo. Ni somo la jinsi gani!

162 Mungu kwanza alikuwa amemtokea Musa katika kichaka kilichowaka moto, Mungu alikuwa amejificha kwenye pazia la Nguzo ya Moto. Sasa sikilizeni kwa makini sana kwa dakika moja. Mungu, alipomtokea Musa kwanza, Yeye alikuwa nyuma ya pazia. Mungu alikuwa katika Nguzo ya Moto, amejificha huko nyuma ya kichaka, unaona; kama vile nyuma ya ngozi, unaona, huko nyuma kwenye kiti cha rehema madhabahuni. Unaona? Alikuwa amejificha nyuma ya pazia. Yeye daima yuko nyuma ya pazia. Na wakati alipomjia Musa, Yeye alikuwa katika Nguzo ya Moto, amejificha nyuma ya pazia la Nguzo ya Moto. Lakini hapa, mbele za watu, Mungu alimthibitisha kwa Nguzo ile ile ya Moto. Unaona? Musa alisema . . .

163 Sasa angalieni. Hivi mnasoma? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Je! mnaziacha akili zenu zipeperushwe mbali? Mnaweza? Mnaweza . . . "Yeye aliye na maskio, na asikie." Unaona?

164 Wakati Mungu alipomtokea Musa, ilikuwa ni katika Nguzo ya Moto, wakati Yeye alipomwita kwenye huduma yake. Ndipo Musa akaja na kuwaambia watu kuhusu jambo hilo. Wasingeweza kuamini jambo hilo, ingawa alifanya miujiza na mambo kadha wa kadha. Lakini, wakati huu, Yeye alijitokeza waziwazi, kisayansi na kuithibitisha huduma ya Musa kwamba ni Mungu yeye yule aliyesema naye, maana alitokea katika sura ya Nguzo ya Moto na akauwasha mlima moto. Nayo ilimjia Musa katika kichaka, ikasema naye. Vema.

165 Mungu kumtokea Musa, kwa mara ya kwanza, katika kile kichaka kilichowaka moto, pazia. Mbele za watu, Mungu alijitia utaji tena na kumthibitisha Musa, kwa utaji, kwa kujitia utaji kwa Moto ule ule, Nguzo ile ile ya Moto ilishuka. Tangu—tangu wakati huo . . . Kutoka kwao, kwa hiyo wangeweza tu kusikia Neno la Mungu. Mnalipata? Neno pekee, waliisikia Sauti Yake. Kwa kuwa, Musa alikuwa, kwao, Neno lililo hai. Musa! Mnaona, Mungu alikuwa amelithibitisha Neno hilo sana kwa kumtumia Musa! Mnaona, Musa alisema . . . Mungu alimwambia Musa, "Shuka uende kule chini. Nitakuwa pamoja nawe. Yeye ni . . . Hakuna kitu kitakachosimama mbele yako. MIMI NIKO AMBAYE NIKO."

166 Musa alishuka, na kusema, "Huenda msiamini jambo hili, labda, bali Mungu alinitokea katika Nguzo ya Moto na kuniambia mambo haya."

167 "Loo, tuna kila namna ya mambo yanayoendelea." Farao alisema, "Mbona!" Mchungaji Farao alisema, "Vema, una ujanja rahisi wa kichawi. Mbona, ninao wachawi hapa wanaoweza kugeuza nyoka akawa . . . kijiti—kijiti kikawa nyoka. Njoni hapa, enyi wachawi." Nao wakaja pale na kufanya jambo lile lile.

168 Musa alijua. Hakuna kitu kilichomsumbua. Kwamba walikuwa na waigaji wangapi, haikuleta tofauti yoyote. Musa alisimama kimya tu. Muda si muda wajua, walitambaa huku na huku kidogo, na, mara, nyoka wa Musa aliwala hao wengine tu. Mnaona? Kwa nini? Kama ilivyokuwa kwa wale mitume, hawakuweza kuelezea jambo Hilo. Musa hakujua jinsi ambavyo Mungu angeenda kufanya jambo hilo, bali alikuwa yuaenda kulifanya.

169 Kumbukeni, Yeye alisema Yambre na Yane watarudi katika siku za mwisho, unaona, kuiga. "Nao wangewadanganya walio wateule kama yamkini," Mathayo 24:24. Unaona? Ni mambo yale yale kabisa, watafanya miujiza ya aina ile ile na kadhalika. Angalia hilo Neno! Angalia hilo Neno! Mtu anasema anafanya mwujiza na angali anataka kuamini kuna Miungu watatu, na kuna wa namna hizi zote; achana nao wa aina hiyo. Tunajua hilo—hilo ni kosa, mnaona, hakuna kitu kama hicho. Mnaona? Neno, kila Neno, kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu! Mwanzo, Neno moja! Hapa, ilisema, "Usiondoe wala kuongeza neno moja." Unaona, halina budi kuwa ni Neno lile lile. Mnaona?

170 Angalia, watu waliona jambo ambalo lilikuwa limetukia. Musa alikuwa ametiwa utaji kama nanii . . . Yeye alikuwa ni nabii, na Mungu alikuwa amethibitisha Neno Lake sasa, akashuka akaenda kule. Naye aliona ishara na maajabu. Na halafu, vema, watu hawa wakajitenga wenyewe, kanisa. Mnaona, *kanisa* maana yake ni "walioitwa watoke." Mnaona? Baada ya wao kuitwa kutoka ulimwenguni na wakawa watu, mnaona, ndipo Mungu alijitambulisha kwamba Yeye alikuwa

ndiye hiyo Nguzo ya Moto. Yeye aliuthibitisha Ujumbe wa Musa. Mnaona? Yeye alikuwa ndiye ile Nguzo ya Moto. Huenda waliipiga picha, nafikiri, kama wangalikuwa na kamera, maana wote ulikuwa ukiwaka Moto. Lakini wao—walithibitisha jambo hilo, Mungu akithibitisha ya kwamba Ujumbe huo ulikuwa ni wa kweli. Ujumbe ulikuwa umewadia, kila kitu kilikuwa, walikuwa watatolewa wakati ule. Akamtia utaji nabii Wake kwa hawa watu wa kutoka.

171 Hao watu, wazieni, waliona jambo fulani lilikuwa limempata. Sasa yeye alikuwa tofauti na Waisraeli hao wengine. Alikuwa ni wa tofauti, ujumbe wake ulikuwa ni wa tofauti, alikuwa tofauti na makuhani, alikuwa tofauti na chochote kile. Unaona, alikuwa ni mtu wa tofauti. Watu waliona jambo fulani lilikuwa limetukia. Mungu alikuwa amejificha nyuma ya pazia la nabii Wake, apate kuwaambia Neno Lake. Hilo ndilo alilokuwa amefanya. Musa alikuwa ndiye hilo Neno lililo hai kwa watu, lililotiwa utaji kwa Nguzo ya Moto, likinena kile kitakachotiwa utaji baadaye nyuma ya ngozi za pomboo. Mnaona?

172 Ilibidi Neno litoke kwa Musa, kwanza. Mnaona? Musa alikuwa na Neno. Yalikuwa yameandikwa na Mungu, hakuna mtu angaliweza kuyafasiri, ilimbidi Musa ayafasiri, kwanza. Hiyo ndiyo sababu yeye alitia uso wake utaji, maana yeye. . . Mnaliona? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaona?

*Hii* hapa. [Ndugu Branham anaichukua Biblia yake—Mh.] Tungeweza kuichukua, tuibebe, na chochote kile pale, bali haina budi kufunuliwa. Kusudi apate kulifunua, ilibidi Musa awe ni Mungu kwa watu hao.

Mnasema, "Upuuzi huo."

173 Mbona, Yeye alisema, hata alimwambia Musa, Yeye Mwenyewe, "Wewe utakuwa Mungu, naye Haruni atakuwa ni nabii wako! . . .?. . . " Unaona? Kwa hiyo huyo hapo anakuja, unaona, ilimbidi Mwenyewe kujitia utaji, maana Mungu daima yuko nyuma ya pazia. Loo, jamani! Mnaliona? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mungu amefichwa kutoka kwa watu.

174 Kasema, "Baba, ninakushukuru, Wewe umelificha kwa wenye hekima na akili, na kuwafunulia watoto wachanga, hao wanaotaka kujifunza." Mnaona?

175 Mungu alijificha nyuma ya pazia. Musa aliuficha uso wake. Musa alikuwa ni Neno lililo hai lililotiwa utaji wakati huo. Watu waliiona hiyo Nguzo ya Moto, wakasema, "Sasa tumeridhika." Unaona? "Hebu Musa anene." Unaona? "Usiache Mungu anene, tusije tukafa." Musa aliingia moja kwa moja kwenye hiyo Nguzo ya Moto. Mnaona?

176 Kisha akasema sasa, Yeye alisema, "Sasa si—sitanena nao tena namna hii. Nitawapa nabii." Mnaona? Na hivyo ndivyo alivyofanya daima. Mnaona? Kasema, "Sasa acha waende." Lakini nabii huyu hana budi kuwa na Neno hili. Kama akitiwa

utaji kwa mapokeo, Mungu kamwe hakumtuma. Kama ametiwa utaji kwa Neno, Mungu atalithibitisha. Mungu hulifasiri Neno Lake Mwenyewe. Musa aliyanena; Mungu akayafasiri. Amina.

177 Musa alisema, "Bwana alisema hivyo!" Naye Bwana akafanya yale hasa aliyosema. Hilo lililifanya sahihi.

178 Sasa Yeye alisema, "Sasa, Musa, unafahamu. Watu wanafahamu sasa. Unaona, nimekuonyesha, nimekuthibitisha." Mungu alikuwa amejitia utaji katika nabii huyu, apate kuwaambia watu Neno Lake. Musa alikuwa ni Mungu aliye hai kwao, Neno la Mungu lililo hai likidhihirishwa. Hiyo ndiyo sababu uso wake umetiwa utaji. Unaona?

179 Na je! mnajua kitu kile kile katika Mkristo wa kweli kimetiwa utaji leo, kwa wasioamini? Wanawaona hao wanawake wenye nywele ndefu na kadhalika, wanasema ni . . . "Hebu angalieni yule mtindo wa kale." Wanawake husokota nywele zao mgongoni mwao, wakasema, "Ana tairi lililokwisha pumzi, tairi la akiba pale juu." Unaona, yote imetiwa utaji. Wao ni vipofu. "Loo," wanasema, "Nina Ph.D, L . . . " Sijali una kitu gani, ungali hulijui Neno. Kweli kabisa. "Loo, hilo, hilo ni jambo dogo tu. Mimi . . . " Chukua mafunzo madogo kwanza.

180 Vipi kuhusu watu wanaosema ya kwamba wametiwa utaji Mbele za Mungu, na wanahubiri mapokeo fulani ya kanisa? Loo, rehema, Mungu wangu! Ambao wanaongeza kwake na kuondoa kwake, na chochote kile, kwa kuingiza masomo yao wenyewe na mawazo yao wenyewe, wala si Neno la Mungu, mnaona, ni utaji wa aina gani? Hao wana utaji wa kikanisa. Mungu ameupasua utaji huo ukafunguka wazi kabisa!

181 Wao walisema, "Hakuna kitu kama manabii. Hakuna kitu kama hicho, katika siku hizi za mwisho, kama mitume na manabii. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Hakuna kitu kama waonaji, tena. Hakuna kitu kama Marko 16 ikitimizwa. Wakati wa mitume umekwisha." Walilitia utaji kutoka kwa watu. Lakini Mungu alitoka nje moja kwa moja na Roho Wake Mtakatifu wa Moto, na kukipasua kitu hicho toka juu hata chi- . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Mungu amelipasua pazia.

182 Musa alikuwa ndiye pazia, Neno la Mungu lililo hai limetiwa utaji nyuma ya mwili wa binadamu. Ile Nguzo ya Moto ilikuwa ndani ya Musa, hakika, ikinena kile kitakachotiwa utaji baadaye nyuma ya ngozi, mnaona.

183 Sasa, hilo, Neno, Neno lililetwa, kisha likaandikwa, halafu likawekwa nyuma na lingali limetiwa utaji, kwa maana Mungu daima alikuwa katika Neno hilo. Amina! Yeye ni Neno, daima. Yeye alikuwa katika Neno hilo. Hiyo ndiyo sababu ilibidi Neno hilo litiwe utaji.

184 Loo, ndugu, dada, hivi mnalishika? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Angalieni! Hivi hamwoni? Limekuwa na utaji

kote katika nyakati hizi, kulingana na yale Mungu aliyosema, nalo litafunguliwa katika siku za mwisho, hiyo Mihuri Saba itavunjwa, na Kitu hicho chote kitaonekana wazi kabisa kwa watu, yale yaliyotukia kotekote. Katika saa ya Ujumbe wa malaika wa saba, siri zote za Mungu zinapaswa kujulikana katika huyo Eliya, saa hii ya mwisho; jinsi ambavyo Kristo ametupwa nje ya kanisa Lake, Mwana wa Mungu; jinsi ambavyo anafunuliwa kama Mwana wa Adamu tena; jinsi ambavyo Kanisa litawekwa katika utaratibu, na kila kitu kwa ajili ya siku ya mwisho, hakuna kanuni za imani, hakuna dhehebu, ni Neno tu kabisa likiishi katika mtu binafsi. "Nitachukua mmoja, na nimwache mmoja. Nitamchukua *huyu*, na kumwacha *yule*." Mnaona? Kuna ninii tu. . . Hakuna kamba, hakuna madhehebu, hakuna kufungwa wala chochote kile; ni moyo kuwa pamoja na Mungu, na Yeye peke Yake. Mnaona?

185 Angalia, ametiwa utaji katika mwili wa binadamu. Musa akiwa na Neno hilo, akinena kile kitakachowekwa nyuma ya ngozi ya pomboo baadaye. Ili kwamba. . . Vivyo hivyo na Kristo ndiye Musa wetu. Kristo ndiye Musa wetu. Yeye alikuwa ni Mungu aliyetiwa utaji katika mwili wa binadamu, kutiwa utaji katika ubinadamu, katika mwili. Hiyo ni kweli. Naye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye alitiwa utaji kwa ngozi za pomboo. Alikuwa ametiwa utaji. Na wakati huu alitiwa utaji katika Mwanadamu. Mnaona? Sasa angalia, "yeye yule jana, leo, na hata milele," aliahidia Neno Lake kwa wakati *huu*. Yeye angali ni Kristo, Neno lililoahidiwa la wakati huu, lililotiwa utaji katika mwili wa binadamu. Neno ni Mungu.

186 Ule upako ni mtu. Neno *Kristo* maana yake ni aliyetiwa mafuta, mnaona, "aliyetiwa mafuta." Basi, Musa alikuwa ni Kristo katika siku zake, alikuwa ndiye mtiwa mafuta. Yeremia alikuwa ni Kristo katika siku zake, akiwa na sehemu ya Neno kwa siku hizo.

187 Lakini wakati Yesu alipokuja, Yeye alikuja kama Mkombozi Aliyetiwa Mafuta; na huyo alikuwa vyote viwili ni Musa na yote yaliyokuwa ndani ya Musa, na Neno lote, na Uungu wote kwa jinsi ya mwili ulikuwa ndani Yake. Hiyo ndiyo sababu pazia lote la hekalu lilipasuka, nacho kiti cha rehema kikaonekana wazi kabisa, Yeye alikuwa ndiye Mtiwa mafuta.

188 Angalieni sasa, ule utaji katika mwili wa binadamu, Neno lililoahidiwa la wakati huu halina budi pia kutiwa utaji. Angalieni. Wafuasi wa kanisa wanaopenda dhambi na wenye dhambi hawawezi kuliona kwa sababu ya pazia la binadamu.

189 Hiyo ndiyo sababu wasingeweza kumwona. "Mbona, Yeye ni mwanadamu. Alitokea wapi? Ana kadi gani ya ushirika? Yeye ni mfuasi wa kanisa gani?" Ninataka kuzungumza juu ya hilo usiku wa leo. "Yeye ni wa kanisa gani?" Mnaona? Na kwa hiyo, mnaona, sasa, "Yeye ni wa kanisa gani, ni wa kundi li—lipi?

Alipata masomo gani? Alipata wapi elimu Yake? Vema, Mtu huyu alizaliwa, kulingana na mapokeo, ama kulingana na—na hadithi Zake mtaani hapa, Mtu huyu alizaliwa nje ya ndoa takatifu. Mbona, Yeye, hakika, Yeye ni wa ibilisi. Mnaona, Yeye—Yeye ni wa ibilisi. Yeye alizaliwa nje ya ndoa takatifu, na Yusufu alimwoa tu yule mwanamke kuzuia asije akapigwa mawe, maana alikuwa ni mzinzi. Na ati Mtu huyo aje huku atwambie sisi makuhani la kufanya?"

190 Na huyo hapo Mungu amesimama pale, akilifunua hilo Neno, akisema kwa sauti kuu, "Mungu Wangu, mbona umeniacha?" Nyimbo zile zile walizokuwa wakiimba hekaluni, ambazo Daudi alikuwa amewatungia miaka mingi iliyopita, kumhusu Kristo. "Mifupa Yangu yote imetenguka. Waliichoma Mikono Yangu na miguu Yangu." Na hao hapo wamesimama pale, wakiuimba huo, na Mtu yuyo huyo akifa msalabani. Basi wakati walipomaliza na ninii . . .

191 Hapo alipokufa, Mungu wa Mbinguni alishuka, kama alivyofanya juu ya Mlima Sinai, pamoja na Moto Mtakatifu, na kulichoma hilo pazia la hekalu toka juu hata chini, akalipasua vipande viwili. Nao wangefanya nini? Waliangalia huko nje moja kwa moja kupitia dirisha la hekalu, hapo Kalvari, na huyo hapo Mungu akionekana wazi, ile Dhabihu.

192 Lakini hawalioni bado, siku hizi. Mungu katika siku hizi za mwisho ameyapasulia mbali hayo mapokeo, na kulifanya Neno la wakati huu dhahiri kabisa, na wangali hawajui jambo Hilo. Hawalijui kamwe. Ni—ni rahisi sana. Mnaona, ni rahisi tu. Liko mbali sana na mambo ya ulimwenguni.

193 Nilihubiri hivi majuzi kwenye kusanyiko fulani, juu ya, "Kuwa nati." Moja ya siku hizi ninataka kuhubiri juu ya hilo, "Kuwa nati." Sisi sote ni nati kwa mtu mwingine, kwa hiyo—kwa hiyo nitakuwa moja kwa Kristo. Paulo alisema alikuwa "amehesabiwa kuwa mjinga." Hakika, inakubidi kuwa. Mnaona, inahitaji nati kushikilia vitu pamoja. Mnaona? Hiyo ni kweli.

194 Kwa hiyo angalia ule utaji, mwili wa binadamu. La, sasa, watu wanaopenda dhambi wasingeweza kuona jambo hilo. Hao watu wa kidini wenye mapokeo, hawakuweza kuliona hilo, kwa kuwa Yeye alikuwa ni mwanadamu. Kwa nini? Mwili huo wa kibinadamu ulimficha Mungu.

195 Sasa, kama Yeye angalikuwa Nguzo kuu ya Moto iliyoshuka chini, mnaona, Nguzo kuu ya Moto ilikuwa imeshuka na kuwaonyesha kwamba Yeye alikuwa ni nani, ya kwamba alikuwa ni Nguzo hii kubwa ya Moto, huenda wangaliamini jambo hilo; kama Yehova angalizunguka huku na huko.

Lakini mnaona kile alichofanya, kusudi aweze kuwaruka hao watu wote werevu, wenye hekima, Yeye alijifunua tu kama alivyomwahidi Musa, unaona, "Nitanena nao kupitia Nabii." Naye alikuwa ni Mwana wa Adamu, Nabii. Na baadhi yao

walilitambua jambo Hilo, yapata asilimia ya asilimia moja ya ulimwengu, waliliamini; hao wengine hawakuliamini. Lakini, Yeye alikuwa, vivyo hivyo.

196 Lakini huyo hapo Mungu Mwenye nguvu amesimama akionekana dhahiri kabisa, kile Kiti cha Rehema! Yeye alikufa wakati watoto Wake Mwenyewe wakisema. . . Watoto Wake Mwenyewe pale, wakisema, "Hatumtaki! Mwondoshe!" Wakamtemea mate.

197 Mfano, huko nyuma kabisa, wakati Daudi alipokuwa akiondoka hekaluni, mfalme aliyekataliwa. Akashuka akipita barabarani, na maskini jamaa mdogo kiwete akitambaa, kamwe hakumpenda, alimwita "maskini mnafiki" ama kitu fulani, akamtemea mate moja kwa moja usoni mwake. Ndipo huyo mlinzi akauchomoa upanga, kasema, "Je! nitaacha kichwa cha yule mbwa kikae juu yake; na amemtemea mate mfalme wangu?"

198 Daudi akasema, "Mwache, Mungu alimwambia hivyo." Daudi labda hakujua alilosema. Alipanda juu ya mlima, akiangalia nyuma, akilia.

199 Miaka mia nane kutoka hapo, Mwana wa Daudi alikuwa akipanda mlima ule ule, akiangalia huko mbali, akiulilia Yerusalemu, Mfalme aliyekataliwa. Nao wakamtemea mate usoni Mwake.

200 Hivi hamwoni? Ni jambo lile lile. Mnaona Neno hilo likishuka kuja, likifuatilia leo hii? Daima linakataliwa na walio wengi, mnaona, na kuaminiwa na walio wachache.

201 Sasa, angalieni, wasingeamini jambo Hilo. Hao Wayunani, wasingeweza kumwona, Yeye alikuwa katika hekalu Lake la binadamu. "Mbona," wao walisema, "jina la mtu huyu ni Yesu; Yeye anatoka Nazareti."

202 Sasa, walikuwa na jina moja tu huko siku hizo. Kama vile, "Yohana, Jim," wangesema, "Yohana kutoka Jeffersonville, Jim kutoka New Albany," ama kitu kama hicho, mnaona.

203 Yeye alisema, "Huyu ni Yesu kutoka Nazareti. Inaaminiwa na wengi kwamba mama Yake alitiwa mimba na askari." Mnaona? Halafu basi hilo ndilo waliloamini hasa. Hakika! Na kasema walisema, sasa, "Na huyu ni Yesu wa Nazareti." Mnaona? "Ni Nani?" Mnaona, hawakuweza kufahamu Hilo.

204 Lakini, mbona, Neno hili siku hiyo, wakati alipokuwa akihubiri, alisema, "Yachunguzeni Maandiko. Ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele, Nayo yanashuhudia kwamba Mimi ni Nani. Kama hamwezi kuniamini; mnisahau Mimi, kama pazia, aminini Neno linalotoka. Wawili ni mashahidi," Yeye alisema, "Mimi ninanena na Baba ananena kwa niaba Yangu." Amina. Hiyo ni kweli.

205 Ninazungumza juu ya Neno la siku hii, na Baba analithibitisha. Sasa je! huo si ni ushuhuda kwenu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ndio, mnaona. Hivyo ndivyo inavyopaswa kutimizwa.

206 Angalia katika Wakorintho wa Pili sasa, ninii . . . katika Wakorintho wa Pili, mlango wa 3, kifungu cha 6, lile hekalu la kale lilimpa Mungu makao nyuma ya ngozi za kale, kutoka kwa Wayahudi. Wakati lile pazia la kale lilipopasuliwa, bado Wayahudi . . . walipofushwa kujua Yeye alikuwa ni Nani, wangali hawajui kwamba Yeye ni nani. Na basi Pentekoste ilifunua kwamba Mungu wa kweli na aliye hai alikuwa ni Nani, wakati hilo pazia lilipokatwa vipande viwili, na Mungu, kutoka juu. Kwa nini pazia hilo likafanya hivyo? Kwa nini likafanya hivyo?

207 Kwa nini kulitokea Ujumbe kama huu leo kufanya yale umefanya? Kwa nini ukaja? Ni kwa nini?

208 Kuna mtu aliyekuwa anipigie simu, siku moja hapa si muda mrefu uliopita, alitaka kuhojiana nami juu ya zile—zile nyakati za kanisa, ya kwamba, "Mungu alikuwa katika kanisa lake takatifu," na mambo kama hayo. Na nikatambua kwamba ilikuwa ni mwanamke mhubiri, nami nikalisahau tu jambo hilo. Mnaona, kama ingekuwa ni mwanamume fulani hilo lingekuwa ni sawa, lingekuwa ni tofauti. Lakini, kwa hiyo, lakini kuna haja gani ya kwenda moja kwa moja mpaka nchi nyingine kule, wakati inanibidi kuacha mkutano hapa kufanya jambo hilo, mnaona? Kwa hiyo niliachana tu nao. Kipofu akimwongoza kipofu, wote wanaanguka shimoni.

209 Kwa hiyo, kwa hiyo sasa katika wakati huu, wakati ule utaji wa kale wa kimadhehebu na mapokeo umepasuliwa, kutoka kwenye Neno la Mungu, kusudi lipate kudhihirishwa! Mnaona ninalomaanisha? Mapokeo yanasema, "Mambo hayo yote yamepita." Hebu hilo likolee kidogo. "Mambo hayo yamepita." Lakini, katika siku hii ya mwisho, huo utaji wa mapokeo umepasuliwa, na hii hapa Nguzo ya Moto imesimama. Mnaona? Huyu hapa, akidhihirisha Neno kwa ajili ya siku hii. Pazia limepasuliwa.

Sasa, ulimwengu, bado hawaamini jambo Hilo. Haidhuru nini, hawalioni. Hawalioni. Halikutumwa kwao.

210 Kumbuka, Mwana wa Mungu hakufunuliwa kwa Sodoma; wajumbe wawili ndio waliofunuliwa. Hiyo ni kweli.

211 Lakini, jambo hili, Mungu Mwenyewe katika mwili wa binadamu alifunuliwa kwa Ibrahimu, yule Mteule. Basi angalia kile alichofanya kujifunua Mwenyewe. Na sasa Ibrahimu alijua, wakati Yeye alipojua kilichokuwa katika wazo la Sara nyuma yake, yeye alisema, alimwita Yeye, "Elohimu! Mtumishi Wako . . . "

212 Angalia sasa, kusudi liweze kudhihirishwa. Neno limekuwa na utaji miaka hii yote, kwa watu, "Haliwezi kutendeka."

213 Mnakumbuka lile somo nililohubiri ile asubuhi wakati nilipoondoka hapa kwa mara ya kwanza, kuhusu Goliathi na Daudi? Nilisema, "Mtazameni yule mpinzani kule nje, akisema ya kwamba 'siku za miujiza zimepita.'"

Tazameni hizo kanda zinavyofuatana, tazameni kila moja, jinsi imekuja ikiwa dhahiri zaidi na zaidi; kama mna masikio ya kusikia, mnaona, macho ya kuona.

Ati nini? Nilisema, "Hapo umesimama huo ulimwengu mkuu wa kikanisa kule nje, ulio katika wakati huu wa kisayansi, kwamba haiwezekani." Bali nilisema, "Mungu . . . " Katika Nuru hiyo, kabla haijapata kupigwa, ila mara moja; kamwe haijapata kupigwa. Ilikuwa ni huko chini mtoni; hawakuipiga picha. Mnaona? Nikasema, "Yeye aliniambia itatendeka; Yeye angetoa mwito na ungesambaa katika mataifa."

214 Na hata kwa Daktari Davis, alisema, "Wewe, ukiwa na elimu ya msingi, uliingia katika darasa la saba, ati utakuwa ukiwaombea wafalme na watawala, na utaanzisha uamsho ambao utaenea katika mataifa?"

Nikasema, "Hilo ndilo Yeye alisema."

215 Na limetendeka. Mnaona? Mnaona, limetendeka. Jambo ndilo hilo, kwamba, Yeye hahitaji ufasiri wowote. Amelifasiri. Mnaona, Yeye amelifanya tayari, hilo linajifasiri lenyewe, mnaona, kuwaita Wateule Wake, mnaona, kutoka—kutoka kwenye kila tabaka la maisha. Sasa limedhihihirishwa.

216 Nilisema ya kwamba Daudi alisimama kule nje, maskini jamaa mdogo sana, aliyekonda, mgongo umejikunyata sana, kombeo mkononi mwake. Na, mbona, Sauli alimwangalia, yule kiongozi wa shirika la wahudumu, kasema, "Mbona, wewe, hata hujafunzwa!" Akasema, "Hebu nione kama ninaweza kukupa Ph.D. ama kitu fulani." Akamvika vazi hili la kujihami, likaninii . . . Akakuta kwamba halikumfaa mtu wa Mungu.

217 Kasema, "Ondoa kitu hiki kwangu." Kasema, "Sijui chochote kuhusu hicho." Kasema, "Acha niende jinsi ninavyojua, kile nilichompiga simba nacho, kile nilichompiga dubu nacho." Kwa namna fulani alikuwa ni mtu anayependa maisha ya mwituni. Akasema, "Acha niende hivi."

218 Na maskini Goliathi huyu akasema, "Hivi mnamtuma mbwa atoke kupigana nami?" Kasema, "Nitakunyanyua kwa ncha ya mkuki wangu na kuning'iniza mzoga wako huko juu na kuwaacha ndege waule."

219 Daudi akasema, "Unanikabili kama Mfilisti, na vazi la kujihami na mkuki, nami nitakukabili katika Jina la Bwana Mungu wa Israeli." Mtazame nabii huyo, Daudi, alisema, "Leo nitakikata kichwa chako kutoka begani mwako." Amina!

Loo, jamani! Yeye alijua alichokuwa nacho, yule aliyekuwa amemwamini, na alishawishika kabisa Yeye aliweza kukilinda kile alichokiweka amana Kwake. Unaona? Kwa hiyo jambo hilo lilitukia hata hivyo.

220 Ule msemo wa kale, "Siku za miujiza zimepita," kuta zimebomolewa! Yehova angali anasimama akionekana dhahiri kabisa, akilidhihirisha Neno Lake, Yule aliyefunuliwa. Hiyo ni kweli. Angalia.

221 Kanisa la Kimataifa pia limepofushwa kutokana na utaji, baada ya huo kupasuliwa na kumwonyesha Mungu, lile pazia la kikanisa. Jinsi gani? Kwa kutia Neno utaji katika mwili wa mwanadamu tena. Hilo hasa ndilo Israeli walishindwa kuona. Kama ingalikuwa ni Malaika fulani ama kitu fulani, Israeli wangaliamini jambo hilo. Lakini kwa kuwa haingeweza kuwa ni Malaika, ilibidi iwe ni mwanadamu. Amina!

Mungu hawezi kulivunja Neno Lake. Katika siku za mwisho haina budi kuwa ni jambo lile lile tena. Mnaona? Ni kitu gani kilichowapofusha Israeli? Yule Mtu. "Wewe ni Mwanadamu unayejifanya Mungu." Hilo ndilo walilomwulia, na, leo hii, kwa sababu Ujumbe umekuja kupitia kwa mwanadamu wala si Malaika. Mnaona? Mungu hawezi kubadilisha njia Yake, kubadilisha Neno Lake. Yeye alisema habadiliki. Mnaona? Angalia, aliahidi! Nao Mataifa wamepofushwa tu leo kama vile Israeli walivyopofushwa, kwa sababu (nini?) ule utaji. Mungu akitiwa utaji katika mwanadamu, aliwapofusha Israeli.

Angalia, imewahi kumpofusha mmoja. Mmoja, itampofusha; huyo mwingine, itamfunulia Kweli. Itayafumba macho ya baadhi, na kuyafumbua macho ya mwingine.

222 Angalia, Yesu alisimama na kusema, "Vema, jina lako ni—ni—ni Simoni, na jina la baba yako lilikuwa ni Yona."

Akasema, "Bwana Mungu!" Mnaona? Filipo . . .

Akasema, "Wewe ulijuaje?"

Akasema, "Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!"

Naye akasema, "Rabi, ulinitambua lini?"

223 Yeye akasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya ule mti, nilikuona."

224 Akasema, "Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli."

225 Vema, hao hapo wamesimama, wakasema, "Yeye ni Beelzebuli." Mnaona? Ilifanya nini? Ilifungua macho ya mmoja, ikampofusha mwingine. Makuhani walisema nini? "Mbona, Jamaa yule ni Beelzebuli!"

226 Maskini mwanamke huyo alisema, "Ninajua yuaja Masihi, aitwaye Aliyetiwa Mafuta. Unaona, Aliyetiwa Mafuta atakuja.

Hatujakuwa na manabii . . . Yamkini Wewe ni nabii. Lakini Aliyetiwa Mafuta atakuja. Tunamtazamia. Hizi ni siku za mwisho kwa ajili ya Mataifa . . . ama kwa ajili ya Wayahudi." Kasema, "Hii ndiyo siku ya mwisho." Mnaona, Msamaria na Myahudi pia walikuwa wakimtazamia Masihi. Mnaona? Kasema, "Huu ndio wakati wa kutokea Kwake. Tunajua, Yeye atakapokuja, atafanya mambo haya. Atatwambia mambo haya."

Yesu akasema, "Mimi Ndiye."

Macho yake yakafunguliwa; polisi, makuhani walipofushwa.

227 Hilo ndilo ambalo Injili hufanya daima. Inayafungua macho ya baadhi, inafunua Kweli kwa wengine, wakati ikiwapofusha wengine; ina maana maradufu. Wengine wanaweza kumchukua huyo Mwana na kumwangalia moja kwa moja, na kuwa vipofu; wengine wanaweza kumchukua na kutoka nje Naye. Ni tofauti.

228 Kama ilivyofanyika katika kila wakati, Uungu ukitiwa utaji katika mwili wa binadamu. Angalieni, Yeye alifanya hivyo. Manabii walikuwa ni Uungu, umetiwa utaji. Walikuwa ni Neno la Mungu (hiyo ni kweli?) lililotiwa utaji katika mwili wa binadamu. Kwa hiyo wala hawakumwona Musa wetu, mnaona, Yesu.

229 Tazameni kilichowekwa utaji nyuma ya zile ngozi za kale za pomboo katika lile hekalu la kale, kilikuwa ni Neno, kilikuwa ni Neno likidhihirishwa katika mbao za mawe.

230 Sasa, nitajaribu kuondoka katika karibu dakika ishirini sasa, nikiweza, tuseme saa tano na nusu. Tazameni, kama mkiangalia, nimefungua kurasa fulani hapa, mnaona, nisije nikapata . . . nisije kukatiza ninii . . . kulifanya refu sana. Ninajua mna joto, mmechoka.

231 Nyuma ya lile hekalu la kale, katika lile pazia, ni kitu gani kilichokuwa kule nyuma? Yehova alikuwa ni nani? Ni kitu gani kilichofichwa kule nyuma? Lile pazia lilikuwa likificha nini? Loo, haleluya! Lile pazia lilikuwa likificha nini? Lilikuwa likificha Neno. Lile pazia, ngozi za kale za pomboo, zilikuwa zinaficha, zinaficha Neno kwa macho yao, ya kawaida. Kule nyuma, pia, kulikuwako na mkate wa wonyesho. Nyuma kule, pia, kulikuwako na Utukufu wa Shekina. Lakini yote yalikuwa yamefichwa kwao. Yote yalikuwa yamefichwa. Utukufu wote wa Mungu ulikuwa moja kwa moja nyuma ya ile ngozi ya kale ya pomboo, hiyo ni kweli, yote yamefichwa kwa macho ya kawaida.

232 Ndivyo ilivyo leo, pia. Linaitwa "kundi la watakatifu wanaojifingirisha, walokole," bali wao hawajui ni kitu gani kilichofichwa huko nyuma. Hicho ndicho hawajui. Unaona?

233 Ndipo wakati Mungu, katika rehema, alipolipasua lile pazia kwa ajili yao wapate kuona, walikuwa wamefungwa sana katika

mapokeo yao wao . . . ilikuwa bado imefichwa kwao, hata katika siku hii.

234 Ndivyo ilivyo sasa! Ule Utukufu, zile Nguvu za Roho Mtakatifu, ule Utukufu wa Shekina ambao humshukia mwaminio, sasa ninamaanisha mwaminio halisi, unaofanya kazi za Mungu na imani kuingia ndani yake, apate kuliamini Neno la Mungu, ambalo limefichwa kabisa kwa macho yao. Wao wanasema, "Hayo mambo yamepita." Mnaona, wao wangali wanaishi nyuma ya pazia.

Hamko nyuma ya pazia hilo tena, enyi Watoto wadogo. Mungu anaonekana wazi kabisa kwenu.

235 Hivi majuzi, Ndugu Fred Sothmann, Ndugu Tom Simpson . . . Sijui kama aliwahi kufika hapa ama hakufika. Wengi wetu tulikuwa huko kwenye kanisa la Kibaptisti, na mhudumu akasema jambo fulani lililosikika zuri sana. Sote tukasema, "Amina!" Kila mtu kanisani aliinyosha shingo yake na kuangalia nyuma. Mnaona? Mnaona? Tulipata kombo lililotoka nyuma ya Shekina pale, mnajua, na kwa namna fulani tulifurahia kulipata. Tulisema, kwa maneno mengine, "Asante, Bwana!" Unaona? Na, walipofanya hivyo, jamaa hawa walikuwa wametiwa utaji sana walilicheka tu. Hawakujua kuwa Hilo lote lilihusu nini. Mnaona? Wangali wametiwa utaji. Kwa hiyo, kuna wengine walio ndani na wengine walio nje. Na kwa hiyo . . . Lakini Mungu anaonekana waziwazi kabisa mbele zetu, amefichwa. Vivyo hivyo sasa!

236 Ndipo wakati Mungu, katika rehema Zake, alipolipasua pazia, alionekana waziwazi kabisa. Lakini, wao walikuwa wamefungwa sana katika mapokeo yao, Yeye alikuwa angali amefichwa kwao.

Vivyo hivyo sasa! Utukufu huo wote, umefichwa, umefichwa kwa ajili yetu katika Kristo, lile Neno, ambaye Ndiye Hekalu letu.

237 Loo, sasa, itanilazimu kuchimba ndani katika jambo hili kidogo. Samahani kwa mihemko yangu asubuhi ya leo, lakini, loo, nime—nimetamani kulitoa hili kwa muda mrefu sana, mimi . . . linajifunga tu ndani yangu. Mnaona?

238 Angalia, Utukufu wote ulio ndani ya Mungu umo katika Neno. Baraka zote zilizo katika Mungu zimo katika Neno. Zimefichwa, kwa asiyeamini, kwa mapokeo. Mnaona ninalomaanisha? Bali yote yamo katika Kristo. Yote aliyokuwa Mungu, *alijimimina* Mwenyewe, "kenos," na akaingia katika Kristo; na sisi, katika Kristo, tuko nyuma ya pazia.

239 "Vema, mimi nimo ndani ya Kristo," unasema. Halafu unaamini kuna Miungu watatu? Unabatiza katika jina la "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu"? Unaamini katika mapokeo haya yote na kadhalika unayoamini, ya wazee? La, bado ungali uko

nyuma ya pazia. Unaona? Ingia ndani ya pazia. Yeye, Kristo, ni Neno.

240 "Vipi? Mimi siamini katika uponyaji wa Kiungu. Siamini katika miujiza hii na mambo kama Hayo."

241 Vema, unaona, wewe—wewe humo ndani, ndani ya pazia. Hujui lolote juu Yake. Unaona? Kristo ni Neno! Na tunapokuwa ndani ya Neno, tuko ndani ya Kristo. Na ninawezaje kuwa katika Kristo, nikimkana Kristo? Yeye ndiye aliyesema, "Hakuna hata neno moja litakaloongezwa wala kuondolewa." Unawezaje kuondoa na kuongeza kwalo, basi? Unaona, inakuonyesha ni utaji gani umekutia utaji. Unaona?

242 Sisi ndani Yake! Basi sisi, tukiwa ndani Yake, tungali tumetiwa utaji kwa wanadini na maprofesa wa ulimwengu huu. Mnaona, Utukufu wetu tulio nao na tunaufurahia, tungali tumetiwa utaji kwa hao walio nje. Wanafikiri sisi ni "wendawazimu, nati," tena. Mnaona? Mnaona? Hiyo ni kweli. Bali sisi tulio humu ndani, katika Kristo, tuliobatizwa katika Yeye, (Wakorintho wa Kwanza 12), katika Yeye, sisi ni washiriki wa Utukufu huu. Mnaona? Bali sio nje; ungali unaangalia ndani, ukilikana. Unaona?

243 Kwa hiyo sasa tumealikwa ndani Yake, tupate kuwa washiriki wa yote aliyo Yeye. Tumealikwa ndani Yake, ambalo limefichwa wasioamini, kwa pazia la mwili wa binadamu. Unaona? Wanaujua Utukufu huo, wanausoma, umo katika Neno hapa, "Utukufu wa Mungu" na mambo kama hayo, ni neno tu kwao. Kwetu sisi, ni dhihirisho! Mnaona? Sio neno tena; ni uhalisi! Amina!

244 Mungu alisema, "Na iwe nuru," hilo lilikuwa ni neno. Lakini sasa kuna nuru. Si neno; ni nuru. Mnaona ninachomaanisha?

245 Sasa si Neno tu lililoandikwa kwetu, ni kitu halisi. Tuko ndani Yake. Sasa tunafurahia. Sasa tunamwona Yeye. Sasa tunamwona, lile Neno, akijidhihirisha Mwenyewe. Limefichwa, huko nje, kwa sababu (kwa nini?) Limetiwa utaji katika mwili wa binadamu. Mnaona?

246 Loo, wao wanasema, "Kundi hilo la watu, walienda shule wapi? Wana—wana elimu gani? Wapi, walitoka wa—wapi? Wao ni wa kundi li—li—lipi?" Mnaona? A-ha! Mnaona, hawalipati.

247 Mtu mmoja alimwambia mwingine, hivi majuzi, kasema, "Inakubidi uwe mfuasi wa dhehebu fulani upate kuwa Mkristo."

248 Akasema, "Mimi ni Mkristo; mimi si mfuasi wa lolote la hayo." A-ha. Kasema, "Mungu aliniondolea kansa hii," kasema, "sasa wasemaje juu ya hilo?" Ilikuwa ni daktari. Akasema, "Nionyeshe madhehebu yanayofanya jambo hilo." Unaona? Vema. Unaona? Lingali limetiwa utaji.

249 Sisi tuko ndani ya Kristo. Sasa, kama vile katika wakati huo, waaminio wote wa kweli wanamwona, Neno la ahadi

la siku hizi, likidhihirishwa wazi. Hilo ni neno kubwa kama mnaweza kulipata. Mnaona? Mnaona? Waaminio wote wa kweli, walio katika Neno, wanamwona Mungu waziwazi. Lile pazia limepasuliwa, na Mungu anasimama waziwazi mbele zako, amedhihirishwa. Mnaona? Mungu, akidhihirishwa, wazi.

250 Ili kufanya jambo hili, utaji wetu wa kale wa kimadhehebu na wa mapokeo hauna budi kupasuliwa tena. Kusudi upate kuona kwamba Hilo ni kitu gani, inakubidi kutoka katikati ya upuuzi huo. Unaona? Kamwe hutaweza kutoka; wataendelea kuuvuta utaji huo mbele zako, kila wakati, "Loo, Hilo ni bure." Lakini hili hapa limeandikwa, na hili hapa limedhihirishwa, unaona. Mnaona?

251 Sasa, vipi kama jamaa fulani anakataa kuliona jua, aseme, "Loo, hapo, ninajua Mungu alisema, 'Iwe nuru,' lakini hakuna kitu kama hicho. Ninashuka niende kwenye chumba cha chini. Mimi—mimi ni—nakataa kuliona"? Jamaa huyo ana wazimu. Ana kasoro fulani.

252 Kuna kasoro kwa mwanamume ama mwanamke, anayeweza kuona ahadi ya Mungu na, kuiona ikidhihirishwa, halafu akatae kuiamini kwa sababu dhehebu linashusha pazia. Unaona, ametiwa utaji!

253 Kusudi jambo hili lifanyike, mapazia yetu ya mapokeo ya kimadhehebu hayana budi kupasuliwa, na Roho wa Mungu wa Moto na Upanga, ambao ni Neno Lake. Daima Neno Lake ni Upanga Wake. Mnaona? Naye aliuchukua upanga Wake siku hiyo, uliojaa Moto, na kulipasua lile pazia toka juu hata chini. Yeye hufanya jambo lile lile kwa Upanga ule ule siku hizi! Si "kanuni yangu ya imani, kitabu changu cha kanuni za imani, ninii yangu—katekismo yangu." Bali Upanga wa Bwana, unaona, hulipasua pazia mpaka chini, nawe unamwona Mungu amesimama akionekana dhahiri, akidhihirishwa katika Neno Lake. Ni tamasha lenye utukufu jinsi gani kuangalia! Unaona? Vema. Roho Mtakatifu wa Mungu na Moto, Upanga Wake, hulipasua. Neno hulipasua pazia la kimadhehebu.

254 Vema, kama ulisema tu, "Neno," nalo Neno halitendi kazi? Upanga ungefaa nini hapa, na kusema, "Hauwezi kupasua"? Unasema, "A-ha," wala hautapasua?

255 Lakini unapouweka huo Upanga wa Mungu pale na kuuangalia ukipasua, una—unashikwa na mkono ulioteuliwa na uliotumwa kufanya hivyo. Unaona, hulipasua vipande viwili, na Huyo hapo. Hapo linamwonyesha Mungu waziwazi, yule Yehova mkuu. Hilo ni Neno Lake lililodhihirishwa, ile sehemu iliyoahidiwa kwa ajili ya siku hiyo. Mnalipata? Mnaona? Wakati huo Upanga, ahadi ya siku hizi, katika siku hii, kile kinachopaswa kutukia, na Mungu anachukua Upanga Wake na kulipasua pazia la kimadhehebu na kulivuta, na kujidhihirisha Mwenyewe na kuonyesha ya kwamba Yeye yupo hapo, angali ni

Nguzo ile ile ya Moto. Angalia, hilo ni Neno lililodhihirishwa kwa ajili ya ahadi za leo.

256 Tunaona jambo Hilo kama vile Petro wakati aliposema, "Bwana, twende kwa nani, baada ya kuona Haya?" Tungeenda wapi? Tungejiunga na kanisa gani, wakati tumezaliwa katika Moja? Unaona? Ungewezaje . . . Ungeweza kujiunga na dhehebu gani baada ya kujua Kweli hizi, unaona, wakati hayo (kila moja) wanalikana? Kila moja lao! Sijampata mmoja atakayesema au kufanya kitu kwa ajili Yake. Kweli. Hiyo ni kweli.

257 Nilianza kwenye safari hizi hapa chini, ambako makanisa arobaini na mbili katika mahali pamoja yalikuwa mdhamini; nilipofika kule, sikuwa na hata moja. Kila moja lao lilisema, "Anaamini katika usalama wa Milele." Hilo linawaondosha wale washika sheria. Moja lilisema, "Anabatiza katika Jina la Yesu." Hilo linawaondosha hao wengine wote, unaona. Kwa hiyo, moja lilisema, "Anaamini katika uzao wa nyoka. Nyoka hana mbegu!" Hilo linaninii . . .

258 Biblia ilisema, "Nitaweka uadui kati ya Uzao wake na uzao wa nyoka." Unaona? Unaona hapo?

259 Hilo, lile—lile pazia, limeondolewa kwenye Neno. Unaona? Hiyo ni kweli. Limefunuliwa kwa watoto wachanga. Lime—limeinuliwa. Wanaliona. Nalo litakuwa, kama ilivyosemwa wakati mmoja . . . Hiyo ni kweli. Basi itakuwa, kama ilivyosemwa wakati mmoja, "Mnapoona," wakati utaji huu unapoondolewa kwenye Neno, mapokeo yanaondolewa kwenye Neno, kama vile Yesu alivyosema wakati mmoja, "mnaponiona Mimi, mnamwona Baba." Mnaona? Mungu na Neno Lake ni mmoja. Sasa mnaelewa? Neno linapodhihirishwa, ni Kitu gani? Mnaona?

260 Yesu alisema, "Yachunguzeni Maandiko, mnadhani mna U- . . . Mmemwamini Mungu, niaminini na Mimi pia. Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Bali kama ninazifanya hizo kazi, Mimi na Baba Yangu ni mmoja. Mnaponiona Mimi, mmemwona Baba."

261 Na mnapoliona Neno likidhihirishwa, mnamwona Baba, Mungu, kwa kuwa Neno ni Baba. Neno ni Mungu. Nalo Neno, likidhihirishwa, ni Mungu Mwenyewe akichukua Neno Lake Mwenyewe na kulidhihirisha miongoni mwa waaminio. Hakuna kitu kinachoweza kulifanya liishi ila waaminio, waaminio tu. Si . . . Halitaninii . . .

262 Unaweza kuchukua ngano na kuipanda katika ninii—katika ninii—udongo wa aina nyingine, kamwe haitaota. Lakini, ni nini, haina budi kuwa na mbolea fulani ardhini kuikuza ngano. Na kama hakuna—kama hakuninii . . . kama mbolea hiyo ardhini haija—haijaninii, ngano hiyo haijarutubishwa kwa mbolea hiyo, kamwe haitaota. Kwa hiyo haidhuru Neno linaanguka wapi, kama halianguki kwenye moyo ulio mzuri . . .

263 Yesu alisema hivyo. "Zingine zilianguka kando ya njia, kwenye udongo wa mawe, nao ndege wa angani wakaja wakaila." Na ndipo akasema, "Zingine zilianguka katika miiba na michongoma, ambazo zilichipuka na kusongwa mara moja," mapokeo, madhehebu, shughuli za dunia ziliisonga. Lakini akasema, "Zingine zilianguka juu ya udongo ulio mzuri na kuzaa mia," kasema, "huo ndio Ufalme wa Mungu."

Ni jambo lile lile, mnaona, wengine hawataamini kamwe.

264 Wengine wataamini kwa kitambo kidogo, kama wale wanafunzi. Walimfuata, wengi wao, wale sabini na wawili walimfuata kwa miaka kadhaa, wapate kujua; kama mwaka mmoja na nusu, ama miaka miwili; wapate tu kujua, mpaka watakapoweza kupata kitu fulani ndani Yake, baadhi... kama jinsi alivyokuwa na nguvu ya kufanya mambo haya, ama kama vile mguu wa sungura, namna fulani ya mchawi, kile angeweza kufanya kuleta mambo haya, jinsi alivyoweza kujua yaliyokuwa mioyoni mwa watu na yale waliyokuwa wakiwazia. Ndipo hatimaye wakaona kwamba Yeye alisema kuwa Yeye "alishuka kutoka Mbinguni," Yeye "alikuwa Ndiye Neno Mwenyewe." Na wakati walipolipata hivyo, hawakuweza kulivumilia. Wakasema, "Hakuna mtu anayeweza kufahamu jambo Hili." Ndipo wakaondoka wakamwacha. Hao ni wale walioanguka penye miiba.

265 Linarejesha kwa jambo lile lile, katika kila kusanyiko, una wanaojifanya waaminio, wasioamini, na waaminio. Imekuwa hivyo katika kila kusanyiko. Unawapata wakati wote. Baadhi yao wanajifanya kana kwamba ni waaminio, hao ndio walio wabaya kabisa. Na halafu wana wale ambao kweli ni wasioamini; yeye hatakusumbua, yeye ataondoka tu na kutikisa kichwa chake. Lakini wale ambao wanajifanya kuwa waaminio, wanasema ni waaminio, hao ndio, hao ndio aina inayokubidi kuangalia, ni hao wanaojifanya kuwa waaminio. Halafu kuna walio waaminio halisi. Unawaona hao watatu hapo?

266 Kulikuwako na wasioamini. Mara Yeye aliposema, "Muule Mwili wa Mwana wa Adamu," loo, jamani, hilo lilikuwa ndilo jambo lenyewe!

267 Hao wengine walikuwa wanaojifanya waaminio. Walibaki mpaka, kama vile Yuda alivyofanya, moja kwa moja hata mwisho.

268 Lakini basi waaminio wa kweli, hawakuweza kuelezea jambo Hilo, bali waliliamini, hata hivyo. Waliendelea moja kwa moja.

269 Lile pazia, mapokeo ya wasioamini, yakiondolewa, mnamwona Mungu. Wakati utaji wa mapokeo umeondolewa, unaweza kuona ya kwamba Mungu angali ni Mungu wa Neno Lake. Yeye angali anadumisha Neno Lake. Yeye ni ninii—Yeye ndiye Mungu, Mwandishi wa Neno Lake.

Hilo limefichwa nyuma ya pazia la ngozi, kwa wengine. Naam, hiyo ni kweli. Kwa wale wasioweza kwenda nyuma ya pazia, Yeye angali yuko nyuma ya mapazia ya ngozi.

270 Angalia. Basi, sisi, ndipo tunakuwa sehemu Yake, kwa kuwa wewe ni utaji unaomficha Yeye. Wewe ni sehemu Yake, mradi Kristo yumo ndani yako, kama vile Kristo alivyokuwa wa Mungu. Kwa kuwa Mungu alikuwa ndani Yake, ilimfanya Mungu. Na kwa kuwa Kristo yumo ndani yako, tumaini la Utukufu, unakuwa sehemu ya Kristo. "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Unaona? Unakuwa sehemu ya Kristo mradi tu Kristo amefichwa ndani yako. Ndipo jambo hilo limefichwa kwa asiyeamini, bali wewe unajua yumo ndani yako. Unakuwa hekalu la Kristo aliye nyuma ya pazia, ngozi. Ndipo sisi, kwa saba-. . .Nyuma, kwa sababu ya pazia hili, pazia tena katika mwili wa binadamu, linamficha Mungu (lile Neno) kutoka kwa asiyeamini.

271 Kama ilivyoandikwa, mnaona, "Zilizoandikwa, ninyi ni nyaraka zilizoandikwa," Biblia ilisema. Sasa, *waraka* ni nini? Ni "neno lililoandikwa." Nanyi ni "zilizoandikwa." Maneno mengine, ungelisoma namna hii, "Ninyi," Hilo lilisema, "ninyi ni nyaraka zilizoandikwa," ama, "ninyi ni Neno, ambalo limeandikwa, lililodhihirishwa," hakuna kitu kinachoweza kuongezewa Kwake. Huwezi kusema, "Mimi ni waraka ulioandikwa," na kuishi namna nyingine mbali na vile *Hii* imeandika tayari, [Ndugu Branham anapigapiga Biblia yake—Mh.] kwa maana hakuna kitu kinachoweza kuongezwa wala kuondolewa.

272 Kwa kuwa Daktari Lee Vayle anakiandika kitabu hiki maarufu sana, ninawatakeni mkione hivi punde. Ndugu Vayle yupo hapa, yupo hapa mahali fulani. Nilimwona huko nje. Sidhani anaweza kuingia. Lakini yeye anaandika kitabu kule, na—na ni cha kushangaza sana, cha Wakati wa Laodikia. Nami ninawatakeni. . .Kitatoka kwenye mtambo wa kupiga chapa hivi karibuni sana. Kwa hiyo, tunakipitia kwa mara ya mwisho sasa. Na alikuwa akiandika, na tulikuwa tukijadiliana juu Yake hapo ndani, mnaona, kuhusu. . .

273 Kila mtu daima amenijia, kasema, "Ndugu Branham, zile ngurumo saba ambazo ile sauti ilinguruma, na Yeye akasema, 'Usiziandike, unaona, bali kifunge,'" kasema, "hizo zitakuwa ni ngurumo saba zitakazofunuliwa katika siku za mwisho, unaona, ngurumo saba zitakazotuambia sisi?" Sasa, hilo si linasikika ni zuri sana? Unaona? Lakini angalia kile unachozungumzia unaposema hivyo.

Yeye alisema, "Angalia usiziandike." Unaona? Hizi ngurumo saba zinatoa sauti zao, mnaona, Naye akasema, "Usiandike jambo hilo, unaona, bali litatiwa muhuri katika Kitabu hata siku za mwisho."

274 Sasa mtu fulani amekuwa, wengi wamekuwa wakiniambia, nao wanathiolojia walisema, "Ndugu Branham, kama Bwana Mungu . . . " Kasema, "Kama—kama . . . Pamoja na ujuzi wako, ambao Bwana amekupa kwa ajili ya watu Wake," akisema hivi kwa unyenyekevu, kasema, "wewe ungestahili kuandika Bi—Biblia mwenyewe, Neno lako, kama Mungu amedhihirisha."

275 Nikasema "Huenda hilo likawa ni kweli." Unaona, yeye alikuwa akijaribu kunikamata. Unaona? Nikasema, "Lakini, unaona, nisingeweza kufanya hivyo."

Akasema, "Kwa nini usingeweza? Una sifa zote."

276 Nikasema, "Lakini, wewe angalia, neno moja haliwezi kuongezewa wala kutolewa." Unaona?

277 Naye akasema, "Vema, basi, hizo ngurumo saba, unaona," kasema, "je! hizo ngurumo saba zikinguruma, huo si utakuwa ni Ufunuo ukitolewa kwa mtu fulani?"

278 Nikasema, "La, bwana, itakuwa ni kuongeza Kwake ama kuondoa Kitu kutoka Kwake."

279 Yote yamefunuliwa Mle ndani, nayo ile Mihuri Saba ilifungua ufunuo kwamba Hizo zilikuwa ni nini. Hivyo ndivyo zilivyokuwa. Mnaona, zingali katika Neno. Unaona, huwezi kutoka katika hilo Neno. Halitaliacha Neno. Na Roho wa Mungu kamwe hataliacha hilo Neno. Atakaa moja kwa moja na Neno; likiwapofusha wengine, na kuyafumbua macho ya wengine. Daima litafanya jambo hilo.

280 "Ninyi ni nyaraka zilizoandikwa, zinazosomwa na watu wote." Ama, ninyi ni . . . Ninalitafsiri Hilo, kuligeuza upande huu, unaona, kuligeuza tu, "Ninyi ni nyaraka ambazo zimeandikwa," maana hamwezi kuongeza lolote Kwake, "zinazosomwa na watu wote; Neno la Mungu lililodhihirishwa," kwa maneno mengine.

Na Petro na Yohana, kuonyesha jambo hilo, walipoenda huko juu, waliona walikuwa ni watu wasio na elimu na wasio na maarifa, hawakuwa na elimu, bali wao walitambua walikuwa pamoja na Yesu. Unaona? Walikuwa hawana elimu wala maarifa, bali walikuwa nyaraka zilizoandikwa, mnaona, wakasoma ya kwamba walikuwa pamoja na Yesu. Maana, Yesu alikuwa akijidhihirisha Mwenyewe kupitia kwao, Kristo ametiwa utaji katika miili yao; akidhihirishwa, akifanywa hai.

281 Kama vile alivyokuwa katika Musa. Wakati Neno lilipokuwa ndani ya Musa, yeye alikuwa ni Mungu katika mwili. Wakati lilipokuwa katika Yesu, lilikuwa ni Mungu katika mwili. Mnaona? Jambo pekee alilofanya lilikuwa ni kubadilisha kinyago Chake, si Neno Lake, si tabia Yake. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye alibadilisha tu umbo Lake. Alibadilika kutoka kwa Nuhu akawa Musa; alibadilika kutoka kwa Musa akawa Daudi; kutoka kwa Daudi, Yusufu; na kuendelea mpaka

akafikia kwenye utimilifu wa Mungu kwa jinsi ya mwili. Mnaona?

282 Bado ni Mungu yeye yule! Amina. Amina. Ninatumaini hilo linaingia. Mnaona? Ni Mungu yeye yule, bali Yeye anachukua tu pazia jingine. Mnaona, Yeye huvaa utaji mwingine.

283 Yeye alifanya jambo hilo katika wale watengenezaji, akajifunika pazia, akajifunika pazia. Mpaka, hatimaye, ikaja kupitia wakati wa Kilutheri, kote kote katika wakati huo mwingine, ndipo hatimaye linafikia kwenye Ukamilifu. Kabla tu halijafikia, nabii anainuka tena. Kile jambo hilo linachofanya, linalionyesha mbele Neno kwa mfano, likionyesha hapa nyuma, likifunua yaliyokuwa yamefanywa, yale yaliyoachwa, kusudi Kanisa lisikose...lisikose ufahamu. Ndipo wakati hili linapofifia kabisa, basi, kama Yohana alivyosema, "Sina budi kupungua, Yeye hana budi kuzidi," ndipo yote katika yote yanaingia ndani Yake. Anadhihirishwa kikamilifu, kupitia Luther, Wesley, na wakati wa Pentekoste, na kuendelea moja kwa moja, moja kwa moja, Yeye amedhihirishwa kikamilifu, unaona, anashuka, ule udhihirisho tu, Mungu akijifunua: Mtazameni (Sasa, angalieni.) akidhihirishwa katika ahadi Zake kwa ajili ya siku *hii*, kama *wao* walivyofanya.

284 Sasa Musa alikuwa ni Neno siku hiyo, kwa maana alipewa Neno la siku hiyo; Musa. Yusufu alikuwa Neno katika siku zake, akimwonyesha Kristo kikamilifu. Unaona, kila mmoja wao alikuwa ni Neno.

285 Na Yesu alipokuja, Yeye alikuwa ni Neno katika utimilifu Wake, kwa sababu mpango wote wa ukombozi ulikaa ndani Yake. Mpango wote wa ukombozi haukuwa ndani ya Musa, haukuwa ndani ya Yusufu, haukuwa ndani ya Eliya. Unaona, wao walikuwa tu ni sehemu ya Neno, wakilinyooshea kidole. Unaona? Sasa angalieni, wekeni wazo lenu; hili hapa linakuja, kama nisemavyo. Mnaona, mpango wote haukuwa ndani yao. Walikuwa wakiunyooshea kidole.

286 Kwa hiyo, baada Yake, ule Utimilifu, hatuwezi kuelekeza kwa kitu kingine. Unaelekeza Kwake tena, lile Neno. [Ndugu Branham anaichukua Biblia yake—Mh.] *Hii* ndiyo Ufunuo mkamilifu; hakuna kitu kinachoweza kuongezewa wala kuondolewa Kwake. *Huo* hapo Ufunuo mkamilifu. Yote hayo, kivuli cha Yeye atakayekuja; lakini alipokuja, Yeye alikuwa ndiye Mkamilifu. Waebrania 1, "Mungu zamani alisema na baba zetu kwa njia ya manabii," Mungu alinena kupitia mapazia, manabii, "lakini katika siku hizi za mwisho kwa njia ya Mwanawe, Yesu Kristo." Haya basi. Akifunuliwa pale Kalvari, Mwana wa Mungu, amefunuliwa.

287 Angalia, "alifanywa hai." Na, leo hii, wakati Neno linapodhihirishwa katika vyombo vya kibinadamu, mapazia, ni Neno zima lililotimizwa katika siku hiyo, ambalo linamrudia

Mungu. Kwa kubatizwa katika Yeye, kulingana na Wakorintho wa Kwanza 12, tunakuwa tumetambulishwa pamoja Naye. Amina.

288 Nilisema nusu saa, lakini je! ninaweza kuendelea kidogo tu zaidi? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaona? Angalieni, siwezi kamwe kulikosa hili papa hapa ndani. Angalia, kutambulishwa pamoja na Yeye!

289 Sasa angalia. Ni wangapi wananchi wa Marekani waliopo hapa? Inueni mikono yenu. Vema, wewe ni mwananchi wa Marekani, basi unatambulishwa na taifa hili. Chochote taifa hili lilicho, huna budi kuwa. Hiyo ni kweli? Wewe ni utukufu wake wote na wewe ni aibu yake yote. Unatambulishwa pamoja nalo. Wewe ni Mmarekani, kwa hiyo unajivika Marekani. Haleluya!

290 Nilikuwa pamoja na George Washington wakati alipovuka Delaware. Ninatambulishwa pamoja naye. Hiyo ni kweli. Nilikuwa pamoja na Abraham Lincoln kwenye ile Hotuba ya Gettysburg. Nilikuwa nimesimama pale. Nilikuwa pamoja na wale askari pale Guam, ninyi vijana, wakati mlipoipandisha ile bendera. Nilikuwako kule. Mimi ni Mmarekani; nimetambulishwa nayo. Amina. Sasa, kusudi niwe Mmarekani, chochote kilicho aibu yake katika yale Mapinduzi, ninakibeba, maana mimi ni Mmarekani. Hiyo ni kweli.

291 Na kama Mkristo, ninatambulishwa na Yeye. Amina! Nilikuwa pamoja na Nuhu wakati alipoingia ndani ya safina. Nilikuwa pamoja na Musa wakati alipotoka huko Misri. Amina! Nilikuwa Eliya juu ya Mlima Kameli. Naam, bwana! Utukufu kwa Mungu! Nilikuwa pamoja naye wakati alipofanya hilo. Nilikuwa kweli pamoja Naye, nilijitambulisha mwenyewe katika mauti Yake pale Kalvari wakati nilipokufa kwa mambo ya ulimwengu, mwenyewe na mapokeo yote. Nilitambulishwa pamoja Naye. Nilitambulishwa na Yeye kwenye asubuhi ya Pasaka alipofufuka katika wafu. Nilitambulishwa pamoja na Yeye kwenye Siku ya Pentekoste, wakati Roho Mtakatifu aliposhuka kama upepo wenye nguvu ukienda kasi. Nilitambulishwa pamoja na Yeye. Yote aliyokuwa Yeye ndiyo niliyo, yote niliyo ndiyo aliyokuwa; amina, tukiwa tumekufa ndani Yake tunatambulishwa pamoja Naye. Kile Yeye alicho ndicho nilicho mimi. Amina!

292 Kile taifa hili lilicho ndicho nilicho mimi. Ninajivunia kuwa hivyo. Niko tayari kuchukua aibu yake. Niko tayari kuchukua dhihaka kuwa Mmarekani. Hiyo ni kweli. Na mimi ni hayo maradufu kwa Yesu Kristo! Yote aliyopata kuwa Yeye ndiyo niliyo mimi. Ninapenda kutambulishwa pamoja Naye.

293 Hao mitume, waliporudi, waliwazia . . . walidhihakiwa, na kuitwa chochote kile, walihesabu ilikuwa ni heshima kubwa kuchukua dhihaka ya Jina Lake.

294 Nina furaha leo kuwa mmoja wao, kutambulishwa na Neno, ambalo ni Kristo. Kutambulishwa na Yeye! Tukibatizwa ndani Yake, tunatambulishwa; tunatambulishwa katika mfano Wake, tunatambulishwa na Neno Lake, ambalo ni Yeye. Nikiwa ndani ya Kristo, mimi ni Neno Lake; kwa kuwa Yeye ni Neno, na kile alicho ndicho nilicho mimi. Amina! Mnalipata? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema.

295 Neno likidhihirishwa, ama kufunuliwa katika Ufunuo mle ndani, basi hilo linaniweka wapi? Kama Yeye ni huo Utukufu wa Shekina, mimi ni sehemu Yake. Amina! Loo! Amina! Hiyo ni kweli. Neno lenyewe likifunuliwa, linajifunua Lenyewe.

Wazia! Siri za Mungu zikijulishwa kwetu katika siku hii, kwa Mjumbe yule yule wa Mbinguni aliyetambulishwa kwao katika siku hizo; angalieni, Nguzo ile ile ya Moto iliyomtuma Musa; Nguzo ile ile ya Moto iliyokuwa juu ya Musa aliyeandika Biblia; Nguzo ile ile ya Moto ambayo Paulo alikutana nayo akienda zake Dameski.

296 Ndipo Paulo aliandika Agano Jipya. Kumbuka, Mathayo, Marko, Luka, na Yohana, wao waliandika tu kile walichoona; lakini Paulo alikuwa na Ufunuo. Aliutoa, kwa kuwa alikuwa amekutana na ile Nguzo ya Moto, mwenyewe. Na hebu wazieni, ile ile . . .

297 Hapo, Yusufu, wote waliandika kile kilichotukia, kila mmoja alichoandika huko nyuma katika siku hiyo. Bali wakati Musa alipotokea jukwaani, yeye alikuwa na Ufunuo. Alikuwa amekutana na Nguzo ya Moto, na Musa alifunuliwa yaliyotukia katika Mwanzo. Yeye aliandika vitabu vinne vya kwanza vya Biblia, Musa aliviandika. Hiyo ni kweli? Kwa kuwa yeye alikutana na Mungu katika umbo la Nguzo ya Moto, ametiwa utaji katika Nguzo ya Moto.

298 Wakati Paulo alipokutana Naye akienda zake . . . Wale wanafunzi waliandika tu yale waliyomwona akifanya, bali Musa alikuwa na Ufunuo; alishuka akaenda Misri kwa muda wa miaka mitatu na kusoma, na kuona kwamba yule Mungu wa Agano la Kale alikuwa Ndiye Yesu wa lile Jipya, Ufunuo! "Sikuliasi lile ono la Mbinguni." Hiyo ni kweli. Kweli!

299 Na wazieni jambo Hilo! Nguzo ile ile ya Moto iliyowashukia watu hao walioiandika Biblia, ndiyo Nguzo ile ile ya Moto hapa, leo, ikifasiri Biblia. Amina! Jinsi tunavyomshukuru kwa ajili ya jambo hilo! Ile ile! Ni faraja ya jinsi gani! Ni utambulisho wa jinsi gani! Ninafurahi sana kutambulishwa katika jambo hilo, sijui la kufanya! Afadhali nitambulishwe katika Hiyo kuliko Baptisti yote, Methodisti, Presbiteri, Lutheri, na hayo mengine yote. Kutambulishwa katika hilo Neno ambamo mnakaa huo Utukufu wa Shekina na Ufunuo!

300 Nguzo ya Moto ikijitokeza waziwazi miongoni mwetu, ikitambulisha ya kwamba Ujumbe ni wa kweli, kama Yeye

alivyofanya kwenye Mlima Sinai. Kumbuka, kabla Ujumbe wa kweli haujakuja, Musa alihubiri na akawaongoza kutoka Misri; lakini huko, kabla zile amri halisi kuwekwa (Mihuri iliingizwa), Mungu alishuka mbele ya watu na kuthibitisha ya kwamba Musa alikuwa ametumwa kutoka Kwake, (hiyo ni kweli) katika ile Nguzo ya Moto ambayo Musa alisema alikuwa ameiona katika kichaka na ikanena naye.

301 Loo, katika siku hizi za mwisho, kuona Nguzo ile ile ya Moto moja kwa moja miongoni mwetu, ikinena Neno lile lile; si hivyo tu, bali ikilifasiri kwa kulidhihirisha, na kulithibitisha, ni Kweli.

Kwa hiyo, watu hawana njia moja ya kutokuamini, isipokuwa wawe wanataka kufanya makusudi. Na, basi, "Yeye anayetenda dhambi makusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile Kweli, hakuna tena dhabihu ya dhambi."

302 Tazameni, Nguzo ile ile ya Moto iliyotumwa kwa Musa na kwa Paulo, ambayo iliiandika Biblia, sasa imetumwa kuifunua. Neema ya Mungu, Mungu asiyebadilika, akitimiza zile ahadi za Mathayo 28, "Tazama, niko pamoja nanyi sikuzote"; akitimiza Yohana Mtakatifu 14:12, "Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi pia"; akitimiza Luka Mtakatifu 17:28-29, "Katika siku za mwisho Mwana wa Adamu atafunuliwa," mnaona, mnaona; Malaki 4, "Angalieni, ninawapelekeeni Eliya nabii, atakayeirejesha Imani ya watu irejee kwenye Neno la asili." Mnaona? Jinsi ambavyo hii . . . Mnaona? Loo, jamani!

303 Yeye alikufa, apate kujifunua Mwenyewe kwetu. Sasa hebu na tufe kwa nafsi zetu, tupate kumfunua Yeye kwa wengine. Hebu na tufe kwa mapokeo na kadhalika, tupate kumfunua kwa mwingine. Tufe kwa madhehebu, tupate kumfunua kwa wengine.

304 Angalia, lile hekalu la kale lilikuwa na Utukufu wa Shekina ndani yake, na ile Nuru ya Shekina juu ya Neno. Neno ni Mbegu; lilileta ule mkate wa wonyesho kwa waaminio pekee. Damu pia ilikuwa juu ya agano; nayo Damu ni maji, maji ambayo huipa punje uzima, ngano, mbegu, ambayo ni Neno.

305 Kama vile Yesu alivyosema, "Kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka wa shaba," na kisha tena Yeye akasema. "Mungu aliupenda ulimwengu akamtoa Mwanawe pekee; kila amwaminiye asiangamie." Musa aliupiga ule mwamba jangwani, apate kuwaokoa watu wanaoangamia, ama kuyaleta maji. Mungu alimpiga Yesu, apate kutoa Roho Kwake, kwa ajili ya watu waliokuwa wakiangamia. Damu ilitoka Kwake, ambayo ni, "Maji ya kuosha kwa Neno." Ambayo, maji huleta Uhai kwa Mbegu. Nayo ilileta Utukufu wa Shekina; ukaangaza juu ya Neno, ambalo lilileta mkate wa wonyesho. Nao huo mkate wa wonyesho ulikuwa tu ni kwa ajili ya watu waliochaguliwa. A-ha. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

306 Sasa kuvunja kuingia katika lile pazia, kupitia lile pazia, kuingia katika Uwepo Wake, ambapo Neno lipo (sio kanuni ya imani), Neno; mle ndani ukiona ule Utukufu wa Shekina, Shekina, zile Nguvu, Roho Mtakatifu akiliangazia Neno, akileta ile ahadi, inaonyesha wewe uko nyuma ya pazia. Amina!

> Nimepita mapazia yaliyopasuliwa ambapo Utukufu haukomi, (Loo!)
> Haleluya, haleluya; ninaishi katika Uwepo wa Mfalme.
> Nimepita mapazia yaliyopasuliwa ambapo Utukufu haukomi,
> Ninaishi katika Uwepo wa Mfalme.

307 Ile ngozi ya kale ya pomboo, madhehebu, imepasuliwa. Nimepenya hiyo, nikaingia katika Utukufu wa Shekina, nami ninaliona Neno. Ninaona ile Nguzo ya Moto ikitenda kazi. Ninaona Neno likidhihirishwa. Yale aliyosema angeyafanya katika siku hizi za mwisho, ninaliona likikua. Ninaona watoto wakila huo Mkate wa Shekina unaotoka kwenye kule kuiva kwa hilo Neno, ambao wanaliamini. Amina! Ni saa nzuri ya jinsi gani tunayoishi! Mnaona, ile Shekina ilikuwa juu ya Neno; na kule chini kulikuwako na ule Mkate. Na hapo ilikuwapo ile Damu, imenyunyizwa, ambayo inaipa maji. Roho hulipa Neno Uhai. Na ninii . . .

Ni wangapi walisoma, waliisikia ile kanda juu ya *Lile Shtaka*? Naam. Wengi wenu mmeisikia. Mnaona pale, inahitaji . . .

Hilo Neno halina budi kukua. Kusudi likue, halina budi kuwa katika udongo mzuri. Mnaona? Na Mungu anapoweka ahadi, nayo inaugusa huo moyo, haiwezi kushindwa.

308 Nuhu alingojea miaka mia moja na ishirini. Ibrahimu alingojea miaka ishirini na mitano, juu ya yule mtoto. Mungu alisema hivyo, na hilo lilitosha. Unaona? Ni kitu gani? Neno lilikuwa hapo likitiwa maji na imani, wakiliamini, likaleta matokeo. Lilileta mwana; lilileta mvua; lilileta gharika; lilileta bikira ambaye alichukua mimba.

309 Nabii alisema, "Bikira atachukua mimba." Hapana shaka ila kwamba kila msichana mdogo alitoka akaenda akaweka tayari nguo zake za mtoto mchanga. Vema, huyu nabii Isaya alikuwa ni nabii aliyetambulishwa, aliyethibitishwa na Mungu. Ndipo Bwana akasema, "Bikira atachukua mimba. Nitawapa ishara ya kimbinguni, ishara kuu; bikira atachukua mimba."

310 Hapo, hao watu wote, hao waaminio, kama tu ninyi nyote. Nao walimsikia huyo nabii akisema jambo hilo, kila msichana mdogo . . . Kila mtu alisema, "Huyo atakuwa ni binti yangu. Naam, bwana." Kila mtu alitoka akaenda kununua vijiatu na nguo ya madoadoa na kila kitu, wakijiandaa, kwa kuwa walijua atamzaa. Kizazi hicho kikapita, nao wakafikiri, "Nabii

huyo aliyetambulishwa, aliyethibitishwa na Mungu, angewezaje kusema jambo lolote lisilo sahihi? Lazima iwe hivyo!"

311 Ilikuwa ni miaka mia nane baadaye, lakini akamzaa mtoto huyo. "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe."

312 "Na itakuwa katika siku za mwisho," asema Mungu. Mnaona, sisi hapa, Nu—Nuru juu ya Neno. Kama vile nuru ya jua huibadilisha mbegu kutoka utukufu hadi utukufu, sisi pia tulifanyika—tunakuwa zaidi kama Yeye tunapoishi katika Uwepo Wake; kama Yeye, tukibadilishwa kuwa katika sura Yake yenye baraka tunapotembea pamoja Naye.

313 Angalia kile jua hufanya. Ukipanda mbegu, ni kitu gani kinachotukia? Mbegu hiyo huoza. Ndani ya mbegu hiyo mna uzima. Uzima hutokea na kuchipusha shina. Sasa, hilo halionekani kama ile ya kwanza.

Kuna Luther. Ilikuwa ni shina. Vema.

Hilo shina liliendelea na, muda si muda wajua, ilichupusha kishada. Unaona, huo ulikuwa ni uamsho wa Wesley; haukuwa kama huo mwingine.

Ndipo ukaja uamsho wa Kipentekoste, mnaona, ukaleta ubatizo wa Roho Mtakatifu. Vema.

Ni kitu gani kilichotukia? Tunapata kuvu kwenye sikio. Unaanza kuonekana ni mbaya. Kitu *hiki*, kitu *kile*, hakionekani kama ni Neno. Hakilingani na Hilo lingine. Si kama Punje asilia iliyopandwa.

314 Lakini Mungu angali yupo kulifanya hilo—hilo vivyo hivyo. Angalia, linafanya nini? Hatimaye linarudi kwenye Mbegu ya asili tena. Wakati Yeye alipokuja katika mfano wa Martin Luther; wakati alipokuja katika mfano wa John Wesley; wakati alipokuja katika mfano wa Pentekoste; Yeye anatarajiwa kujifunua Mwenyewe tena kama Mbegu ile ile iliyopandwa, Mwana wa Adamu. Yeye alijifunua kama Mwana wa Mungu, kupitia kwenye wakati wa shina na kadhalika, bali katika wakati huu wa mwisho atajifunua Mwenyewe kama Mwana wa Adamu tena. Mnalipata? [Kusanyikio linasema, "Amina."—Mh.] Vema, kama vile hapo mwanzo, imefinyangwa!

315 Na hilo shina linakua vipi? Linakua wakati wote. Shina hilo dogo hukua, lingali si kama punje ya asili. Wala ujumbe wa Luther; la, moja kwa moja zikaja ju—jumbe hizo zingine, Finney, Sankey, Knox, Calvin, na kuendelea moja kwa moja, hakuna hata mmoja wao. Zilikuwa bado ni ujumbe lakini, jambo lilikuwa kwamba, hawakupata Ufunuo Wake mzima kwa kuwa wakati haukuwa umetimia. Huwezi kutia suke kwenye mahindi kabla wakati wake wa kuja haujatimia. Unaona? Na halafu, hatimaye, inarudi tena ile Mbegu asili iliyoingia ardhini.

316 Tazama Mungu hufuata maumbile kikamilifu. Unaona, Yeye alizaliwa mwana-kondoo, hiyo ndiyo sababu alizaliwa nje katika hori. Wana-kondoo hawazaliwi vitandani. Mnaona, Yeye *aliongozwa* akapelekwa Kalvari. Mwana-kondoo, kondoo huongozwa. Hiyo ni kweli. Mbuzi huwaongoza machinjioni, mnajua jambo hilo, machinjioni. Mbuzi huwaongoza, bali hawana budi kuongozwa. A-ha! Hiyo ni kweli. Kwa hiyo Yeye aliongozwa machinjioni, mnaona, kwa sababu alikuwa ni Mwana-Kondoo.

317 Kila kitu kilimtambulisha katika maumbile. Hiyo ndiyo sababu alizaliwa Marchi ama Aprili, sio Desemba; asingeweza Desemba, kuna futi ishirini za theluji kule wakati huo wa mwaka. Sio mungu-jua yeyote, bali Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu. Mnaona? Mungu-jua wa Kirumi tarehe ishirini na tano Desemba, wakati jua linapopitia mahali pake mle ndani nao walikuwa na sarakasi za Kirumi, na kuitwa siku ya kuzaliwa kwa mungu-jua, nao wanaifanya kuwa ni ya Mwana wa Mungu. La, la. Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu. Siku ya kuzaliwa Kwake ilikuwa inaendana pamoja na maumbile mengine. Kweli kabisa.

Sasa angalia tena sasa tunapoendelea, tuna muda mfupi uliosalia.

318 Sasa kwa walio wakamilifu. Baada ya shina kuumbika; baada ya kishada kuumbika; baada ya punje kuja kwenye gunzi; basi haina budi kufikia ukamilifu wake, inarudi kwenye punje ya kawaida tena.

Pia, kumbukeni, punje haina budi kurutubishwa. Mnaona? Isiporutubishwa, haitaishi. Mnaona? Hakuna mmoja wa hao waliokuwa nje ya hizo jumbe atakayewahi kupata Uzima. Haina budi kurutubishwa. Lakini, kumbuka, Uzima ule ule uliokuwa katika shina umo katika punje. Unajiivisha tu ukirudi moja kwa moja, mnaona. Yeye alijifunua Mwenyewe, (nini?) Mwana wa Adamu, ile punje iliyoingia ardhini. Mnaupata Ujumbe huo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Wayunani walimwambia, "Tungetaka kumwona Yesu."

319 Yeye akasema, "Punje ya ngano isipoanguka ardhini." Mnaona? Vema.

320 Sasa Yeye alijifunua Mwenyewe vipi baada ya hapo? Katika umbo tofauti; shina na kishada, na kadhalika, na majani yote na kila kitu. Yeye alijifunua mwenyewe wakati huo, (kitu gani?) Roho yule yule, bali katika umbo tofauti. Mnaona? Lakini mwisho wa hindi hilo ni nini? Linarudi likawa ile mbegu ya asili tena. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

321 Na huduma Yake inakuja, kutoka kwenye yale matengenezo, kurudi kwenye Neno la asili tena. Neno humjia nabii. Naye aliliahidi, katika Malaki 4, "Na kuirudisha Imani ya watu iirudie ile punje ya asili." Ile iliyoingia ardhini iko hapa vile

vile. Punje imepitia hapa. Ilichipuka kama Mwana wa Mungu, sasa inajifunua Yenyewe hapa kama Mwana wa Adamu, kisha inajifunua kama Mwana wa Daudi kwenye Kiti cha Enzi. Mnaona, hao Wana watatu, hakika kabisa. Loo, jamani, tena kama ile ya asili!

322 Sasa kwa huduma kamilifu Yake Mwenyewe; sio mtu fulani, sio dhehebu fulani, kama walivyotenda kote katika ule wakati pale, mnaona; bali Mwenyewe akidhihirishwa, anajidhihirisha Mwenyewe kwa ahadi, akiifanya Luka Mtakatifu 17:28, Malaki 4, na kadhalika, Waebrania 13:8, kweli tu kabisa. Katika wakati huo, inapaswa kuwa ni wakati gani? Wakati Uzao wa kifalme wa Ibrahimu unapomtazamia Mwana aliyeahidiwa. Na mifano yote haina budi kutimizwa. Na Mungu Mwenyewe alijitokeza katika umbo la mwanadamu, kwa uzao wa kawaida wa Ibrahimu, kabla ya yale maangamizi, na Yesu alisema litakuwa ni jambo lile lile kwa Uzao huu wa kifalme kabla ya kurudi kwa Mwana aliyeahidiwa.

323 Angalia ule utaji wa kale uliouficha ule Utukufu. Zile ngozi za kale za pomboo, hapakuwapo na uzuri wa kutamaniwa; wala na mwili Wake. Hiyo ndiyo sababu watu walisema, "Maskini Jamaa mdogo aliyejikunyata jinsi hiyo?" Labda mwenye umri wa miaka thelathini, na akiwa na mvi, na ndevu zake zina mvi, hakuonekana mzuri sana. Biblia ilisema, "Hakuna uzuri hata tumtamani." Hakuonekana kama Mfalme, ile ngozi ya kale ya pomboo, lakini, loo, kile kilichokuwa ndani!

324 Na maskini kundi dogo la "watakatifu wanaojifingirisha" limeketi pamoja katika jengo lenye joto kama hili, wanavyowaita, hakuna uzuri mwingi wa kutamaniwa, bali ni kile kilicho ndani! Nina hakika kimefichwa kwa mioyo mingi, unaona. Unaona? Vema.

325 Kwa nje ilikuwa si lolote, bali yote yalikuwa upande wa ndani. Ukiisha kuingia ndani Yake, basi unaliona. Unaingiaje ndani Yake; kupeana mikono, kujiunga? La. Kuzaliwa ndani Yake. Kufa, kutupilia mbali ngozi yako ya kale ya pomboo, unaona, utu wako wa kale, upate kuingia kwenye ule mpya. Mnaona? Iache ngozi ya kale ya pomboo.

326 Nuru ya Shekina haininii. . .Sikilizeni, enyi wahudumu! Wahudumu, ninawatakeni msikilize jambo Hili. Mara unapokuwa ndani. . .Sasa nitalichukua hili kwa urahisi sana, kusudi mwe na hakika ya kulipata. Mara ukiwa ndani ya lile pazia, chini ya Utukufu wa Shekina, Nuru ya Shekina hailichukui Neno la Mungu na kumfunua Kristo kwamba ni "mpiga ramli," la, kama vile madhehebu yanavyofanya siku hizi, "mawasiliano ya kiakili, mtakatifu anayejifingirisha, Beelzebuli." Utukufu wa Shekina haumfunui jinsi hiyo.

327 Lakini Utukufu wa Shekina huivisha ile Mbegu iliyoahidiwa kwa ajili ya wakati huo, ya Neno, ilimwonyesha kwamba Yeye

angali ni Yungiyungi la Bondeni. Huzaa hiyo Mbegu, Yungiyungi la Bondeni, Mkate wa Uzima, Alfa na Omega, yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye ni sehemu ya waaminio. Utukufu wa Shekina hufunua, kwa mwaminio, ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

328 Sio, "Zile siku, Yeye amepita, na Yeye alikufa na yote yamekwisha." Kwa hiyo rafiki, kama unaamini jambo hilo, kamwe hujaugusa Utukufu wa Shekina. Utukufu wa Shekina ungewezaje kumfunua katika nafsi tatu? Unaona? Utukufu wa Shekina ungewezaje kumfunua akibatizwa, watu, katika jina la "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," wakati hapajakuwapo na mtu katika Biblia aliyebatizwa hivyo? Utukufu wa Shekina ungewezaje kumwekea mpaka kama mtume, wakati Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Mnaona?

329 Utukufu wa Shekina humdhihirisha. Huleta Neno la ahadi, moja kwa moja kwako. Hiyo ndiyo sababu iliyomfanya kuutia utaji uso wa Musa, kwa sababu ndani yake mlikuwamo na Neno. Alimficha Yesu, kama Mtu mdogo mnyenyekevu, wasije wakamwona Yehova. Naye anajitia utaji siku hizi, katika vyombo vya udongo, pamoja na Shekina. Nje wanaonekana kana kwamba ni kundi la watakatifu wanaojifingirisha, ngozi za kale za pomboo, bali ndani yake zinaficha Utukufu wa Shekina.

Nalo linaivisha Mkate wa Wonyesho tunaousherehekea, na kuendesha magari kote nchini kwa sababu yake, kwa mamia ya maili, mnaona. Ni Chakula cha waaminio. Ni cha mwaminio pekee. Kumbukeni, ule Mkate wa Wonyesho ulikuwa tu ni wa mwaminio peke yake, mnaona, Mbegu ya Mkate wa Wonyesho. Angalia. Unafanya kitu gani? Huo Utukufu wa Shekina, juu ya Mkate wa Wonyesho, uliufanya usiharibike.

330 Kumbukeni, ile mana iliyotoka Mbinguni, ilikaa katika Utukufu wa Shekina, kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Nje, ilipata vifurukuta mikia ndani yake, kwa ghafla sana, ulioza. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

331 Nje ya Utukufu wa Shekina, "Siku za miujiza zimekwisha. Mnaona, yote ni ulokole." Lakini ndani . . .

332 Tazama, walipata mbegu za alizeti kutoka kwenye ghala moja huko Misri iliyowekwa mle katika siku za Yusufu, karibu, miaka elfu nne, iliyopita. Yusufu aliziweka kwenye ghala. Wakazipanda. Zikaishi. Kwa nini? Zilikuwa na uhai.

333 Utukufu huu wa Shekina ni nini siku hizi? Kuvunja ng'ambo ya pazia, kuona ni Mungu Gani anayesimama mbele zenu, kuona ni Mungu Gani anayesimama hapa mbele yetu, ile—ile Nguzo ya Moto. Yeye ametiwa utaji katika mwili wa binadamu. Lakini inafanya nini Shek'na, ilifanya nini? Ile Mbegu ya Mkate wa Wonyesho, Neno tunalopaswa kuishi kwalo katika siku hii, kwa ahadi hizi, ule Utukufu wa Shekina unaivisha Mkate huo wa Wonyesho, unalifanya litimie, unalifanya Mkate kwa mwaminio;

lililokuwa kwenye kurasa za Biblia, mwaka baada ya mwaka, Neno la wakati huu.

334 Kwa madhehebu, ni jiwe la kujikwaa. Kwa madhehebu, wao wanajikwaa Kwalo. Kote katika nyakati, Luther, Wesley, Martin Luther, na wote, Sankey, Finney, John Smith, Knox, wote walijikwaa Kwalo.

335 Lakini ni jambo gani litakalofanywa katika siku za mwisho? "*Kufunua*" ni kitu gani? "Kuleta!" Malaki 4 inafaa kufanya nini? Kuwarudisha watu kutoka kwenye kikwazo hicho, kuyavunja mapokeo, na kuufunua Mkate pamoja na Utukufu wa Shekina. Liangalieni likiiva na kuzaa kile hasa lilichosema lingezaa, loo, jamani, Mkate wa Wonyesho kwa ajili ya wakati huu. Kwa madhehebu, ni jiwe la kikwazo, "kundi la walokole." Bali, sisi tunaoamini!

336 Lakini sasa kama vile Ufunuo 10 imeahidi, "Siri zote za Mungu, ambazo zimefichwa katika kurasa kote katika miaka, zingeivishwa, zingeletwa katika wakati wa Ujumbe wa malaika wa saba." Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Ni kitu gani Yeye alisema, mwaka mmoja na miezi sita iliyopita, kuelekea miaka miwili sasa? "Nenda huko Tucson; uwe kaskazini mwa Tucson, mlipuko mkuu," na kile kingetukia, "Mihuri ingefunuliwa," Mihuri inayofunua mambo haya. Kurudi tu vile alivyosema.

Ni kitu gani? Inaonyesha haiwezi kuwa ni mwanadamu. Linaingia kikamilifu, limenyoka liwezavyo kuwa, kila wakati. Ni kitu gani? Ni mkono wa Mungu, unaona, mbele zetu. Na kwa sababu liko kwenye kundi dogo, limetiwa utaji katika mwili wa binadamu, limefichwa kwa ulimwengu wa nje. Yeye amefichwa kutoka kwa ulimwengu wa nje. Anajifunua Mwenyewe kwa watoto wachanga ambao watajifunza. Mnaona? Hiyo ni kweli.

337 Kila, mnaona, kila mfano katika Biblia, kila mfano wa Biblia, unadhihirishwa papa hapa mbele zetu. Mungu yeye yule, katika Nguzo ya Moto, ambaye aliiandika Biblia, katika Agano la Kale na Jipya pia, yupo papa hapa akilidhihirisha, akionyesha kile hasa kilichokuwa, akilifasiri moja kwa moja tena, na kuhakikisha ya kwamba ndilo tafsiri.

338 "Tunayo tafsiri!" Basi hebu na tuone likitendeka. Mnaona, jambo ndilo hilo, hebu na tulione likidhihirishwa.

339 Kudhihirishwa! Yesu alisema, "Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, msiniamini." Mnaona, halina budi kuthibitishwa.

340 Lakini sasa—sasa, si kuthibitishwa kama Yesu, wao walimfunga ki—kitambaa kichwani mwake na kumpiga kichwani, wakasema, "Kama Wewe ni Nabii, twambie ni nani aliyekupiga." "Na kama Wewe ni Mwana wa Mungu, geuza mikate hii." Mnaona, huyo ni ibilisi. "Kama wewe ni Mwana wa Mungu, shuka kwenye huo ms- . . . "

341 Ninamaanisha, ule Ufunuo ambao Yeye anapaswa kufanya, hivyo ndivyo ilivyo. Lakini sasa, wakati ufunuo 10 ikifunuliwa, siri za Mungu zinadhihihirishwa, zinajulikana, kama vile Kitabu cha Mihuri Saba kilivyoahidi.

Sasa hebu imani yako ndani Yake Yeye ambaye ni Neno . . . Maana, katika Ufunuo 10 inasema . . .

342 Ama, Ufunuo 19, hasa. Nilikuwa nimeliandika hapa, Ufunuo 10, kukiendea; bali sio 10, ni 19. Wakati Yeye atakapokuja, Yeye ataitwa, "Neno la Mungu," amempanda farasi mweupe, na wafuasi wa Mbinguni watakuwa nyuma Yake.

343 Pasueni pazia la kimadhehebu la elimu! Pasueni pazia la kimadhehebu la mapokeo! Pasueni mapazia hayo yanayomficha Yeye kutoka kwenu! Pasueni mapazia hayo ya kiburi, enyi wanawake. Ninyi ni—ninyi ni binti za Mfalme; tendeni kama mabinti, ishini kama mabinti. Pasueni kila pazia, haidhuru kile Ph.D. ama LL.D. inachosema. Kama ni kinyume na Biblia hiyo, pasua upite pazia hilo!

Kwa kuwa, tumevuka pazia lililopasuliwa. Tuko ng'ambo ya pili sasa, upande wa pili. Nanyi mtaona, kama tu mtafanya jambo hilo, mvunje hayo mapokeo ya kale na kadhalika, na mumjie Yeye, mtamwona Yeye amesimama, yule Mshindi Mkuu, Neno la ahadi kwa ajili ya wakati huu, lililodhihirishwa. Mtamwona Mungu Mwenye Nguvu amefunuliwa, mtamwona moja kwa moja miongoni mwetu hapa, amefunuliwa, Mungu Mwenye Nguvu, asiyeshindwa na mapokeo.

344 Walijaribu kumficha huko nyuma; walimficha, kwa miaka kadhaa, lakini wakati wa ile ahadi ukakaribia. Mungu akamwinua Musa wakati mmoja, naye akawaweka watoto huru kutokana na mambo hayo. Naye angali ni . . . Yeye hawezi kushindwa. "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita." Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

345 Wanasema, "Haiwezekani." Lakini ilitendeka. Ndipo, ilipotendeka, wao walisema, "Ni la ibilisi."

346 Lakini hilo halilibadilishi Neno la Mungu, hata kidogo. Lingali linabaki "Mungu," kwa mwaminio, "Mshindi Mwenye Nguvu; yeye yule jana, leo, na hata milele," kwa tabia Yake, kwa Neno Lake, Waebrania 13:8.

347 Ninafunga, katika kusema jambo hili, maana ni saa sita kasoro dakika tano, kusema jambo hili tu. Nina kama kurasa kumi, kumi na mbili zaidi. Nitazichukua wakati mwingine, labda usiku wa leo.

348 Angalia, angalia jambo hili. Kulikuwako na mnada wakati mmoja, na walikuwa na fidla ya kale. Mmeisikia mara nyingi. Fidla ya kale; na huyo dalali akasema, "Ninapewa ngapi kwake?" Huenda nisilipate hili vizuri sawasawa, kulingana na lile shairi. Imepita miaka mingi, mingi sana, ila nimeikumbuka.

Ndipo wakaiokota fidla hiyo ya kale, haikuonekana ni nzuri sana; ilionekana ni yenye thamani ndogo, kila kitu. Hata asingepata tenda kwake. Hatimaye, nafikiri alipata tenda ya dola moja, ama kitu kama hicho.

349 Na kulikuwako na mtu mmoja aliyekuwa amesimama pale ambaye hakuona ilipaswa kuuzwa kwa bei hiyo, kwa hiyo aliendа akaichukua. Akaiparuza kwa mikono yake, kisha akachukua uta na kuusugua kwa resini, kisha akapiga wimbo. Na wakati alipofanya hivyo, kila mtu akaanza kulia. Kamwe hawajapata kusikia muziki kama huo maishani mwao.

Ndipo yule dalali akasema, “Ninapewa ngapi?”

350 “Elfu mbili!” “Elfu tano!” “Elfu kumi!” Mnaona? Ilikuwa ni kitu gani? Mkono wa mtaalamu ulifunua kile kilichokuwa kimefichwa katika ala hiyo.

351 Vivyo hivyo sasa! Kile Kitabu cha Kale, ni chenye kuparuza, kimechekwa, kikachomwa, na kudhihakiwa. Lakini wakati umetimia ambapo wana mnada wa kimadhehebu, Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Wanaliuza haraka sana. Kuna mnada wa kimadhehebu unaokuja.

352 Lakini, kumbukeni, kuna kitu fulani katika Kitabu hicho cha Kale kilichoahidi ya kwamba kungekuwako na mkono uliokusudiwa tangu zamani, uliochaguliwa, ambao ungekichukua na kulifanya Neno la Kitabu hiki, kupitia moyo uliokusudiwa tangu zamani, kwenye jukumu ambalo ulikusudiwa, kufunua ahadi zilizomo ndani Yake. Huenda wakaonekana, loo, kama kundi la maskini watakatifu wanaojifingirisha, ama kitu kama hicho kinginecho; bali inahitaji tu mkono wa Bwana, Neno juu Yake, kulifunua hilo Neno, nao wanakuwa ni zaidi ya watakatifu wanaojifingirisha. Inakuwa hivyo kwa kila mmoja wetu, sivyo, enyi marafiki? Sio kundi la ulokole. Inategemea ule uta uko kwenye mkono wa nani.

Na tuombe.

353 Baba yetu wa Mbinguni, kwa imani leo ninamwona Bwana wa kile Kitabu cha Kale, ambacho wamekibadilisha na mapokeo. Walikibadilisha kwa madhehebu. Walijaribu kukifanyia biashara. Sasa wanakiuza kwa Ba—Baraza la mwanadamu Ulimwenguni, la makanisa, ukomunisti, ukafiri. Mnada unaendelea, Bwana.

354 Mungu, ingilia kati! Hakika, Wewe utafanya hivyo. Tutumie nabii huyo, Bwana, anayeuchukua huo uta, anayelichukua Neno hili na kuthibitisha ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Wengi, Bwana, watayauza maisha yao, watatupilia mbali mapokeo ya kale, watayapasua mapazia. Wanataka jambo Hilo, Bwana. Watatoa chochote kile, chochote kile, wape tu Yesu.

355 Bwana, nafikiri umewathibitishia sasa. Wanatoka kila upande. Wanatumia riziki zao. Wanafanya kila kitu, kujitahidi kufika kwenye mikutano, kufanya yote wawezayo, kwa kuwa wameipata ile Lulu ya thamani kuu. Mambo mengine ni madogo sana. Wabariki, Baba.

356 Kwenye jukwaa hili, asubuhi ya leo, Bwana, kuna leso. Huenda itawabidi baadhi yao kuondoka leo, kabla ya ibada ya uponyaji usiku wa leo. Ee Mungu wa Milele, angalia chini. Ninajua Wewe upo hapa, umetiwa utaji. Nami ninatuma vipazia hivi vidogo, Bwana, vinavyoitwa "leso," na "aproni," na "vijibuti" kwa ajili ya watoto wachanga. Nami ninavituma kama ishara ndogo za vipazia, kwamba Neno Lako limehubiriwa juu yake asubuhi ya leo, na, kama mwaminio, ninaweka mikono yangu juu ya hizo, mwili wangu, ikionyesha kwamba ninaliamini. Na, kwa imani, kila mtu kwenye jengo hili anafanya vivyo hivyo, Bwana. Jalia wagonjwa wapone.

357 Unaweza kulipiga Ne—Neno kutoka hapa, Bwana, kama vile yule mpiga fidla wa kale alivyofanya kwa ile fidla, litimize, Bwana. Lifanye liimbe tuni sahihi, uta ukiwa mkononi mwa Bwana, ndipo tutamwona amesimama akionekana dhahiri.

358 Jinsi ambavyo hapana shaka watu hao walifikiri siku hiyo, wakati wasingeweza kutoa chochote, wakati hawakutoa kitu kwa ajili ya ile fidla ya kale. Hawakuitaka. Wasingetaka kuwa nayo nyumbani mwao. Lakini mara ilipochukuliwa na mtu ambaye angeweza kuitumia kwelikweli, ndipo basi waliuza kila walichokuwa nacho, kuipata. Walikuwa wakizozana na kuipigania. Ilikuwa imechelewa sana wakati huo.

359 Ndivyo itakavyokuwa wakati mmoja wakati Baragumu ya Bwana itakapopigwa, hakutakuwako na wakati tena. Wale waliokuwa wameangaliwa na kudhihakiwa, waliosimama mbele ya pazia lililokuwa limefunguliwa na kuona Neno la Mungu limedhihirishwa (*wengine* watapiga mayowe walipate, lakini, kama Wewe ulivyosema, "Itakuwa imechelewa sana wakati huo"), waliingia kwenye Karamu ya Arusi, *nao* waliachwa nje mahali palipo na kulia, kuomboleza, na kusaga meno.

360 Msaidie kila mtu kuamini, asubuhi ya leo, Baba; pasua kila pazia la uchoyo, kila pazia la kutokuamini, na kumwona Mshindi Mkuu akifunuliwa mbele ya waaminio. Kwa kuwa, "Loo, Mimi niko pamoja nanyi daima, hata ukamilifu wa dahari. Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, hata hivyo ninyi mtaniona." Jionyeshe Mwenyewe miongoni mwetu, Bwana, kama vile ulivyokuwa ukifanya. Daima dumu hivyo mpaka tutakapoonekana mbele Zako, wakati en morphe itakapobadilishwa na Wewe uwe tena Mwana wa Adamu, na Mwana wa Daudi. Tujalie, Bwana, kwa Jina la Yesu Kristo.

Wakati tumeinamisha vichwa vyetu, sote katika maombi.

361 Sijui leo kama wapo baadhi hapa ambao. . .ndani ama nje. Hakuna njia ya kuleta wito wa madhabahuni hapa, kwa kuwa hapana nafasi. Lakini sijui, kwa uaminifu, hivi mnaamini hili kwamba ni Kweli? Mnaamini kwamba katika siku hii tunayoishi, na machafuko haya yote na wakati wa kisayansi kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, katika siku za Musa, siku za Kristo, ambapo Mungu, yule Baba mkuu wa sisi sote tuliozaliwa katika Yeye, anasimama miongoni mwetu leo?

362 Nguzo hii ya Moto inayoonekana ambayo imethibitishwa kisayansi, miaka mingi iliyopita, kama mvulana mdogo, ilisema nami huko nje na kuniambia ningeishi papa hapa, kile ambacho kingetukia. Kuwaambia juu ya jambo hilo, na kisha Hiyo. . . Siku moja huko chini mtoni, kabla ya huduma kuanza, uamsho wa kwanza, Yeye alijitokeza angani, akajitambulisha Mwenyewe na akatoa lile agizo. Miaka hii yote nimelificha moyoni mwangu, nikimficha Kristo, Nguzo ile ile ya Moto ikitafsiri Neno, kama ilivyoahidiwa. Tuko katika siku ya mwisho, kule Kuja kabisa kwa Bwana. Na kama ukijikuta nje ya pazia hilo, ambalo ni mauti kukaa nje yake, je! waweza kwa imani, asubuhi ya leo, kusema, "Kwa msaada wa Mungu. Na kwa msaada Wako, Bwana, ninataka kupasua nipitie kwenye pazia hilo. Ninataka kufika mahali ulipo Wewe, kuona Neno lote la Mungu."

363 Usijaribu kuwa Musa. Usijaribu kuwa Haruni. Usijaribu. Kuwa tu jinsi ulivyo, bali uwe Mkristo.

364 Je! mngeweza, huku vichwa vyenu vimeinamishwa, kumwinulia Mungu mikono, useme, "Bwana Mungu, nisaidie niingie ndani ya pazia"? Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hilo ni, hebu angalieni tu mikono hiyo!

365 Huko nje, kumbukeni, huenda nisiuone mkono wako kamwe. Haininii—hakuna faida sana kwangu kuuona, hata hivyo; ni, Mungu. Inaninii tu, kwangu mimi, inanifanya tu nione ya kwamba Mbe—Mbegu imeangukia mahali fulani, na, bali Mungu anauona moyo ulio halisi.

366 Kama kuna wowote wengine ambao hawakuinua mikono yao, wangetaka kuiinua sasa, inueni mikono yenu na mkumbukwe katika maombi. Inueni mikono yenu. Mungu akubariki. Hilo ni zuri. Mungu akubariki.

367 Baba, tunaomba leo ya kwamba hawa, Bwana, ambao hawajavuka pazia lile. Wanasimama huko nje kama Israeli; wanaangalia. Wanaamini, bali hawajapita Hili bado, wapate kuona ile Nuru kuu ya Shekina, ya kiroho na ya kimwili pia, zaidi sana hivi kwamba jicho la kimitambo la kamera linaendelea kupiga picha; majuma mawili tu yaliyopita, ilipigwa tena. Unajifunua Mwenyewe, Bwana, Mungu aliye Mkuu akifunuliwa kwa mwaminio; angali amefichwa kwa asiyeamini, bali amefunuliwa kwa mwaminio.

Naomba wapite, leo, Bwana, waone fahari Yake kuu na Utukufu. Jalia mioyo yao ibadilishwe kabla hata hatujarudi kwenye kanisa hili usiku wa leo. Jalia wote wajazwe na Roho Wako, Uwepo Wako. Bwana na aichukue imani hiyo waliyo nayo, aiangaze katika Neno; jalia ile tuni irudi, "Umechaguliwa, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kuamini jambo Hili. Amini, ewe mwanangu, na uokolewe."

368 Baba, Mungu, tunawakabidhi mikononi Mwako sasa, tukitambua hakuna jambo lingine tunaloweza kufanya. Yote yako Kwako sasa, Baba. Ninawakabidhi Kwako. Katika jina la Yesu Kristo, Mwanao. Amina.

Nampenda, nampenda
Kwani. . . alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

369 Je! Mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Wa ajabu, wa ajabu, Yesu kwangu
Mshauri, Mfalme wa Amani, Yeye ni Mungu Mwenye Nguvu;
Yeye ananiokoa, ananilinda na dhambi yote na aibu,
Wa ajabu, Mkombozi wangu, Jina Lake lisifiwe!

Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, sasa nimepatikana, huru na hukumu,
Yesu anatoa uhuru na wokovu mkamilifu;
Ananiokoa, ananilinda na dhambi yote na aibu,
Wa ajabu ni Mkombozi wangu, Jina Lake lisifiwe!

Loo, wa ajabu, wa ajabu, Yesu kwangu
Mshauri, Mfalme wa Amani, Yeye ni Mungu Mwenye Nguvu;
Loo, Yeye ananiokoa, ananilinda na dhambi yote na aibu,
Wa ajabu, Mkombozi wangu, Jina Lake lisifiwe!

370 Ni wangapi wanaomwona Yeye amesimama, yule Mshindi Mkuu, Neno lililofanyika mwili, akifunuliwa mbele zetu; Alfa, Omega; Yeye Aliyekuwako, Aliyeko, na Atakayekuja; Shina na Uzao wa Daudi; alikuwa ni Mwana wa Adamu, Mwana wa Mungu, Mwana wa Adamu, Naye atakuwa ni Mwana wa Daudi? Unaamini kwa moyo wako wote? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Akijifunua Mwenyewe katika kila wakati, akiletwa kwa mwaminio, akijificha katika mwili wa binadamu kutoka kwa asiyeamini. Yeye amefichwa nyuma ya pazia. Mungu na apasue kila pazia, na tumwone jinsi alivyo!

Yesu huvunja kila pingu,
Yesu huvunja kila pingu,
Loo, Yesu huvunja kila pingu,
Anapokufanya huru!

Ng'ambo ya pili ya Yordani,
Katika mashamba matamu ya Edeni
Ambako ule Mti wa Uzima unachanua,
Kuna raha kwangu.

Yesu huvu-. . .

Hivi hamtaki kuuvuka Yordani sasa? Si ni muda mrefu wa kutosha jangwani? Hebu na tuvuke tuingie kwenye ahadi!

Yesu anavunja kila pingu,
Yesu anavunja kila pingu,
Loo, alipokuweka huru!

371 Na tuinue mkono wetu sasa

Mimi daima, nitamsifu,
Mimi daima, nitamsifu,
Mimi daima, nitamsifu,
Kwa kuwa Yeye huniweka huru!

372 Amina! Hilo haliwafanyi mjisikie vizuri? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Loo, jinsi lilivyo la ajabu! Ni ajabu jinsi gani, sivyo, basi? Hebu na tupeane mikono mmoja kwa mwingine sasa, tukisema:

Yesu anavunja kila pingu,
Yesu anavunja kila pingu,
Loo, Yesu anavunja kila pingu, (Mungu akubariki, ndugu)
Loo, na anakuweka huru!

Mimi daima, nitamsifu, (Mungu Mwenye Nguvu)
Mimi . . . ("Yeye yule jana, leo, na hata milele," alibadilisha tu umbo Lake.) . . . msifuni,
Mimi daima, daima nitamsifu,
Kwa kuwa Yeye (ameniondolea kanuni zote za imani) kuniweka . . . (kuamini Neno Lake)

373 Loo, hivi hamwezi kusikia Fidla ya Bwana huku, uta juu ya Neno hili? Ni yeye yule jana, leo!

Mimi daima, nitamsifu,
Mimi daima, nitamsifu,
Mimi . . . (Yeye, lile Neno!) . . . daima, daima nitamsifu, (Yeye alifanya nini?)
Kwa kuwa Yeye aliniweka (nyuma ya pazia) huru!

374 Mungu asifiwe! Ninampenda. Hivi hamumpendi? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hii si ni ya Kimbinguni?

["Amina."] Ninapenda hizo sifa za Neno, mnaona, kama tu Roho Mtakatifu katika njia hiyo tamu, nyenyekevu. Na—napenda tu jambo Hilo. Loo, wazia tu!

> Ng'ambo ya pili ya Yordani, (ninakaribia huko sasa)
> Katika . . . matamu (kusikopatikana na mauti) ya Edeni, . . . (Nitapata nini kule?)
> Ambako ule Mti wa . . . (ambao ulikuwa katika bustani ya Edeni) unachanua,
> Kuna raha kwangu.

375 Mnataka kwenda? Yeye huvunja kila pingu.

> Yesu vunja (kila mapokeo) kila pingu,
> Yesu vunja kila pingu (madhehebu yote, kanuni zote za imani),
> Vunja kila mnyororo,
> Naye anakufanya huru!

376 Mungu asifiwe! Ninampenda tu. Si ajabu Isaya alisema, "Yeye ni Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele, Wa Ajabu!"

> Wa ajabu, wa ajabu, Yesu kwangu
> Mshauri, Mfalme wa Amani, Yeye ni Mungu Mwenye Nguvu;
> Loo, Yeye ananiokoa, ananilinda na dhambi yote na aibu,
> Wa ajabu, Mkombozi wangu, Jina Lake lisifiwe!

377 Loo, jamani! Hilo linachangamsha moyo wangu. Jinsi Yeye alivyo wa ajabu! Ninawaambia, hakuna mwisho wa Jambo Hili. Hilo, niliingia kwenye hili miaka thelathini na mitatu iliyopita, nikijisikia jinsi hii. Na kama Yeye akikawia, siku moja nitayafunga macho yangu, nitatoka namna hiyo hiyo. Amina!

> Wa ajabu, wa ajabu, Yesu kwangu
> Mshauri, Mfalme wangu wa Amani, Yeye ni Mungu Mwenye Nguvu;
> Yeye ananiokoa, ananilinda na dhambi zote na aibu,
> Wa ajabu, Mkombozi wangu, Jina Lake lisifiwe!

378 Ningekaa hapa siku nzima, kwenye jambo Hilo. Paulo alisema, "Kama nikiimba, nitaimba katika Roho." A-ha. "Kama nikihubiri, nitahubiri katika Roho. Nikitembea, nitatembea katika Roho. Nikizungumza, nitazungumza katika Roho." Hebu kila kitu kitendwe katika Neno na Roho. Naam, bwana. Amina! Yote ni Kweli ya Mungu.

379 Ninamwona, Mungu Mwenye Nguvu, amefunuliwa. Ninamwona akivuta kuondoa kanuni za imani, madhehebu;

anawavuta kuwaondoa we—wenye kushuku, mipango ya elimu, na kila kitu; anasonga mbele, kasimama pale. Mnafikiri kanuni za imani zingemshinda? Mnafikiri madhehebu yangemshinda? Mnafikiri Baraza la Ulimwenguni lingemshinda? Yeye alishinda kila kitu, akavunja kila mnyororo, akapasua kuzimu kukafunguka; akauvunja ule muhuri, akaingia katika Patakatifu pa patakatifu; akajifunua Mwenyewe kwetu, akiwa ni Neno, yeye yule jana, leo, na hata milele. Amina. Ninampenda.

380 Sasa, mpaka tutakapokutana alasiri ya leo, tunataka kufanya jambo moja, hilo ni:

> Peleka Jina la Yesu,
> Mwana wa huzuni na mashaka;
> Litakupa furaha na faraja,
> Loo, peleka kokote uendako.
>
> Jina la thamani, ni tamu jinsi gani!
> Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
> Jina la thamani . . . (Naam, nimeyapata, tayari.) . . . ni tamu jinsi gani!
> Tumaini la duniani na . . . ( . . . ? . . . )

381 Shetani akijaribu kukujaribu, ya kwamba huangalii jambo sahihi, mwelekeze kwenye Neno kama Yesu alivyofanya. Mnaona? Mnaona? Amina.

> Katika Jina la Yesu nasujudu,
> Ninamwinamia miguuni Pake,
> Mfalme wa wafalme Mbinguni tutamvika taji,
> Safari yetu ikomapo.
>
> Jina la thamani, ni tamu jinsi gani!
> Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
> Jina la thamani, ni tamu jinsi gani
> Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

382 Billy atakuwa ndani, yapata saa kumi na mbili, akisambaza kadi za maombi kwa wale wanaotaka kuja kwenye mstari wa maombi. Nafikiri afadhali tufanye jambo hilo. Hatukuwa tufanye hivyo, lakini, kwa kuwa sisi ni wengi, afadhali tufanye jambo hilo, mnaona.

383 Sasa mkumbukeni Yeye! Mdumisheni siku zote niani mwenu, moyoni mwenu. Kokote uendako, unaona, mdumishe Yesu niani mwako.

> Peleka Jina la Yesu (sasa sikilizeni) nawe,
> Kama ngao kutokana na kila mtego; (ni jambo gani hutukia?)
> Majaribu yakikuzunguka, (inabidi tufanye nini?)
> Litamke tu Jina hilo katika maombi.

Jina la thamani, Jina la thamani, Loo, ni tamu
jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, ni tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

384 Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa. Nitamwomba mchungaji kama atakuja na kuliruhusu kusanyiko liondoke. Ndugu Neville, Mungu akubariki, Ndugu Neville.

*KUFUNULIWA KWA MUNGU* SWA64-0614M
(The Unveiling Of God)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 14 Juni, 1964, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org